ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.

10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.
11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

46.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
49.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
64.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
65Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

66.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
67.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
68. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
69.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
70.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
71.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
72.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
73.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
74.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
75.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
78.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Nane – Tarehe 29 Januari, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HOJA BINAFSI YA MJUMBE

Mhe. Spika: Kama tulivyoondokeana jana Waheshimiwa Wajumbe kwamba muda wetu unatukwaza sana na tumeondoa kipindi cha maswali leo hii asubuhii ili kuipa nafasi hoja hii kupata michango ya ziada. Tulisema kwamba tukitumia masaa yote matatu kuanzia sasa hadi saa sita basi tunamudu kusikiliza Wajumbe 12 tu kwa kuwapa dakika 15 kila mmoja. Sasa tueke dondoo zetu vizuri twende moja kwa moja kwenye hoja yenyewe historia sawa tunaweza kuzungumza kidogo, lakini tusipoteze lengo la kwenda kwenye hoja yenyewe.

Lakini ningependelea zaidi kama kuna jambo limeshazungumzwa ingawa ina ugumu wa kuepuka na hiyo basi tujaribu kutafuta jambo jipya na wapo baadhi wa Wajumbe ambao walionesha katika maombi yao kwamba mimi nina jambo jipya ambalo kwa kweli sijasikia Wajumbe kulizungumza na nitapenda kwa mnasaba huo basi nianze na huyo alieniomba muda mchache pengine dakika 10 au 15 zitamtosha kama alivyoeleza ili afanye hivyo halafu itakuwa inatupa muongozo wa kuweza kuleta yale mambo mapya mapya. Basi tumsikilize Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi atasema yale kama alivyoahidi kwa muda mchache na baada ya hapo tumsikilize Mhe. Nassor Ahmed Mazrui.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi ya mwanzo leo asubuhi sitofika hata dakika kumi mimi tano zinanitosha.

Mhe. Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutuajaalia kufika hapa tukiwa wazima wa afya na siha, kupitia kwako Mhe. Spika, ninayo yafuatayo ambayo naomba mtoa hoja ayapate.

Nianze kusema kama alivyotwambia Mhe. Haji Faki Shaali majuzi kama “likipita zumari vinanda tena havina ladha” na limeshapita zumari la Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora, Mhe. Waziri wa Elimu, Utamaduni na Michezo, Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji, Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na kadhalika. Kwa hivyo kifirimbi changu nakizuia hapo.

Mhe. Spika, nakubaliana na maelezo ya kina aliyotoa Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora na Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji yeye akiwa mjumbe wa Kamati kuu na pia ni Mjumbe wa Chama cha Mapinduzi, sina ziada ya hapo na naomba mtoa hoja ayazingatie kwa kina kwa maana ndio maazimio yetu ya Butiama na atukubalie tupate kusonga mbele.

Mhe. Spika, msisitizo kwangu mimi haja ya kuwepo kura ya maoni ya moja kwa moja ni muhimu sana tusihofie mawazo ya Wazanzibari hilo ni muhimu sana kwangu mimi kura ya maoni ya moja kwa moja ili wananchi wa Zanzibar waweze kutoa ridhaa yao juu ya mfumo ambao wao wanahisi unafaa katika utawala na usimamizi wa siasa katika nchi yetu, tusihofie maoni yao.

Mhe. Spika, mimi ninaamini Wazanzibari wanaielewa nchi yao vyema na wanaielewa historia yao wanaelewa yanayopita kwenye macho yao na naamini watafanya maamuzi ya busara hawataki kufindishwa na naamini watatuweka pahala pazuri zaidi. Kwa maana hata neno maridhiano linatokana na neno ridhaa kwa hiyo ridhaa yao kupatikana ni muhimu sana.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba kwangu mimi ni muhimu zaidi taratibu hizi za kupata ridhaa kwa wananchi Wazanzibari zikamilike kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 hilo ni muhimu sana na naungana na wenzangu kwamba shughuli hiyo iachiwe Serikali ya Mapinduzi kukamilisha utaratibu huo kabla ya Uchaguzi Mkuu. Kwangu mimi ni hatari sana kuingia kwenye Uchanguzi Mkuu bila ya kuweka hali hii vizuri.

Kwa hiyo, naungana na wenzangu waliochangia kwa upande wangu huku kwamba ni muhimu sana ridhaa ya wananchi ipatikane mapema kabla ya uchaguzi mkuu maamuzi hayo yafanyiwe kazi na tusende kwenye Uchaguzi Mkuu bila ya kupata maridhiano sahihi na maelekezo ya wananchi wa Zanzibar.

Nimalizie Mhe. Spika, kwa kumpongeza sana Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia akiwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa ujasiri wake na upeo wake wa tangu alipoteuliwa kutaka chama chake kukaa na Chama cha Upinzani cha *CUF* kutafuta mustakbali mwema kwa ajili ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla. Nimpongeze pia Mhe.Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Barza la Mapinduzi na Maalim Seif Sharif Hamad kwa maamuzi yao ya busara.

Mhe. Spika, mimi nakushukuru sana na namuomba mtoa hoja ayazingatie aliyopewa ayapime kama alivyosema Mhe. Fatma Fereji na hatimae naamini atakubaliana na mawazo yaliokuwa ya wengi ili tumalize shughuli hii ya leo

kwa salama na bila ya mikwaruzano na mivutano isiyokuwa na haja. Mhe. Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mheshimiwa umetuwekea muongozo unaowezesha na wengine wakapata nafasi. Bila ya kukawia na haraka kidogo naomba sasa nimkaribishe Mhe. Nassor Ahmed Mazrui na baada ya hapo tumsikilize Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: *"Bismillah Rahmani Rahim Wasalatu Wasalam Ala Rasulillah alayhi Wasalam".*

Mhe. Spika, naomba kutoa nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kujaalia siku ya leo hii ya Ijumaa asubuhi kuwa ni mtu wa pili katika kuchangia hoja hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Namshukuru Mwenyezi Mungu ambae ameumba mbingu na ardhi na vyote viliomo katika dunia hii wakiwemo binaadamu, ambao binaadamu amewapa umbo zuri na akili ya kutosha ya kuweza kung'amua lipi jema na lipi baya na kutokana na hayo basi atotenda mema Mwenyezi Mungu atamlipa hata akiwa ni kidogo kama mdudu chungu, na mtenda mabaya vile vile atamlipa vile vile.

Mhe. Spika, dua ambayo kwamba kila siku asubuhi unaisoma hapa ni dua ambayo kwamba inaelezea vyovyote vile na Mwenyezi Mungu *inshalla* dua hii ndio anayoitakabalia.

Mhe. Spika, hoja hii ambayo imeletwa kwetu hapa na Mhe. Abubakary Khamis ni hoja ambayo kwamba italeta hatma ya Mzanzibari. Mhe. Spika, historia ya Zanzibar imeonesha wazi kwamba chaguzi zote zilizofanywa kabla ya Mapinduzi chaguzi tatu na baada ya Mapinduzi changuzi tatu zimetoa picha halisi ya namna gani Uchaguzi wa Zanzibar ulivyokuwa unakumbwa na kugubikwa na machafuko ya hali ya hewa na kuwa watu kuwa roho juu juu na kwa kweli uchaguzi unaleta mashaka makubwa sana. Hii ni historia ya nyuma ambapo vyama vingi viliundwa vikiwa chini ya utawala wa Muengereza na utawala wa kislutani ambapo wananchi wote walichanganyikiwa na hapo ndipo ulipoanza mzizi wa fitina.

Mzizi wa fitina huu hatuwezi sisi kuendeleza lazima Baraza hili lako leo liukate mzizi wa fitina huu. Muengezea maisha akitawala huwa anawa- *divide* watu. Kwa hiyo ile *division* imekuwa *so dip* mpaka leo bado inatuathiri. Kama anavyosema Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muunngano wa Tanzania kwamba tusiwe watu wa historia. Historia ibaki kama historia lakini tuandae mipango yetu ya kufanya ili tusiwe watumwa wa historia ili kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, tukiangalia utakuta kwamba mazungumzo ya maridhiano baina ya Dr. Aman Abeid Aman Karume na Maalim Seif Sharif Hamad Sheikh Mjaka ambayo yamefanywa Novemba, 2009, haya mazungumzo kwamba Mhe. Spika, naomba kuyaombea dua na naunga mkono moja kwa moja bila ya kujali kilichozungumzwa katika mazungumzo haya kama vile sikuhoji wala sitohoji mazungumzo waliyokaa hayati Abeid Aman Karume na hayati Mwalim J.K Nyerere wakaleta Muungano huu mpaka leo tunao basi sihoji vile vile kwa Mhe. Aman Abeid Karume na Mhe. Maalim Seif Shariff.

Mhe. Spika, mimi binafsi na naamini wananchi wengi wanamuamini na wana imani na kwa dhati na Dr. Aman Abeid Karume vile vile wana imani na wanamuamini Maalim Seif Sharif Hamad na ndio maana tukasema kwamba maridhiano haya na sisi tumeyaridhia na tunaamini viongozi wetu wanayoyazungumza ni kwa manufaa yetu na kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Spika, tunapotaka kujali suala la hoja hii tusimwangalie mtu fulani au chama fulani au mwahala fulani. Lakini tuangalie mustakbali wa nchi yetu. Tukianza kuangalia sura ya mtu tukaanza kumuogopa Maalimu Seif Sharif Hamad kuwa tuna mashaka mashaka nae tukaanza kumtilia mashaka Dr. Aman Abeid Karume hatufiki mwahali popote. Lazima turidhiane lazima tushikamane tuwe kitu kimoja na tuaminiane ili tuweze kuwa na msingi bora na msingi madhubuti wa kuweza kuleta mazungumzo haya mpaka kufikia hatima yake kuleta hatima ya kweli ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, wana siasa ndio sisi na sisi ndio tunao jukumu kubwa kwa wananchi wetu. Wananchi wetu wanaangalia nini sisi tunawaambia ili wafate. Kwa hivyo, tujue kwamba hii ni dhamana “ikiwa kiongozi anajaribu kuwaacha anao waongoza wapate matatizo kwa ajili ya uongozi wake kwa mfano uchaguzi unakuja watu wanapigwa wanaharibiwa mali zao wanaadhibiwa halafu yeye anakuwa Rais. Basi kiongozi kama huyo ni matatizo tuwe na viongozi ambao kwamba wanaingia madarakani wananchi wanakuwa na furaha wamepiga kura kwa furaha na uchaguzi umekwenda kwa haki uhuru na amani”.

Mhe. Spika, hilo ndio suala muhimu na hilo ndilo tatizo kubwa la Zanzibar wakati wa uchaguzi kila mtu roho juu juu. Wasi wasi wangu ni kwamba wakati wa uchaguzi usije ukawa sawa sawa na wakati wa kupiga kura ikiwa watu wako roho juu juu na ikiwa watu wengine hawaendi kupiga hii tutakuwa tunajidanganya, ndio tunazidi kupotea njia na Mwenyezi Mungu atatuhuku kwa hayo *“Kullu Kum-rai*. Kila mtu ni mchungaji na kila mtu ataulizwa kwa anachokichunga na Mwenyezi Mungu kasema “kuwa lenye kheri na nyinyi ni kusuluhishana”. Mkiweza kusuluhishana basi hilo ni kheri kwenu na ikija kheri

kwenu basi hapo ndipo itakuja kheri ya kweli kweli nchi yenu itaneemeka na itakuwa na neema kubwa watu wataondokana na wasi wasi.

Mhe. Spika, maslahi ya nchi yetu kwanza kiliko maslahi ya mtu yoyote wala chama chochote wala upande wowote wala mtu yeyote wana siasa lazima tusome nyakati tukaposhindwa kusoma nyakati tutakuwa hatubadiliki na mwana siasa ambae habadiliko basi hafahamiki.

Mhe. Spika, kuimarika kwa Zanzibar Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiimarika ndio kuimarika kwa Muungano. Serikali ya Zanzibar ikiwa lege lege watu hawafahamiani kazi haziendi mitafaruku ya huku na kule na Muungano vile vile utakuwa unalega lega. Muungano vile vile muhimili wake mkubwa ni kuona kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko imara inafanyakazi zake vizuri na hapo Muungano utaweza kuimarika, bila kukubalika kifikra na kimawazo hatuwezi kwenda mbele.

Uchaguzi wa mwaka 2010 unaokuja kama haukuwa uchaguzi wa amani, huru na haki basi tuna matatizo makubwa sana na yanaweza kuwa makubwa sana haya kuliko yaliopita nyuma, wanasema "yaliopita si ndwele tugange yajayo". Tuhakikishe Mhe. Spika, tunakwenda kwenye uchaguzi huo tumejitayarisha kwa upole au kwa kadiri ya uwezo wetu kwamba hakutatokea matatizo mengine yoyote ambayo kama yametokezea kabla ya hapo, viashiro vyote vya kuvunjika amani lazima vifikiwe viondoshwe ili tuweze kwenda kwenye uchaguzi wa haki na huru na amani.

Mhe. Spika, mfumo wa uchaguzi ubadilike, sio ule uliotolewa mwaka 1995 mpaka hivi leo. Serikali ya Umoja wa Kitaifa tuifahamu maana wengine wanachanganya Serikali ya Mseto hii Serikali ya Mseto ni kitu mbali na *definition* yake ni mbali na Serikali ya Kitaifa ni kitu mbali.

Mhe. Spika, mimi ni mfanyabiashara na safiri sana kwa mwaka siku 90 mpaka 120 mimi nakuwa nje ya nchi ninapotua tu Uwanja wa Ndege wa Zanzibaar hali yangu huanza kusononeka nikiwa kwamba kisiwa hiki ni kisiwa ambacho kinaweza kuendelea na ikawa ni nyota ya Afrika. Lakini hali ninayaona kabisa hainiridhishi na inanisononesha sana, nasononekana kama anavyosononeka Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kuhusu mizozo hii ya Zanzibar.

Mhe. Spika, miaka kiasi 12 iliyopita Mhe. Ali Juma Shamuhuna shahidi wangu tulikwenda kutembelea kisiwa cha Mauritius na yeye akiwa ni kiongozi wa msafara mimi nilikwenda mara tatu mara moja nilifatana na yeye ni kiongozi wetu wa msafara na mara ya pili nilikwenda mimi kama ni kiongozi wa msafara na Bodi ya Tanzania na tatu nilikwenda katika ufunguzi wa Air Tanzania kutoa katika kiwanja cha Mauritius.

Mhe. Ali Juma Shamuhuna ni shahidi tulipokwenda katika mkutano wa waekezaji wa Mauritius Waziri mwenzake alitwambia kwamba nyinyi mlipata uhuru wenu au Mapinduzi yenu mwaka 1964 sisi Mauritius tulipata uhuru wetu mwaka 1968. Lakini tuangalieni sisi tulipo na mjiangalie nyie mlipo. Sisi tulichagua *the write pass* na nyie mkachagua *wrong pass*. Na hata Mhe. Waziri Ali Juma Shamuhuna alipotwambia kwamba tumsikilize mwenyewe ……

Mhe. Spika: Mhe. Mujumbe umebakiwa na dakika tatu.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika, maendeleo yalipotikana Mauritius hayana mfano na kisiwa cha Mauritius kiko mbali sana na Bara la Afrika ukilinganisha na Zanzibar. Zanzibar iko chini ya Bara la Afrika. Lakini tumeshindwa kwa sababu hatuna nafasi ya kuzungumzia maendeleo ya kweli ya Zanzibar tunagombana kila siku ugomvi hawishi hatufahamiani haya Mhe. Spika, sasa hivi ni wakati wa kuyaondoa. Hofu juu ya suala la kwamba Sera ya chama hiki na sera chama hiki tafauti hii naomba Wajumbe kabisa waiondoe, leo Rais Barak Obama kule kapata kura nyingi kama Rais wa Marekani na Sera yake nzuri sana lakini akienda katika *House* sera yake haipiti mpaka leo sera ya elimu haijapita hana viti ana kura nyingi huku lakini hana vituitusitarajie kuwa hali itakuwa hivi kila siku. Rais anaweza kuwa na kura nyingi lakini viti katika Baraza vikawa tafauti.

Mhe. Spika, naomba kumalizia kwa kusema kwamba sisi Wanzanzibari na hasa sisi viongozi katika Baraza hili tuna jukumu kubwa sana kwa Mwenyezi Mungu siku ya leo ikipita bila ya kuwa na msimamo madhubuti wa kuweza kuona kwamba matatizo haya kabisa tunayazika na hayazuki tena kwa maendeleo ya kweli kabisa katika nchi yetu basi tutakuwa tunalaumiwa kwa wananchi wetu na kwa Mwenyezi Mungu vile vile.

Mhe. Spika, juzi na jana Rais wa Afghanistan kafuta mawaziri wote ambao walikuwa Wataliban kawaondoa kakaa nao kaongea nao Watalibani waunde Serikali ya pamoja jana mjini London katika mkutano wa kimataifa nia yake ya kuunda Serikali ambayo kwamba atawa- *include* serikali yake. Angalieni vita vya Afghanistan mataifa ya dunia nzima yamekuwa *involved* angalieni uchungu wa Afghanistan lakini maendeleo hayapatikani. Tukiangalia katika nchi za Ulaya Canada imo katika Serikali ya Umoja wa kimataifa na hakuna mizozo yoyote na *alhamdulillah* nchi zinakwenda. Kwa hivyo, Afghanistan leo watashindana na Wataliban seuze sisi ndugu tunajua na hakuna kubwa mno isipokuwa ni machache tu ya kuweza kuelewana.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, namaliza kwa kusema kwamba biashara zetu zitakuwa uchumi wetu utakuwa na wawekezaji wataongezeka ikiwa tutakuwa na amani na utulivu katika nchi yetu hatufikii malengo hayo kama hatukuwa na Serikali ya Umoja wa kimataifa. Kuna haja kubwa ya kuhusu Zanzibar yetu na Wazanzibari wote kuungana kwa pamoja bila ya kujadili chama itikadi kabila rangi, dini mwanaume au mwanamke lugha au asili fikra mtazamo, utajiri au umasikini. Tukiweza kufikia hapo Zanzibar itakuwa ni *Star of African*. *Asalama alaykum warahmatullah wabarakatuh*. (*Makofi*).

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Kwanza na mimi nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kutoa maoni yangu kutokana na hii hoja ya Mhe. Abubakary Khamis.

Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Rais wangu Aman Abeid Karume na pia namshukuru Maalim Seif Sharif Hamad kwa kukaa pamoja na kuleta mustakabali mzuri wa uleta amani katika nchi yetu.

Mhe. Spika, wengi Wajumbe hapa wametoa mifano ya nchi za wenzetu kwa lengo na nia nzuri tu. Lakini Mhe. Spika, mtu mmoja kusimama na kusema kwa mfano Mauritius na nchi nyengine hiyo Mhe. Spika, haijawa ni kigezo cha kufata nchi za wenzetu.

Mhe. Spika, maoni yangu mimi kama tuna nia nzuri sana kabisa kutokana na kuiunga mkono hoja hii basi mimi ningeona tusifanye haraka tukaunda tume tukenda Mauritius, tukenda na Singapore ili baadae tukaja hapa. Mhe. Spika, hii ina maana kwa sababu unanukuu sehemu ambayo iliyokuwa tayari wenzetu wanavitu kama ambavyo hoja hii iliyokuja hapa.

Mhe. Spika, hili suala ni zito tusilione *simple* kuna watu wengine wanacheka wengine wamelia si kitu cha masihara na hasa tukiangalia historia yetu huko nyuma historia yetu tulivyotokana nayo na leo Mwenyezi Mungu anatuleta katika meza, sasa mimi ningeomba Mhe. Spika, si vibaya kabisa Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej aliposema jana mimi nilifurahika kabisa nikasema na mimi nitakapopata mchango wangu nitoe maoni yangu na sisi tuunde tume kabla ya kulikubali hili suala, twende Singapore tuangalie vipi wenzetu mfumo huo, alitaja kila jinsi Mheshimiwa jana. Alisema kuna vyama vingi kabisa makabila mengi na kila kabila lina lugha yake sisi leo Zanzibar makabila hayajfika mengi kiasi hicho, udini pia litaja, sasa hii ni nzuri sana mimi namuunga mkono Mhe. Fatma Fereji ni lazima tuwe na kigezo kilichokuwa halali kwa kuona sio kwa kusema.

Mhe. Spika, mimi nimsifu kaka yangu hapa Mhe. Waziri wa Nchi Katiba na Utawala Bora, nimsifu dada yangu Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na

Uwekezaji ameeleza vizuri sana kwa ufasaha kabisa, utulivu kabisa na wengine wenzetu walifurahi ndani yake na hata akaelekeza kuwa mswada huu uende vizuri kabisa. Mimi sikuamini, nilisema hapa kila nikijaribu kutaka kulitoa ili nilirushe huko, nilikuwa ninajiandaa hivyo, lakini Mwenyezi Mungu kawajaalia kaleta baraka nzuri halikutoka hili wala hakukutokea tatizo hilo. Tumekwenda vizuri sana Mhe. Spika.

Kutokana na hali hii wengi wetu tunakubaliana kuwa suala hili lirudi kwa wananchi likapate ridhaa kabisa halafu baadae turudi hapa tulipange yale tuliyokusudia. Tuwe na utaratibu mzuri kama uko wenzetu walivyokaa Butiama, walituletea suala hili kwa utaratibu mzuri. Kwa hivyo, na sisi tukubaliane nalo bila ya kuwa na pingamizi ya aina yoyote.

Lakini Mhe. Spika, humu nasikia, unajua sasa hivi tuna vyama viwili ambavyo tunasema ndivyo vyenye nguvu katika hii nchi yetu ya Zanzibar, lakini vipo vyama vyengine, hebu tuone ipo haja kabisa na wao tuwaingiza katika mustakabali huu, na wao wana haki yao kabisa na ikiwezekana tuweke sheria kabisa katika hizo nafasi za rais za kuchagua wapinzani na wao wachaguliwe moja kwa moja. Kwa sababu na wao wana haki au na wao walete vurugu, ndio maana yake hiyo, tuwaambie na wao walete vurugu ili nao waingie katika mustakabali huu? Lakini hapana, wao ni watu wastaarabu kabisa.

Jana Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii alimtaja mmoja Mr. Join a yeye aliingia katika urais taratibu tena kwa beni, sasa leo kwa nini tumnyime haki yake. Haya ni mawazo yangu kuona kuwa na wao washiriskishwe kabisa katika masuala haya ili na wao wajisikie kuwa na wao wamefanyiwa usajili wa kisheria kabisa na wao wakubalike.

Mhe. Spika, sitaki niondoe utamu, kaka yangu hapa kamanda wangu jemedari amemaliza leo kazi Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Mhe. Spika, hii hoja tusiogelee sana ndio yale kwa yale kama tulivyosema. Kwa mfano mimi nikitoa historia watu watalia sasa hivi hapa, sasa nasema bora mimi nisitoe au nitaharibu kabisa hii hoja. Kwa sababu historia tunayo. Mfano mdogo naomba kiti chako kiniruhusu.

Mfumo wa vyama vingi. Mhe. Spika, tulielimishwa tukaambiwa mfumo wa vyama vingi ni kupata utajiri, mimi nikasema minalfaidhina, kuwa leo tukikubali mfumo wa vyama vingi sisi masikini tuliokuwa shamba tutakuwa matajiri basi tukakubali Mhe. Spika, tukakubali na kushangiria kwa kofi na tukaambiwa chama kimoja kinaleta ukiritimba, kinajikusanyia madaraka, lakini mfumo wa vyama vingi utakuwa na mgawano wa madaraka. Chama cha *NCCR* Mageuzi sijakiona kuingia barazani ndio mgawano huo wa vyama vingi na wao wamo katika vyama vingi lakini sijasikia kuingia humu nasikia *CUF* na CCM.

Sasa ndio maana nikasema kwamba nina tahadhari kubwa sana, hoja imeniingia, hofu imeniingia kwa hili suala ambalo tunasema tuelekee huko kwenye serikali ya kitaifa na ndio maana mdomo wangu unakuwa mzito kama niliyebeba kontena kujibu au kukubali moja kwa moja. Kwa sababu ya hofu hiyo tu, na ndio maana nikasema kuwa nikiunga mkono suala zito, nisiunge mkono suala zito. Assa najiuliza nielekee wapi?

Mhe. Spika, inabidi sasa tu-*quote* maelezo ya wakubwa wetu na sisi tuegemee pale pale tuseme kuwa alivyosema Mhe. Ramadhan, Mhe. Samia, Mhe. Mansour basi na mimi naunga mkono. Ndio itavyokuwa hivyo. Lakini hili suala ni zito na uzuri wake kuwa sasa hivi sisi wawakilishi wote tunaelekeza huko kwa wananchi kwenye *grass root,* huko ndiko watakaotuelimisha kwa sababu mle kuna watu wengi kila mtu ana fikira zake, ana mawazo yake, sasa watapokaa pamoja akatuletea lile suala basi tunangojea nini sasa, ndio tutaamua tu.

Mhe. Spika, kaka yangu hapa alipokaa kitako amesifu na mambo ya biashara ndani yake, hata na mimi mfanyabiashara mzuri tu katika nchi hii lakini sionekani tu. Hilo ndio lengo tunataka nchi yetu lazima iinuke kibiashara, wale wafanyabiashara ambao wako ubavuni wadogo wadogo na wao tunataka wainuke, lakini kama tukisema nchi kama kutakuwa hakuna amani hiyo ni pahala popote biashara haitofanyika.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kama nilivyokwambia mawazo ya wazee wangu hapa niliyowajata hao mimi nakubaliana nao kuwa hoja hii ielekee kwa wananchi wenyewe watuelekeze tuje hapa tena tuifanye kazi haraka sana. Kwa hayo machache Mhe. Spika, sitaki kujichosha kabisa na mimi naomba nikae kitako. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk umeutumia vizuri muda wa dakika kumi wala hazikufika kumi na tano. Tumkaribishe Mhe. Zahra Ali Hamad na baadae tumsikilize Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu.

Mhe. Zahra Ali Hamad: Nakushukuru sana Mhe. Spika, Bismilahi Rahmani Rahim. Awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kunipa rizki ya pumzi na nikaweza kuzungumza mawili matatu Mhe. Spika, katika jambo muhimu hili ambalo linatukabili Wazanzibari.

Mhe. Spika, nataka nichukue fursa hii adhimu pia kumshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, Mhe. Mizengo Pita Pinda pale jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mhe. Mbunge wa Jimbo la Wawi, Mhe. Hamad Rashid ambaye pia ni kiongozi wa upinzani Bungeni, alipotaka kujua kuwa

Serikali ya Muungano wanayachukuliaje mazungumzo haya ya Wazanzibari mustakabali ambao wamefikia na wakaeleza kama jana ulikuwa unapelekwa kwenye Baraza la Wawakilishi.

Yeye Mhe. Spika, alimnukuu Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na akasema, “Mhe. RAis kauli yake tayari kaitoa kwa Watanzania wote na kasema yeyote yule ambaye anakebehi au kudharau mustakabali huu wa mazungumzo ambao umefikiwa na viongozi wakuu wa Zanzibar wa kisiasa basi mtu huyo inabidi apuuzwe na atengwe”. Kwa hivyo, nachukua fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri Mkuu lakini vile vile kumshukuru Mhe. Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia alionesha nia yake toka siku ya kwanza nadhani ilikuwa ni tarehe 30 Disemba, 2005 wakati alipolihutubia Bunge na kuona dhahiri kuwa Zanzibar tulikuwa tunakwenda sehemu ambayo haifai kwenda.

Mhe. Spika, pia nataka nimshukuru mtoa mada kwa kuleta hoja hii. Inaonekana Mhe. Abubakar Khamis licha ya kuwa ni msomi, mjuzi na mzoefu wa sheria ambaye amekomaa, lakini pia inaonekana ni mwanasiasa ambaye ana upeo wa kuona mbali. Kwa maslahi ya nchi Mhe. Spika, na watu wake bila shaka alikaa Mhe. Abubakar akatafakari, ni kitu gani ambacho tutaweza kuwarithisha vijana wetu, tutaweza kuwarithisha watoto wetu ikiwa tutaendelea kwenda kama hivi tunavyokwenda. Na akaleta hoja hii ili kuwe na upendo miongoni mwa wananchi, ushirikiano, amani, utulivu, mshikamano baina ya wananchi na kujenga maendeleo ya nchi kiuchumi, ustawi, utamaduni wa nchi yetu kwa jumla.

Mhe. Spika, Mhe. Abubakar ametuzindua Wazanzibari bila kujali itikadi ya vyama vyetu, bila ya kujali nafasi ambayo mtu anayo katika jamii kwa kuipongeza hatua ambayo wamefikia viogozi wetu Mhe. Rais wa Zanzibar, Mhe. Amani Abeid Karume na Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kwa kukaa kitako na kuacha tofauti ambazo wanazo na kufikiria yenye mwelekeo mzuri na mustakabal wa nchi yetu na watu wake.

Mimi Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa wa Baraza lako tukufu kuwapa nguvu viongozi wetu kwa hili ambalo wamefikia na tuwe tayari kuwaunga mkono kwa hilo.

Mhe. Spika, naomba kwa dhati kabisa kukubaliana na mtoa hoja ya kuwa fursa hii ambayo tunayo leo au fursa hii ambayo tumefikia ni fursa ya kipekee Mhe. Spika, na inahitaji kufanyiwa kazi kwa kuafiki yale mapendekezo yaliyomo kwenye hoja hii ili kujenga misingi madhubuti itakayoleta upendo, umoja, mshikamano na mashirikiano katika kujenga nchi yetu. Na mimi nakubaliana

kabisa kuwa tukiiacha fursa hii kuna uwezekano wa kurudi tena kwenye ile mitafaruk ambayo kwa kweli mimi sitaki kabisa kuikumbukia.

Mhe. Spika, sisi Wajumbe wa Baraza lako tukufu ni viongozi na kiongozi ana dhaima kwa wale ambao amemleta hapa kuwawakilisha lakini pia ana dhima mbele ya Mwenyezi Mungu. Tujijue kama sisi ni wachunga na kuna siku ya siku Mhe. Spika, tutakwenda kuulizwa juu ya kile tulichokichunga. Kwa maana hiyo basi, ni muhimu kama viongozi kujikumbusha na tukatathmini ni vipi wananchi wetu wanatutegemea na ni vipi wananchi wetu matarajio yao kwetu.

Mhe. Spika, sisi Wazanzibari ni Waisilamu asilimia kubwa na asilimia nyengine ni Wakiristo, kuna vitabu ambavyo wanaviamini na sisi tuna vitabu ambavyo tunaviamini, kuna hadithi na maandiko ambazo tunazifuata za Mitume na Maswahaba.

Kuna hadithi moja Mhe. Spika, naomba niinukuu ya Mtume (*SAW*) ambayo aliwaambia maswahaba wake kuwa, "haitakamilika imani yenu kati ya mmoja wenu kama hatompendelea Muislamu mwenzake yale ambayo anayapenda yeye kwenye nafsi". Huyo ni mtu mmoja mmoja sikwambii sisi kama viongozi ni vipi itaweza kutimia imani yetu kama Waisilamu, kama hatujawapendelea watu wetu yale ambayo tunayapenda, yanaturidhisha, yanatufurahisha, yanatuburudisha ndani ya nafsi yetu.

Mtoa hoja ana mapendekezo yake kadhaa katika katiba, kwenye kifungu cha 9(3), kifungu cha 39, 42 na 61 cha Katiba ya Zanzibar marekebisho ambayo yanakidhi haja na madhumuni ya hoja hii. Kwenye ukurasa wa nne *roman* nne mtoa hoja amependekeza Baraza liweke utaratibu utakaowezesha wananchi wa Zanzibar kushiriki katika kutoa ridhaa yao ya kuunga mkono mfumo wa serikali ya umoja wa kitaifa kwa njia ya maoni au kwa njia nyengine ambayo Wazanzibari kupitia kwa wawakilishi wao waliowachagua wataona inafaa.

Mhe. Spika, nimekaa toka siku ambayo nimeipata hoja hii kwa sababu naamini wale ambao wanahubiri umoja katika nchi hii mimi ni mmoja wao, na kwa kweli Mhe. Spika, nilikuwa napata shida sana toka nilipoingia katika Baraza na nilipopata hoja hii. Nilikuwa nafikiria ni namna gani ambavyo tutaweza kuwatimizia Wazanzibari lile ambalo wanatarajia kwao.

Kiufupi sina tatizo sana na vile ambavyo wanasema waheshimiwa wengine kuwa suala hili lipelekwe kwa wananchi. Kubwa ninaloliona Mhe. Spika, Baraza lako hili liweke njia muwafaka ambayo haitaleta usumbufu kwa wananchi na kwa kweli tutaweza kupata ridhaa zao bila ya woga, hofu na wasi wasi.

Katika hili mimi sina shaka nalo, kwa sababu Wazanzibari wana upeo mkubwa wa kuchambua mambo, wanajua upi mchele na upi kumba. Naamini wanapenda mshikamano na ushahidi wa hayo ninao.

Mimi katika chama changu ni Naibu Katibu wa Jumuiya ya Wanawake. Katika mwezi huu Mhe. Spika, tulikuwa na sherehe kubwa kule Pemba za Mapinduzi, chama changu kilinituma Zahra nenda ukahamasishe wananchi wajitokeze katika sherehe hizi, kwa sababu tunajua ni namna gani ambavyo tulikuwa tukienda. Nilifanya kazi hiyo juu ya kwamba nilikuwa ninaumwa, lakini nilijikubalisha kutokana na uzanzibari wangu na uzalendo ambao naamini ninao katika nchi hii.

Nilikwenda kufanya kazi hiyo nikirudi nawekewa *drip* kwa sababu *pressure* yangu ilikuwa *low* wakati huo, lakini nikahakikisha kama nimefanya. Siku ya siku Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza lako tukufu walikuwa ni mashahidi ya namna gani Wazanzibari wa Unguja na Pemba bila ya kujali itikadi zao ni namna gani ambavyo walijitokeza kwa wingi.

Mhe.Spika, kusema kweli nililia nilipoiona hali ile, nililia Mheshimiwa, nililia kilio kile cha furaha. Kwa sababu kumbe ilionekana Wazanzibari wana haja ya mshikamano, maelewano, lakini ni siasa au ni sisi wanasiasa ndio ambao tulikuwa tukiwafanya wasiwe kitu kimoja. Walikaa kama vile wamefungwa kizani kwa miaka mingi sasa ile ni siku yao ambayo walifunguliwa walikuwa wakitoka kila milango, nililia Mhe. Spika. Inshaallah naomba Mwenyezi Mungu umoja ule auendeleze.

Mfano wa pili katika kisiwa cha Unguja niliona siku ya Ijumaa ya tarehe 16 pale ambapo tulikaa Wazanzibari wote na kumuomba Mwenyezi Mungu atujalie asiturudishe huko tulikokuwa na atulete kwenye umoja huu ambao Mhe. Spika, tunakwenda nao.

Kwa hivyo, mimi sina wasi wasi na hili hoja kupelekwa kwa wananchi isipokuwa uandaliwe utaratibu mzuri ambao wananchi wetu wote watapata ridhaa ya kutoa maoni yao bila ya hofu na woga. Hapa Mhe. Spika, nataka kusisitiza yule mtoa hoja aliposema kama kuna ulazima wa kuundwa kamati. Kamati ambayo itatuondolea dhana, tuna imani na serikali na ndio maana tumemkubali Mhe. Amani Abeid Karume kama ni rais halali na tunaamini kuwa atatufanyia mazuri Wazanzibari. Lakini jambo lolote la wengi halifai kufanywa na upande mmoja ni lazima tushirikiane katika hili twende kwa wananchi.

Siku zote viongozi ni kioo, watakapotuona sisi tunakwenda kwa umoja wetu kama viongozi kutoka pande mbali mbali za vyama ambavyo vinaongoza

katika nchi yetu tunawaletea mustakabali mzuri na ile picha ya kuona kama kweli viongozi wetu wamekubaliana na wameshirikiana. Kwa hviyo, hata wao watakuwa hawana hofu ya kujali chama.

Naheshimu muda wako Mhe. Spika, lakini namalizia kwa kile kipengele cha 9 cha Katiba ya Zanzibar ambacho mtoa mada ametaka kirekebishwe kuwe na serikali ya umoja wa kitaifa. Nasema Mhe. Spika, kifungu hiki mimi nakiunga mkono kwa asilimia mia moja. Kwa sababu tutakapokuwa na umoja wa kitaifa utawafanya wananchi wote kuamini kama ile serikali ni yao na watakuwa na mapenzi na serikali hiyo, watakuwa na mshikamano.

Mhe. Spika, sio vizuri kukumbusha yaliyopita, lakini tuliona ni namna gani wananchi wetu walivyokosa imani na mapenzi juu ya serikali yao. Kwa hivyo, naamini kwamba, sitaki kurudi tulikotoka lakini naaminikwa hili wananchi watakuwa na imani na serikali yao na pia watakuwa na mapenzi na nchi yao. Kama viongozi waheshimiwa ni lazima tubadilike, kiongozi mzuri ni yule anayesoma wakati, wakati huwezi kuuzuia kwa kiganja, wakati ni wimbi la maji makubwa ukiuzuia kwa kiganja utachukuliwa na wakati. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe ilinibidi nitumie busara kubwa namna ya kumwambia asimame huyu, kwa hivyo, kauli sikuweza kutoa nilimuonesha ishara tu. hizo ni busara wakati mwengine mtu anaposema kwa *pressure* unapomzuia anaanguka. Tuendelee.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: Mhe. Spika, nakushukuru sana na nitajitahidi kutumia muda mfupi sana.

Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uzima na afya njema na nikaweza kusimama mbele ya Baraza lako hili tukufu na mimi kutoa maelezo yangu kuhusu hoja binafsi iliyowasilishwa na Mhe. Abubakar Khamis Bakary jana.

Mhe. Spika, hapa tangu jana na leo tunazungumzia jambo muhimu sana, zito sana, jambo ambalo kama hatutofikia pahala tukakubaliana itakuwa ni tatizo na litatutatiza. Litasababisha mzozo na tutazozana. Lakini Mwenyezi Mungu asitupeleke huko.

Kwa sababu hoja iliyoletwa na Mhe. Abubakar ni hoja ya msingi na inasisitiza sana kudumisha amani na utulivu na hilo sisi sote nafikiri hatupingi kwa jambo hili kuona kwamba nchi yetu inaendelea kwa misingi ya amani na utulivu na kuondokana na siasa za chuki.

Mhe. Spika, kweli tumechoshwa, tumetoshwa sana na siasa za chuki siasa ambazo hazileti mantiki, hazileti maana katika jamii. Kwa hivyo, hoja ile ilikuwa inasisitiza kuweko na Umoja wa Kitaifa lakini kasisitiza kwamba lazima kuwe na maridhiano ya pamoja.

Mhe. Spika, hapa nataka niwashukuru sana viongozi wetu wakuu Mhe. Dr. Amani Abeid Karume na Maalim Seif Sharif Hamad. Kwa mara ya kwanza napenda nimsifu na nimshukuru sana Maalim Seif Shariff Hamad kwa uungwana wake na ukomavu wake wa kisiasa kwa kukubali kuwa kuna haja ya kukaa na mwenzake kuyazungumzia maendeleo na maslahi na mustakabali wa nchi yetu ya Zanzibar. Kwa upeo wake huo wakazaa mazungumzo ya pamoja kwa kushirikiana na kushauriana na hatimaye wakapeana mikono.

Hayo ndio yaliyozungumzwa mengine yaliyozungumzwa siyajui, lakini kwa hayo yaliyozungumzwa ya kutujengea umoja, mashirikiano, amani na utulivu katika nchi yetu nawapongeza viongozi hao sana sana, kwa hayo ambayo yanazungumzwa.

Lakini Mhe. Spika, kabla sijaingia katika uchambuzi, mimi Ramadhan Nyonje Pandu Mzanzibari na mwananchi halisi, Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni, mwananchi wa Jambiani Mfumbwi kwa baba na mama ni Mjambiani menyu.

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba mimi sikusimama hapa kwa *pressure* ya magazeti, wala mimi sio miongoni mwa watu ambao wamepewa hizo pesa mnazozisema nyinyi waandishi wa habari. Kwa sababu waandishi wa habari mna ila, mna matatizo, mnatuparaganya sana, sana, sana. Mnataka kutugawa sana sana, hamuitakii mema nchi hii waandishi wa habari nasema na mni-*quote* ninavyozungumza mseme hivyo hivyo, Mhe. Nyonje anasema waandishi wa habari hawaitakii mema nchi hii.

Mhe. Spika, kabla hoja hii haijaletwa kumekuwa na vineno vineno, wawakilishi wamepewa pesa kuja kupinga hoja hii, wawakilishi wameitwa Ikulu kwenda kula chakula cha mchana, waawkilishi wamepewa magari jambo ambao *is non sense* halina maana ni upuuzi mtupu.

Sisi wawakilishi tumechaguliwa na wananchi, tunajua lipi baya na lipi jema, lakini Mhe. Spika, magazeti haya, kuna magazeti nimekuja nayo kuna gazeti moja limeandika wawakilishi wagaiwa mapesa, ni uzandiki, unafiki mtupu ni uhasama sio kweli. Sasa mimi nasimama hapa si kwamba nimepewa pesa ku-*oppose* ama ku-*support,* lakini nazungumza kwa mtazamo wangu ninaouona.

Mhe. Spika, mimi ninazungumza kwamba hoja hii kwa kiasi fulani imeeleweka na wananchi wetu wanaotusikiliza wametuelewa nini wanataka. Kwa sababu

kuna maelezo yanaingiliana maelezo ya upande wa CCM na upande wa *CUF*. Kimsingi ni kwamba hoja hii waheshimiwa ili kutekeleza demokrasia halisi na kama katiba yetu inavyotuongoza kifungu cha 9(1)(a) na (c) tuelekeeni huko, tuelekee kwa wananchi waliotupa idhini na mamlaka ya kutuingiza sisi katika Baraza hili, hivyo, si mambo yote tunaweza kuamua kwa niaba yao, kuna mambo mazito sana ambayo haya inabidi lazima tuwaulize wenyewe wanachi.

Kwa misingi hiyo Mhe. Spika, ninashauri na naomba sana waheshimiwa wenzangu wote wa Baraza hili, kama tunakusudia kujenga Zanzibar yetu, tunakusudia kuendeleza misingi ya amani, utulivu na upendano basi ni lazima twendeni chini kwa wenzetu waliotuingiza katika Baraza hili. Itakuwa ni dhambi kubwa sana tukiamua kwa niaba yao, haidhuru mtoa hoja alizungumza kwamba anakubaliana kwenda kwenye kura za maoni, yaani wananchi wanaweza kutoa uamuzi au vyenginevyo Baraza hili lifanye maamuzi. Suala la kuwa au vyenginevyo Baraza hili lifanye maamuzi, Mhe. Spika, hapo sikubaliani napo, nataka twende kwa wananchi wenyewe tukawaulize, tuwaambie hoja yao na wao watueleze.

Mhe. Spika, wengine walikuwa wanasema mbona hatukufanya kura za maoni kwenye masuala ya Muungano nadhani kitu kama hiki. Lakini kama hawakufanya ni wale katika Baraza hilo lililopita kwa miaka hiyo, wakati hata mimi sijawa mwakilishi waliporidhiana na hilo ni kosa, kwa sababu masuala ambayo yanawagusa wananchi basi ni lazima yaende kwa wananchi wenyewe. Kwa hivyo, tusichukulie kwamba kipindi kile hatukufanya hivyo, lakini kwa sasa tumejirekebisha na kwa sababu tumejirekebisha basi turudi kule kule, kuna ugomvi gani, kuna kasoro gani na kuna matatizo gani.

Mhe. Spika, maelezo yote yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili, kwa kweli hayakutofautiana, turidhiane na tuondoshe mizozo na tofauti zetu ili tufike pahala tukubaliena, kama kweli tuna nia ya kuijenga Zanzibar hii basi tukubali matokeo na kukubali matokeo sio kujidhalilisha ni uungwana halisi. Uungwana huu uliofanywa na Mhe. Dk. Aman Abeid na Mhe. Seif basi hebu haya maridhiano yao haya tunayoyajua tuyapeleke huko kwa wananchi, halafu wao ndio watasema kwamba vipengele moja, mbili na tatu havihusiki. Lakini tutafika pahala tunazozana na tunafika pahala tuna *compromise* tunakuwa hatuna jinsi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ushauri wangu ulikuwa ni huo mmoja, kuona kwamba katiba ina heshimiwa na kwa sababu sina haja ya kunukuu sana. lakini kifungu cha 9(1)(2) kinasema kwamba:

Kifungu cha 9(1)(2)(a)

"Mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe, ambapo nguvu na uwezo wote wa serikali kufuatana na katiba utatoka kwa wananchi wenyewe",

(c) "Katiba hii itahakikisha kwamba wananchi wanashiriki katika serikali yao".

Mhe. Spika, hapo itakuwa wananchi tumewashirikisha na hii dhana ya kwamba tufanye sasa hivi au halafu itatupotezea muda. Tunajua kwamba tukienda katika mazungumzo hayo, wananchi wakikubali mfumo gani utuongoze, tutajua Rais atakayekuja atakuwa na wajibu wa kufuata yale tunayoyataka. Hakufuata tulivyokubaliana Rais ajaye. Nyinyi mnaojipanga Urais. Rais ajaye Mhe. Spika, kama hatakukubaliana mambo tunayoamuliana hapa, basi mimi nitakuwa mmoja, kwa sababu ninajua nitakuja Mwenyezi Mungu akinijaalia nitaingia. Mimi nitakuwa mmoja wa kuleta hoja binafsi ya kutokuwa na imani na yeye na nitawashawishi wenzangu waniunge mkono kwa hili. Tunataka tufike pahala tuone sasa tunakwenda vizuri kama Zanzibar isiwe vipande vipande, Zanzibar moja, watu wamoja na vyama mbali mbali. Kwa hivyo, Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nasema "Waãtaswimu Bihabdillah Jamiyãn Walaatafarraqu". Ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Kumbe humu ndani mnavitu tena pande zote mbili. Ahsante Mhe. Al Hajj mtarajiwa, Ramadhan Nyonje Pandu. Maana jana ulitajwa na Mhe. Ali Suleiman kwamba mtafuatana pamoja. Ahsante sana. Sasa tumsiklize Mhe. Haji Faki Shaali na baadaye Mhe. Ali Mzee Ali *Professor*.

Mhe. Haji Faki Shaali: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kama walivyotangulia wenzangu. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kutoa mawazo yangu juu ya kujenga mustakabali wa nchi yangu ninayoipenda ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kabla sijaenda katika hoja yenyewe, kwanza napenda nifanye marekebisho kidogo kuhusu rafiki yangu Mhe. Haroun Suleiman Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika: Tuwe pamoja kwenye mkutano huu.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Haroun jana alinitaja kwa nia njema kwamba tulifanya ziara kisiri siri, lakini hatukufanya ziara siri siri. Ilikuwa ni mwaka 2004 baada ya uchaguzi mwaka 2003, sisi tuliitambua serikali, nafikiri amesahau. Baada ya uchaguzi wa mwaka 2003 mpaka 2005, tuliitambua

serikali, tukafanya nao kazi vizuri na nikafanya naye ziara mimi na yeye na Mbunge wa Mkoani, tukenda Makoongwe, tukenda Kisiwa Panza kwa wananchi wangu, kwa hivyo haikuwa suala la siri siri.

Lakini nimuongezee zaidi tu afahamu kuwa mimi ni mtu wa aina gani katika siasa. Mwaka jana nilimuomba Mhe. Shamuhuna gari akanipa kwenda nyumbani kwake kuwaangalia mama zangu ambao anao nyumbani kwake. Nadhani ingekuwa kama mimi ni mtu muoga muoga kwa kipindi kile nisingekwenda kwa Mhe. Shamuhuna. Nafikiri nilikuwa na rafiki yangu Mhe. Subeit. Kwa hivyo, mimi ni mwanasiasa ambaye ni *bold* siwezi kufanya mambo ya kisiri siri. Hata wizarani kwake ninapokuja nakuja fawahisha siogopi kitu.

Mhe. Spika, baada ya hayo nije katika hoja yenyewe. Mhe. Spika, mimi mwaka jana baada ya kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM kilichokwenda Butiama na kutoka kauli hii ya kufanywa kura ya maoni. Mtu wa mwanzo aliyesimama kuipinga alikuwa ni ndugu Joseph Warioba, Waziri mkuu mstaafu alipinga suala la kufanyika kura ya maoni. Kwa mawazo yake na kwa vile anavyoifahamu historia ya Zanzibar kwamba hii itatugawa zaidi.

Mhe. Warioba aliangalia mambo mawili makubwa. Aliangalia *Legal impact* na *political impact* ya kura ya maoni, kwa sababu kura ya maoni ina athari mbili. Ina athari ya kisiasa na kisheria. Kisheria mnaweza mkapiga kura ya maoni lile jambo lililokusudiwa upande mmoja wakashinda. Kwa hivyo, kisheria itabidi ule ndio ushindi umepatikana. Lakini athari za kisiasa ni kwamba inaweza ikaleta migogoro mikubwa zaidi kuliko ile iliyokuwepo.

Kwa hivyo na mimi nataka niungane na Mhe. Joseph Warioba kwa hili. Mhe. Spika, suala ambalo mimi naliogopa, pamoja na kumuunga mkono kiongozi wangu Mhe. Abubakar Khamis mwenzangu ambaye namsaidia katika kambi yetu. Lakini hofu yangu iliko katika hii kura ya maoni na zaidi nilikuwa nafuatilia michango ya Ali Suleiman. Kwa kweli Mhe. Ali Suleiman jana mimi nimempenda sana, kazungumza kitu ambacho ndani ya nafsi yake kimo, hakuonesha unafki hata kidogo.

Mhe. Ali Suleiman aliuliza Je, ikiwa kura ya maoni itaonesha wananchi wameikataa, watu wataheshimu. Sasa kisheria watu watapaswa waheshimu, lakini kisiasa huwezi kusema kwamba watu wataheshimu au hawataheshimu. Kwa sababu kuna ile *legal impact* na kuna *political impact*. Kwa hivyo, hili mimi naliogopa sana kusema kweli, kwa sababu kama wananchi wa kisiwa cha Unguja wakisema ndio na wananchi wa Pemba wakasema hapana. Basi tayari itakuwa tumetoa *loophole* kuigawa nchi. Kwa sababu itaonekana kuwa historia ya Unguja na Pemba ni tofauti, *geography* ya Pemba na Unguja ni tofauti na

kila kitu kitaonekana ni tofauti, mambo ambayo yanapelekea kuwa tayari hawa wana *identity* yao na hawa wana *identity* yao kama kinavyozungumza kile kitabu cha *Professor* Shivji jambo ambalo linaweza likapelekea pabaya zaidi. Kwa hivyo, jambo hili mimi naliunga mkono kuwa na kura ya maoni kwa sababu ni yetu. Lakini hofu yangu ni hiyo nataka niieleze na mapema ili nieleweke.

Jengine Mhe. Spika, ambalo nina wasi wasi nalo. Nilisikia kauli ya Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi ndugu Salum, katika kongamano *REDET* Bwawani. Kulikuwa na malalamiko ya vyama kwamba daftari lina matatizo. Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi akakiri kweli lina matatizo na akasema kumepandikizwa watu katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na Mikoa ya Pemba na daftari hili ndio litakuja kutumika kufanyia kura ya maoni. Sasa ikiwa Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Tume ya Uchaguzi kakiri katika kongamano la REDET Bwawani na daftari hili uje ulitumie kwenda kufanya kura ya maoni. Kweli wananchi hao watakubali kwenda kufanya kura ya maoni kwa daftari hili. Sasa hapa pana mambo nasema nieleze yaliomo ndani ya moyo wangu, nisikubali kitu kwa furaha na unafiki ndani yake. Unafiki kwa kweli ni maradhi mabaya sana.

Kwa hivyo, mimi nina wasi wasi na hiyo kura ya maoni kwamba je, katika mazingira haya tuliyonayo sasa bila kuyasafisha na kuwa na chombo kitakachosimamia mambo haya kitakachokubalika na pande zote mbili, kura ya maoni hiyo utakwenda kumfanyia nani.

Mhe. Spika, sasa nakuja kwenye hoja yenyewe. Mimi kwanza naunga mkono wazo la Mhe. Abubakar Khamis la kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Sikubaliane na wazo la ile kuwapata mawaziri kwa kutumia uwiano wa viti, kwa sababu gani. Kwa sababu nina hakika uchaguzi kama utakuwa wa haki na huru chama cha wananchi CUF kitaingia, CCM nina hakika kitaingia. Lakini mimi siridhiki kuingia vyama viwili. Mimi nataka tuende kama wenzetu Ujerumani. Unajua Ujerumani chama kinaweza kikakosa viti katika Bunge, lakini wanatumia vile vile uwiano wa vyama, kuna uwiano wa kura za Wabunge, yaani kuna *category* nyingi za watu kuingia Bungeni. Sasa utakuta Ujerumani unaweza ukakosa viti katika Bunge, lakini unaweza ukapata kwa kupitia katika utaratibu mwengine wa vyama. Kwa maana hiyo tunataka kuviua vyama vyengine ambavyo havina nguvu na mimi nasema hivi tuvilee.

Pendekezo hili Mhe. Rais Mstaafu Mhe. Benjamin Mkapa alikuwa nalo, lakini kwa bahati mbaya alishindwa kulisimamia. Alisema kwa utaratibu tulionao huu kama hatukuwa na *proportional representation* basi vyama vidogo vitakufa. Alikuwa nalo hili Mhe. Benjamin Mkapa, lakini bahati mbaya alishindwa kuisimamia dhamira yake. Kwa hivyo, mimi naona tuendelee na utaratibu, lakini utaratibu huu wa viti kwamba wale wenye viti tu ndio waje humu. Kwa

kweli hii tutakuwa tunaua vyama na bado tutakuwa hatujakubali kujenga demokrasia.

Halafu Mhe. Spika, suala jengine ambalo serikali hailitaki, suala la kwamba kamati ile ya watu 6 haina maana. Sasa hapa mimi ndio naona vichekesho. Nilikuwa nasoma kuna taasisi moja inaitwa *conflict resolution institute*, yaani taasisi ya kutatua migogoro. Sijapata kuona hata mgogoro mmoja ambao msimamizi wa yale yaliyokubaliwa ni upande mmoja, sijapata kuona. Lakini nimesoma kesi katika *legal method* zinazohusu *dispute settlement method*, nimeangalia kesi yake sijapata kuona mgogoro ambao umetatuliwa kwa aina hii tunayopendekeza serikali. Mgogoro ni wa pande mbili a na b, lakini leo upande (a) uchukue dhima kufanya masawazisho ya mambo yote peke yake, hii sijapata kuona.

Nimeangalia katika *legal method* kwenye *profession* ya sheria, nimeangalia katika *dispute conflict resolution institute* sijapata kuona kitu hiki. Sasa nadhani tukianzisha mambo ya ajabu ajabu, hayatatupeleka pahala. Lazima kama tuna nia ya kurekebisha tukubali kwamba *the winner does not take all*, tukubali maoni ya Mhe. Abubakar, tukubali maoni yenu na kila mmoja akubali ku-*loose* baadhi ya mambo. Lakini tuking'ang'ania kila kitu, halafu pendekezo hili mkatae kwa sababu tu halimo katika Butiama nadhani hapo itakuwa hatujawafanyia haki Wazanzibari.

Nataka nimshukuru sana Mhe. Spika, ndugu yangu Enzi Talib. Mhe. Spika, Enzi Talib juzi alipokuwa katika *round table* alisema kitu kimoja kizuri sana. Kwa kweli huyu ni Mzanzibari kwenye akili sana. Alisema mgogoro wote wa Zanzibar ikiwa watatatua Wazanzibari peke yao wanaweza, lakini akiingia mtu wa tatu kuna matatizo.

Sasa na hapa matatizo yametokezea kwa sababu hofu inakuja ile ile aah! Maamuzi ya Butiama. Sasa tunashindwa kufikia maamuzi sahihi kwa ile hofu tu aah! Haya ya Butiama. Halafu tutakuja kusema aah! Haya ya Buguruni, Maalim Abuu atakuwa na hofu ya Buguruni na kule mtakuwa na hofu ya Butiama. Kwa hivyo, sisi ni Wazanzibar na hivi vyama ni vya kitaifa, tunaoyajua matatizo ya Zanzibar ni sisi, mtu wa Butiama hajui matatizo ya hapa na *Professor* Lipumba anajua zaidi matatizo ya Tabora hajui ya Zanzibar. Kwa hivyo, mimi nafikiri tuheshimu vyama vyetu, sisemi kuwa tugombane na vyama vyetu hapana. Mimi namuheshimu *Professor* Lipumba, lakini nasema *Professor* Lipumba hayajui matatizo ya Zanzibar kama ninavyoyajua mimi Haji Faki Shaali. Mtu mwengine yeyote wa Bara wa CCM hawezi kuyajua kama anavyoyajua Mhe. Ali Juma Shamuhuna na Shamsi Vuai Nahodha.

Kwa hivyo, tusipokubali Mhe. Spika, hili tukajenga hofu ya kuogopa Buguruni na tukajenga hofu ya kuogopa Butiama. Kwa kweli tutafanya jambo *superficially* tuondoke hapa na furaha ya muda mchache, turudi kule kule ambapo mimi sipendi. Mimi ni muwazi lazima niseme ukweli.

Halafu ndugu yangu mpenzi wangu Mhe. Thuwaybah alisema jana kwamba kutakuwa na Makamu wa Rais atakuwa boya. *Doctor* unajua kwamba mimi ni Al Hajj siko kwenye upenzi huo, ni upenzi mwengine wa Kiislamu na kibaraza tu. *Doctor* hana matatizo na mimi. Sasa ikiwa tunaingia kwenye maridhiano Mhe. Spika, tuwe wazi. Sisi tunaingia katika maridhiano tunasema upande mmoja utapata Makamo wa Rais lakini atakuwa ni boya. Sasa unaanza kum-*fully* mtu kabla hayamjafika mwenzako, safari hiyo itakuwa salama. Yaani lile jambo unaanza kuli-*fully* kabla safari haijaanzwa safari hiyo itakuwa salama.

Sasa kwa kweli kauli nyengine zinatutia mashaka Mhe. Spika, na katika jambo jengine nililojifunza katika utatuzi wa migogoro, kwanza kila mmoja awe tayari kupoteza na sio kila kitu ukikubali na Mhe. Abuu nafikiri atakubali kupoteza baadhi ya mambo lakini waheshimiwa nawaomba kwa heshima zote, ndugu yenu mwenzenu wa muda mrefu, mtiifu sana kwa serikali hii naomba na serikali ipunguze baadhi ya misimamo, tukaombe radhi Butiama na mtakubaliwa lakini hili la kamati ya watu sita naomba hili kwa kweli tuliridhie kwa sababu wananchi watakapoona kwamba kitu hiki hakipo kwa kweli hawatatuelewa wala hawatakubali maridhiano haya.

Halafu jengine Mhe. Spika katika maridhiano, watu wanatakiwa waangalie *future* na sio *past* mimi ndio maana ukaona sikuzungumza historia ni mwana historia mzuri mimi nilikuwa nafundisha historia. Lakini siku zote katika jambo hili, mnaangaliwa ile *driving phylosophy* yenu iwe ni future *not past*, sasa mimi ndio hata sikutaka leo kuzungumza historia maana ningezungumza historia hapa, somo yangu Mhe. Haji Omar angelia, Mhe Zainab angelia, Mhe Asha angelia, sasa naona bora tusiende kwenye historia na kwenda zaidi kwenye *past*.

Mhe.Spika: Dakika tatu zimebakia.

Mhe. Haji Faki Shaali: Lakini vile vile Mhe. Spika mimi kwa kumalizia nilikuwa na wazo la mpenzi wangu Mhe Mshimba, yeye kazungumza jambo zuri lakini kiutani mimi sizungumzii kiutani, kuna haja ya kujifunza kwa wenzetu katika mambo haya, ziko nchi wameunda serikali za aina hii, nafikiri kuna haja ya kwenda kujifunza na naomba katika watu watakaokwenda kujifunza na mimi Mhe. Spika usije ukaniwacha. Lakini licha ya kwenda nje, kwa sababu sote tutakuwa hatuwezi kwenda na Mhe. Zainab keshachoka madege hayawezi. Kwa hivyo, nashauri kwamba tuwatafute wataalamu

waliobobea waje watufanyie semina katika Baraza letu, namna ya kuendesha Serikali za Umoja wa Kitaifa.

Jengine Mhe. Spika, nataka hekima unayoitumia katika Baraza lako, ukaniweka Haji Faki Shaali CUF na ukamuweka Mhe. Ali Suleiman CCM tukafanya kazi pamoja vizuri bila migongano. Uitumie ili kuishauri serikali iwache hofu. Mhe. Spika, sisi tunafanyakazi katika kamati tukienda hatujulikani kama huyu anatoka CUF au CCM. Kweli mimi leo uniweke na Mhe. Haji Omar Kheir iwe mimi waziri na yeye awe naibu wangu tutagongana wapi, awe nijaalie mimi waziri Kiongozi na mzee wangu yule Mhe. Burhani ninavyomuheshimu awe waziri wangu wa kilimo tutagongana wapi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, uwe na darasa zuri kwa serikali ili utowe ujumbe kama huu.

Mhe. Spika, la mwisho kwa kumalizia nasema kwamba tujifunze kwa baba wa taifa. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilikuwa haiitwi Serikali ya Umoja wa Kitaifa, lakini kwa maumbile yake ulikuwa unaweza kuiita Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kwa sababu gani. Kwa sababu ilijumuisha jamii zote za Watanzania na kwa maana hiyo ilikuwa haina migogoro, ilijumuisha Waislamu, ilijumuisha Wakristo na ilijumuisha makabila yote.

Mhe. Spika, kuna kitu naomba univumilie kidogo, utakata hata dakika mbili kwa mtu yeyote huku, lakini niachie kwa hili. Mhe. Spika, mimi nilikuwa ni CCM na nilikuwa ni Mjumbe wa Baraza Kuu la kwanza la umoja wa vijana la Tanzania na nimesafiri sana Tanzania. Mwenyekiti wangu alikuwa Moh'd Seif Khatib, katibu mkuu wangu alikuwa Rajab Kheir Yussuf, wajumbe wenzangu namkumbuka Bwana Kikwete, Sukwa Said Sukwa. Vijana wengi nawakumbuka kumbuka, hata Moh'd Abdi nafikiri pia alikuwemo, Kikwete tulikuwa pamoja. Natoka mbali katika mambo haya ya siasa Mhe. Zainab anajua.

Mhe. Spika, kuna kitu kwa wakati huo kilikuwa ni siri, lakini sasa sio siri nitakisema kwa nia njema. Mhe. Spika, siku moja nilikuwa nasafiri nakwenda Bukoba, ilikuwa ni Januari 1984 alipojiuzulu Aboud Jumbe. Nilikuwa na watu wa kusini na ni watu wazito na wengine walikuwa wanafanya idara nyeti kabisa tulikuwa nao katika umoja wa vijana wetu, Kusini ya Tanzania. Naomba nivumilie Mhe. Spika, nazungumza jambo zuri.

Sasa ikawa watu wa kusini wanatafakari na kuna kipindi Mzee Rashid Kawawa kidogo alipumzishwa katika nafasi kubwa za kitaifa, lakini watu wa kusini hawakufurahi. Ikatolewa *delegation* ya wazee 12 kutoka Mikoa ya Kusini wakaja kwa mwalimu. Wakazungumza na mwalimu, mwalimu akawafahamu wale wazee, akaona sasa umoja wa kitaifa hapa unahatarika, yaani ule umoja wa nchi unahatarika. Ghafla bwana akarejeshwa kwa katibu mkuu, aliondolewa

Msekwa akapigwa nafasi ya ukatibu mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Nafikiri wale waliokuwa katika CCM wanakumbuka.

Kwa hivyo, hili jambo mimi nalijua chimbuko lake kwa sababu hao niliokuwanao ni jamaa zake, ni watu wa kusini na wengine ni watu wa *intelligence* wakubwa, sitaki kuwataja majina yao sio vizuri. Lakini kidogo tu walipoona ile kuondolewa Kawawa, basi ikataka kuwaletea watu wa kusini tafrani mwalimu akaiona hiyo, basi haraka akasawazisha mambo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, na sisi tujifunze mambo haya, wananchi wamechoshwa na migogoro, wananchi wanataka umoja, lakini umoja wa kweli sio umoja wa magube. Katika kipindi hiki kuelekea katika kura hiyo ya maoni ni lazima tuandae mazingira ambayo kila mmoja ataamini kwenda katika kura ya maoni na baadae kila mmoja atakuwa na nia safi ya kwenda katika huo uchaguzi mkuu. Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunivumilia na nawashukuru wenzangu wote kwa kunivumilia hata kama pengine ile *mood* yangu kidogo imebadilika ni tofauti na walivyochangia wenzangu. Lakini kwa kweli nia yangu nataka niseme lile ambalo naliamini, sitaki kusema kitu nisichokiamini. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Haji Faki Shaali. Sasa tumsikilize Mhe. Ali Mzee Ali *Professor. Professor* huyu anakawaida ya kuja na *library* na *literature* nyingi sana. Lakini leo atafanya *summary* kwa dakika 15 tu.

Mhe. Ali Mzee Ali: Sawa sawa. Mhe. Spika, hata ingekuwa umeniweka pembeni, watoto mambo wameshayaweka sawa. Lakini kwa sababu nimeomba niseme, basi itabidi niseme. Mhe. Spika, leo ni siku ya Ijumaa ni siku tukufu sana kwa Waislamu na leo tunaweka historia ndani ya nchi yetu.

Kwa hivyo, naomba wajumbe waliosalia kuchangia warudi kwenye mstari tulioanzia asubuhi na jana. Madhumuni yetu sisi ni kuijenga Zanzibar mpya. Sasa nimeshtushwa, lakini mwisho rafiki yangu Mhe. Haji Faki Shaali amenifurahisha, amesema aah! Hayo ndio mawazo yangu lakini ameunga mkono.

Mhe. Spika, hapa pana mambo mawili. Kwanza nataka kuungana na mtoa hoja kwa kutaka tutambue mazungumzo ya Rais wa Zanzibar na Maalim Seif Sharif Hamad. Mimi nayatambua, ni mazungumzo muhimu sana, ni mazungumzo yaliyopokelewa.

Serikali ya Norway imetoa pongezi kwa Rais wa Zanzibar na Maalim Seif kwa kukutana na kujenga mustakabali wa Zanzibar. European Union imetoa pongezi, UNDP wametoa pongezi, Balozi wa Afrika ya Kusini ametoa pongezi

na ambaye ni mkuu wa Mabalozi Afrika, CCM mikoa wametoa pongezi, Umoja wa Vijana Zanzibar wametoa pongezi, wasomi wametoa pongezi, Wazanzibari waliokuwa Uingereza wametoa pongezi, Wazanzibari waliokuwa Canada wametoa pongezi na Wazanzibari waliokuwa Denmark wametoa pongezi.

Sasa nasoma pongezi nyengine. Taarifa kwa vyombo vya habari, Rais Jakaya Kikwete amempongeza Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Aman Abeid Karume na Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi CUF, ndugu Seif Sharif Hamad, kwa uamuzi na hatua waliyoichukua kukutana na kufanya mazungumzo katika Ikulu ya Zanzibar tarehe 5 Novemba, 2009.

Rais Kikwete amefurahishwa sana na hatua hiyo na anawatakia mafanikio mema. Aidha amewahakikishia ushirikiano wa kibinafsi na ule wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na Chama cha Mapinduzi.

Vile vile Rais Kikwete amefurahishwa na hatua ya Chama cha CUF kuitambua rasmi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kumtambua Rais Aman Karume kama ni Rais wa Zanzibar kuwa ni hatua muhimu katika kujenga na kuaminiana, anaamini kuwa uamuzi huo utasaidia katika juhudi zilizokuwa zinaendelea na kuyatafutia ufumbuzi matatizo ya kisiasa Zanzibar.

Hii ni hatua kubwa na muhimu sana katika juhudi za kuleta umoja, amani na utulivu katika visiwa vya Zanzibar na Tanzanzia kwa jumla. Sina budi kuwapongeza Rais Aman Karume na Maalim Seif Sharif Hamad, Katibu Mkuu wa CUF kwa uamuzi wao wa busara, unaojali maslahi mapana ya watu wa Zanzibar na Tanzania.

Rais amewataka Wazanzibari na wananchi wote wa Tanzania kwa jumla na jumuia ya kimataifa kuwapongeza, kuwaunga mkono na kushirikiana na Rais Aman Karume na Maalim Seif kwa uamuzi wao wa busara na moyo wao wa ujasiri. Rais Kikwete amesema katika kipindi hiki viongozi wetu hawa wanahitaji kutiwa moyo, ili waendeleze kwa kasi zaidi jitihada zao hadi kufikia ile hatima njema tunayotarajia sote, yaani Zanzibar na Tanzania ambayo watu wake wanaishi kwa amani, umoja, upendo, mshikamano na ushirikiano wa maslahi yao ya nchi hii.

Rais Kikwete amewataka Watanzania wote kwa kauli moja kuwapuuza watu ambao wanabeza na kupinga jitihada hizi za matumaini na hata kujaribu kuzihujumu. Tangu Januari, 2007 vyama vya CCM na CUF vimekuwa katika mazungumzo ya kutatua mgogoro wa kisiasa visiwani Zanzibar, kwa lengo la amani na utulivu katika nchi yetu. Mkutano wa tarehe 5 Novemba, 2009 baina ya Rais Amani Abeid Karume na Katibu Mkuu wa CUF ni kitendo kilicholeta

matumaini makubwa kwa jitihada hizi na kufikia hapa. Hii Mhe. Spika, niliona niisome, sasa wanaobeza wabeze.

Mhe. Spika, sasa nizungumzie hoja ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary. Mhe. Spika, Mhe. Abubakar mimi namheshimu sana, yeye ndie aliyekuwa mwanzilishi wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Mhe. Abubakar ni mwanakindaki wa Afro Shirazi kwa sababu alikuwa Mjumbe wa *NEC*. Mhe. Abubakar amekuwa CCM, amekuwa Afro Shirazi, amekuwa Mwanasheria Mkuu, amekuwa Waziri, ni mtu mzuri, mtu mwema. Naomba nimnukuu Marehemu Said Iddi Bavuai Mwanamapinduzi kati ya watu *arbaa taashara* anasema "Mhe. Abubakar ni kijana madhubuti".

Sasa Mhe. Abubakar Khamis Bakary mimi namheshimu, lakini kama alivyosema waraka ule kwamba Rais Jakaya Mrisho Kikwete alipokuwa anafungua Bunge anasema anakereketwa, anasononeka na hali ya Zanzibar. Kwa hivyo, kamati ikaundwa na wajumbe wake walikuwa Mhe. Yussuf Makamba, Mhe. Kingunge Ngombale Mwiru, Mhe. Lamwai, Mhe. Ali Ameir Moh'd, Mhe. Zainab Omar Moh'd na Vuai Ali Vuai. Upande wa CUF walikuwa Maalim Seif Shariff Hamad, Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Mhe. Juma Duni Haji, Mhe. Hamad Rashid Moh'd na Jussa.

Sasa kamati hii ilifanya kazi kwa miezi 18 tena walikuwa wanakaa hoteli nzuri kule Bagamoyo. Kamati hii kwa pamoja nasoma waraka huu. "Timu ya mazungumzo CCM na CUF zimefikia kwa pamoja maelewano". Wale niliowataja.

"Kuhusu ajenda namba moja mbali na namba nne. Katika mazungumzo ya ajenda namba nne pande mbili zilifikia maelewano juu ya hoja ya kuunda serikali shirikishi baada ya Uchaguzi Mkuu mwaka 2010 na taswira ya serikali hiyo kama ifuatavyo:

Mimi ni Mjumbe wa *NEC*, naunga mkono maamuzi haya ya kuunda serikali shirikishi kwa sababu ndio chama chetu au chama changu ndivyo ilivyokubaliana".

Mhe. Abubakar Khamis Bakary na yeye amekubali kwa sababu hata kwenye hoja yake kasema iundwe serikali shirikishi. Sasa muundo gani? Mshindi wa uchaguzi wa Rais awe Rais Mtendaji. Mimi hiyo naunga mkono na huu ndio msimamo wa chama chetu. *(Makofi)*

Lakini tumekubaliana katika kamati zile mbili. Chama cha pili kura za Rais kitatoa Makamo wa Kwanza wa Rais, nakubaliana na hilo na naomba wajumbe wenzangu tukubaliane na hilo.

Namba 3, Makamo wa Pili wa Rais atateuliwa na Rais kutoka chama chake atakayeongoza Shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi na ni mrithi wa Rais ikitokea lisilotarajiwa. Hilo lilikubaliwa na kamati niliyoitaja. Rais atachagua Mawaziri kwa uwiano baada ya kushauriana na Wakuu wa Vyama husika. Hayo mambo ndio yaliyokubaliwa katika mambo ya msingi.

Serikali shirikishi itatokana na Uchaguzi Mkuu ulio huru na haki ili washiriki wawe na uhalali wa kidemokrasia. Hilo nalikubali, ndivyo tulivyokubaliana Butiama na ndio Serikali Shirikishi ya Kitaifa itaanza mara moja baada ya matokeo ya Uchaguzi Mkuu.

Haya niliyoyasema ndio yaliyokubaliwa na tume zile mbili, sasa tulipokuja kujadili jambo hili tunasema haya mazuri, lakini suala hili bora liende kwa wananchi. Tukawaagiza wenzetu nendeni mkawaambie wenzenu kuwa tumepokea, tumeafiki yote, lakini suala hili bora liende kwa wananchi kwa njia ya kura ya maoni. Ikapelekwa wenzetu wakakataa, wakasema tunakubaliana na yale yale tuliyoyasoma.

Mhe. Spika, ninazo *statement* za Maalim Seif Shariff Hamad za chama kuwa wanakubaliana na yale lakini hili hapana. Mhe. Spika, tumekaa mwaka mmoja na nusu hamna kitu. Tarehe 5 Novemba, 2009 Maalim Seif kenda kuonana na Rais Amani Abeid Karume wamezungumza imepatikana ile ridhaa. Mhe. Spika, nitoe pongezi ni jambo zuri sana.

Mhe. Spika, ridhaa ni jambo muhimu sana. Sasa namuomba Mhe. Abubakar Khamis Bakary, amepoteza muda wake miezi 18 kwa faida ya nchi hii. Haya mambo uliyoyaleta na haya tunatofautiana pahala pamoja tu namba tatu, mengine yote nimeyakubali, nakuomba na hilo ulikubali tujenge mustakbali wa nchi yetu, hapa hatutafuti vyeo tunatafuta kujenga nchi ya mustakbali, tujenge amani na utulivu wananchi wanatusubiri wanatusikiliza. Jukumu la nchi hii hata Rais Jakaya Mrisho Kikwete kasema ni la Wazanzibari wenyewe. Lakini kama Tanzania tuna haki na ulimwengu.

Kwa hivyo, Mhe. Abubakar Khamis Bakary nakuomba kwa unyenyekevu na wewe ndie uliyenipa Masters na shahada ninayo, nakuomba sana kwa maslahi ya Zanzibar na wananchi wake tukubaliane leo Ijumaa tumalize kwa salama usalimini tujenge nchi yetu mengine yatafuata baadae.

Mhe. Spika, leo sitaki kutoa historia zimetoka nyingi sana, ninachoomba tu baada ya hii kumalizika hoja ikishapita siku moja tuandae semina. Mhe. Haji Faki Shaali atoe historia na yeye kwa upande wake ili wananchi wetu

tuwaeleze. Historia tunaizika ya maovu, tunaanzisha historia mpya ya kujenga Zanzibar mpya.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Maalim Seif Shariff Hamad na Mhe. Amani Abeid Karume wote hao humu ndani walikuwepo. Mhe. Spika, kwanza naunga mkono naomba hilo.

Sasa mimi kwenye hili nimemaliza na natumai hayo ya Butiama, Butiama ndio chama chetu tulikotoka, sisi tulikuja huku kwenye vyama na wao wamekuja kwenye vyama, lakini vyama vyenyewe vimekutana na yametajwa majina. Tuache jazba, tuheshimu vyama vyetu, sisi sote humu ndani tulitoka CCM, Afro Shirazi.

Mhe. Spika, ushahidi kwamba sisi sote tulitoka CCM nanukuu *hansard* ya mtu mmoja anasema hivi, "Tulipoanzisha Afro Shirazi tulikataa kutawaliwa na tulikataa demokrasi iliyokuwa ikitumika wakati ule kwa kuwadhalilisha walio wengi. Tukafanya Mapinduzi baada ya kushindwa njia zote nyengine za demokrasi".

Maneno hayo anasema Mhe. Mkuu wa Upinzani Bungeni, Hamad Rashid Moh'd humu ndani. Haya hajasema Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, hajasema Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, haya kasema Mhe. Hamad Rashid tulipounda Afro Shirazi tukafanya Mapinduzi, tulikuwa hatuna budi. Kwa hivyo, hawa kina Mhe. Haji Faki Shaali ndio *Youth League* ndio wenyewe hao, basi tu.

Mhe. Spika, niruhusu nimnukuu mtu wa mwisho anasema hivi, "Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wananchi kwa jumla. Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu watakumbuka tarehe 10 Oktoba, 1984 walipitisha kwa kauli moja Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Ninafuraha kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Mswada wa Sheria wa Kubadilisha Katiba hiyo uliidhinishwa na Rais wa Zanzibar tarehe 01 Disemba, 1984 kuwa sheria kamili. Baada ya mswada huo kutiwa saini, Mhe. Rais wa Zanzibar alikubali katiba hiyo ianzishwe rasmi". Katiba hii tunayoitumia.

Mhe. Spika, nina hakika kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi kwa jumla walilisikia tamko la Rais wa Zanzibar wakati wa kilele cha sherehe za kuadhimisha mwaka wa 21 wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kuanza kutumika rasmi kwa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Mhe. Spika, Mhe. Rais alitangaza kwamba katiba hiyo ianze kutumika rasmi tarehe 12 Januari, 1985. Tamko hili la Rais lilipokewa kwa furaha, shangwe kubwa na wananchi na Watanzania kwa jumla. Natumai

Waheshimiwa Wajumbe watakubaliana na mimi. Namshukuru na kumpongeza Rais Ali Hassan Mwinyi kwa uamuzi wake.

"Tarehe 12 Januari, 1985 kuwa ni siku ya kuanza rasmi kutumika kwa katiba hiyo. Hakuna siku njema zaidi ya siku hiyo, kwani tarehe 12 Januari, ni siku ya kihistoria, ni siku ambayo wananchi wanaithamini sana kwa vile ni siku ambayo nchi yetu ilizaliwa upya na wananchi wake walipoanza kuvuta hewa ya uhuru wa kweli. Kutokana na ukweli huo ni jambo la kufaa sana kwamba mambo makubwa yenye umuhimu na dhamiri kwa nchi hii yaanze siku hiyo".

"Mhe. Spika, sio bahati nasibu kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliacha kutumia rasmi katiba hiyo tarehe 12 Januari, 1980 na wala sio uamuzi wa kubahatisha, ni uamuzi wa hakika ambao sisi Wanamapinduzi na vizazi vyetu tutauenzi maisha". Hayo aliyasema Maalim Seif Shariff Hamad.

Sasa leo Mhe. Abubakar Khamis Bakary anasema misingi ya Mapinduzi ndio itiwe ndani ya katiba. Tumepiga hatua kubwa sana, lakini misingi ya Mapinduzi *objectives* zake, naomba hii Mhe. Spika, uamuru *decree No. 6* itolewe tena watu wapewe.

Madhumuni ya Mapinduzi. *"Primary objectives of Zanzibar Peoples' Republic is to end all economic, social, legal privileges disabilities which have in the past divided various citizen and groups of citizen according to their ranks, sex, religion or origin and to promote equality, reconciliation, unity of the people of Zanzibar".*

Huu ndio msimamo wa Serikali ya Mapinduzi sio msimamo wa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume na leo tunakuja ku-*reconciliation* tena hapa. Ndugu zangu nina mengi sana, lakini nakuombeni kwanza kwenye hili tushirikiane mswada tuupitishe, tujenge nchi yetu, halafu tuone baadae kwa sababu historia itatuandika.

Mhe. Spika, juzi nilikaa jioni hapo nilifurahi sana kwa sababu historia tunayoandika mengi yaliyotamkwa hapo kuwa siku ya Alkhamis utakuja mswada wa Mhe. Abubakar Khamis Bakary, atukuja kusema hivi na hivi.

Mhe. Spika, hapana pahala pazuri kuzungumza kama hapa. Mhe. Spika, kuna hii barua anasema "*Let 2010 be the year of Zanzibar reconcile*, hiyo mtu wa Marekani. Mwaka huu 2010 uwe mwaka wa kupatana na kufahamiana.

Sasa katika suala lote hili mimi naagiza Mhe. Spika, nina *some observation* katika hoja ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary. Katika *observation* yangu ya 8 katika hoja ya kuchangia taratibu mbali tofauti ambazo kwa mujibu wa Kanuni

za Baraza, taratibu hizo haziwezi kutumika kwa pamoja. Kanuni zinaelekeza ama uwe ni Mswada wa Serikali au ni Mswada wa Mjumbe, lakini hauwezi kuwa ni Mswada wa Mjumbe na hapo hapo uwe ni mswada wa serikali. Mtoa hoja anapaswa kuamua anataka utaratibu upi.

Ikiwa anataka serikali iandae mswada basi hoja yake iwe ya kuliomba Baraza liiagize serikali iandae mswada na utakuwa ni Mswada wa Serikali. Endapo yeye mwenyewe Mhe. Mjumbe anataka kuandaa mswada, mjumbe basi hoja yake iwe ni kuomba kibali cha Baraza ili aandae mswada huo. Kwa ilivyo sasa hoja yake haieleweki inataka nini hasa yaani mswada wa serikali au kitu gani. Hii nataka Mhe. Abubakar Khamis Bakary atoe ufafanuzi.

Observation nyengine marekebisho ya katiba ya 9.3. Mimi nasema yale mambo aliyosema Mhe. Abubakar Khamis Bakary yasiorodheshwe kabisa. Lakini sisemi kimabavu mabavu hapana, yasiorodheshwe ili misingi ya (a) mpaka (f) kwani inaturejesha nyuma badala ya kwenda mbele. Utaifishaji wa ardhi na nyumba, utoaji wa elimu na matibabu bila ya malipo, ukatazaji poni na rahani ni mambo ambayo yalikuwa halali, yalikuwa sahihi kwa wakati ule wa mazingira ya Kimapinduzi.

Kwa mazingira ya sasa haki za binadamu suala la utaifishaji kulileta kwenye katiba linaweza kuogopesha na kuwatia hofu wawekezaji, kwani liko kinyume na haki ya kumiliki mali ambayo imo kwenye katiba yetu.

Aidha, sera ya sasa ni *cost sharing* yaani kuchangia gharama kwenye elimu na matibabu. Kwa hivyo, suala la elimu bure na matibabu bure kuliweka kwenye katiba ni kwenda nyuma. Vile vile masuala ya poni na rahani *(pawn and mortgage)* ni mambo ambayo hivi sasa yanakubalika katika vifungu vyetu vya fedha na mabenki. Kukataza mambo hayo kwenye katiba inaturudisha nyuma sana.

Mhe. Spika, mimi niliona nichangie mambo hayo, niweke hoja hiyo sawa na kwa kweli mengine tena mambo ya historia na mengineyo wakishasema, historia nzuri tunazo tujenge nchi yetu.

Mhe. Spika, jana ndugu yangu alilia hapa masikini, Mhe. Assaa Othman Hamad nae nusra alie, Mhe. Ali Suleiman Ali alitaka sote tulie. Lakini Mhe. Spika, tufike pahala tuelewane. “Serikali shirikishi ni suluhisho pekee kwa siasa ya Zanzibar”. Hayo kayasema jana Pius Msekwa. Umoja wa Kitaifa ni mhimili mkuu wa amani na utulivu. Hayo nasema mimi. Baada ya muda mtakuja mseme Mhe. Ali Mzee Ali alisema hivi.

Mhe. Spika, Rais Amani Abeid Karume watu wamempongeza, mimi nasema hivi, Rais Karume yeye ndio kisiwa cha amani na utulivu. Jina lake Amani, anapenda amani na amani ndio hii tayari.

Mhe. Spika, niruhusu kwa heshima na taadhima nisome *hansard* dakika 5 tu. Anasema "Hii *observation* ya pili inaeleza kwamba pande zote mbili wanaotaka vyama vingi, chama kimoja wanakubaliana suala moja muhimu la usalama wan chi hii. Umoja wa nchi hii, amani na utulivu wa nchi hii wanavyosema hilo ni la kwanza. Yaani watu wanasema yote vyama vingi, chama kimoja lakini la muhimu huyu mtu anasema "utulivu wa nchi hii kwamba hata maendeleo yawe mazuri kiasi gani, kama hakuna amani, usalama, utulivu pamoja na umoja, basi maendeleo hayo hawana haja nayo".

Huo ni mchango wako wewe Mhe. Spika, ulipokuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi mwaka 1992 unajadili hoja ya vyama vingi. Mhe. Spika, wewe ni mtu mwema, wewe ni mtu mzuri sana, wewe una sifa. Kwa sababu wewe Mhe. Spika, ulikuwa mjumbe Tume ya Nyalali, humu ndani wewe na Mhe. Ali Juma Shamuhuna. Haya uliyasema wewe wakati sheria ilipopitishwa hapa ya vyama vingi. Mwenyezi Mungu kakujaalia baadae umekuja kuwa msimamizi, leo unasimamia mustakbali wa vyama. Hongera sana una kila sifa, kila unalolitaka ndani ya nchi hii Mwenyezi Mungu atakupa kwa sababu una *CV*.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri Kiongozi shahidi na mimi ninakupa vile vile wasikie wote leo usiseme hili ni siri yetu mimi na wewe. Kwa hivyo Mhe. Spika, namalizia hapa, naunga mkono nawaomba wenzangu Mhe. Abubakar Khamis Bakary akija ku-*wind up*, uje pahala pazuri, kwa furaha na amani na tujenge Zanzibar mpya, tusameheane.

Mhe. Spika, Rais Amani Abeid Karume na Maalim Seif Shariff Hamad hawajasema chochote kule walisema tusameheane tu. Hayo mengine si yao ni ya Kamati ya Butiama. Tusameheane, tujenge nchi yetu na nchi tunaijenga.

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu akupe kila la kheri, akupe maisha marefu. Waheshimiwa Wajumbe Mwenyezi Mungu atujaalie kheri, tupendane, tujenge nchi yetu. Historia iandike zije *hansard* zisomwe. Suala la kwanza ndio, suala la pili ndio, la tatu ndio, kura za maoni ndio, mambo yamekwisha. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Huyo ndie *professor*, yaani leo namuongezea nyengine *professional logist.* Maana pale alipokuja kusoma *hansard* yangu sasa sina budi na mimi nimpe ule muda, cha kwangu eti. *(Kicheko)*

Namshukuru sana Mwenyekiti wa Baraza hili ambaye amechangia hivi punde.

Mhe. Juma Duni Haji: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii. Mhe. Spika, Mhe. Haji Faki Shaali anasema likishapigwa zumari vinanda huwa hata havifani, lakini na mimi nina wajibu kutoa mchango wangu.

Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mhe. Ali Mzee Ali kwa takriban amemaliza mjadala, lakini naomba na mimi nimuunge mkono zaidi. Kitu cha kwanza ningeomba kidogo tu kusahihisha aliposoma ile Kamati ya Wajumbe kamsahau Mhe. Bashange ambaye alikuwa ni mmoja katika upande wetu.

Sasa mimi nilitaka kidogo kusahihisha maelezo ambayo yamekuwa yakizungumzwa hapa kuhusu CUF kukataa kura ya maoni. Mimi bahati nzuri nilikuwa mjumbe kule Bagamoyo, kwa hivyo najua kilichofanyika kwa miezi 14 na wala si 18. Kama alivyosema Mhe. Ali Mzee Ali baada ya miezi 14 tulimaliza kazi yote na maana ya yote ni kwamba hata ile *document* yenyewe tulishaisahihisha ikawa tumeshaisoma kuwa hichi ndio kifurushi chetu.

Suala kubwa lililobaki ambalo Mhe. Spika, nashukuru nililiuliza mimi, nilimuuliza Mhe. Kingunge Ngombale Mwiru, ehe, bosi kifurushi hichi anatekeleza nani? Bi Zainab Omar Moh'd yupo hapa. Kimya kikapita kama dakika 3 akasema tutatekeleza sisi, nyinyi nani? Sisi serikali na chama. Tukawaambia tatizo linaanza hapo, tutaiharibu miezi 14 kwa tatizo hilo. Akasema tatizo gani? Nikawaambia kwamba mjadala huu na Bi Zainab anajua, siku za kwanza ilikuwa hata akisema anajaribu kusogea mbali nitaonekana nasema na babu Juma. Mwisho tukawa tunakaa mpaka saa 4:00 za usiku tunazungumza tunacheka kama sio CCM na CUF. Hiyo ni moja katika aliyoisema Mhe. Ali Mzee Ali kwamba mnapokaa pamoja hata zile dhana za kwamba huyu kumbe si samba ni binadamu zinaondoka.

Mhe. Spika, hata Rais Mstaafu Nelson Mandela anasema walipokutana kwa mara ya kwanza na kina De Clerk baada ya kukubaliana wale wajumbe wa upande wa serikali na wao, walipotoka wakasema *"after all we are all the mandarin".* Wakati ule upande mmoja hawa wakiona kama nusu watu, lakini walipokutana uso kwa uso wakakubaliana kumbe hakuna tofauti yoyote. Sasa na sisi mwanzo ilikuwa hivyo halafu basi.

Sasa nirudi kwenye pointi kwamba suala likawa anatekeleza nani? Sisi tukajenga hoja kwamba 1999 tulikuwa na muafaka ukafeli, tuliiachia serikali. Zikaja hoja kwamba hauna uhalali wa kisheria na kikatiba. Ukaja wa pili mwaka 2001 mimi sikuwepo lakini waliokuwepo Ikulu wanajua. "Meno ya mbwa hayaumani", leo tunafungua kitabu kipya, nao mnajua mwisho wake umeishia wapi, yakatokea yaliyotokea mwaka 2001, hiyo ni historia.

Lakini ukweli ni kwamba kila tulipoacha mfanye nyinyi leo mara ya tatu tuko hapa tunajadili. Tukasema moja katika tatizo la msingi la miafaka hii kufeli ni kwamba mchezaji na rifarii yumo uwanjani. *You can't be a player and a referee*. Kwa hivyo, tukamwambia sikiliza mheshimiwa, lakini Mhe. Abubakar Khamis Bakary siku hiyo aliniachia mimi. Nikawaambia kama hatukufanya pamoja hili maana yake hatujasafiana nia. *Problem* ilikuwa ni *crisis of confidence*. Tatizo la msingi la miafaka yote kufeli ni kukosa kuaminiana.

Mhe. Spika, kweli tulijadili tukafika pahala wenzetu wakasema tunakwenda kwenye chama chetu na sisi tukaja kwenye chama matokeo yake tunayajua, ikaja hoja ya kura ya maoni ambayo tumekaa miezi 14 haikuwahi kutajwa kwenye ajenda na ajenda tulikuwa tunazo tumeshazikamilisha na *document* tayari.

Kwa hivyo Mhe. Spika, msingi wa kilichosababisha mambo kuvurugika ni kukosa kuaminiana. Mwenyezi Mungu mkubwa sana Maalim Seif Shariff Hamad akasema Amani si Amani na mimi si Seif, babu Juma twende, namwambia ndio Maalim nenda, nyinyi ndio mliokuwa mnashindana uwanjani sisi tukicheza tu na ngoe. Kama nyinyi mtafahamu tatizo ni nini, sisi hatuna budi kufuata. Maalim Seif wamekutana na Mhe. Amani anaulizwa na Maalim, wewe huna wajukuu. Akamwambia ninao. Maalim Seif akamwambia na mimi ninao. Akamwambia hivi sisi leo ndio tuliokuwepo. Jamani Mhe. Ali kasema hapa, kuna wakati sote tulikuwa hatupo na mimi nilikuwa sipo hapa, mlipopitisha katiba hii mimi nilikuwa ofisa tu katika serikali, leo niko hapa. Kesho watakuja wengine hapa, lakini leo tuko hapa sisi ndio sisi. Mhe. Spika, ndio sisi tutakachokifanya hapa ndio kitakachoathiri huko tunakokwenda.

Mhe. Spika, Mapinduzi yalipokuwa yanatokea mimi nilikuwa darasa la 6 au la 7. hao waliofanya hayo walitaka sisi tuwe wamoja Wazanzibari. Kasema pale Mhe. Ali. Sisi tulioko hapa leo tunawaachia nini hao wanaokuja, hicho ndio walichoulizana Ikulu Maalim Seif na Mhe. Aman Karume. Wakasafiana nia. Tena sio vibaya mimi kusema, Maalim Seif anasema nilimwambia Aman kwamba mimi nimekukosea wewe Aman na wewe umenikosea mimi.

Wajumbe: Mhe. Rais Aman Karume.

Mhe. Juma Duni Haji: Mhe. Rais Aman. Naomba radhi Mhe. Spika. Lakini hivi itatusaidia nini. Yaliyopita si ndwele tugange yajayo tuwaachie wajukuu wetu hatima njema. Sote humu ndani tuna wajukuu, tunataka tuwaachie wenzetu jambo jema.

Mhe. Spika, wale waliosema maridhiano gani hicho ndicho kilichofanyika Afrika ya Kusini. Mandela alizungumza na Pickbota, mpaka Pickbota akapata

kiharusi. Hawakukubaliana mpaka akajiuzulu Pickbota. Alipokuja Mick Dicklack akasema mfunguweni Mandela tuone hiyo ndwele itakayotokea, kiruhusuni chama chake kifanye siasa. Wakakutana wakasema yaliyopita sindwele yaishe. Mick Dicklack anamwambia Mandela, tulikuwa kama tumegubikwa na mawazo kumbe kile kilichokizuri kwa wazungu ndio kizuri kwa Waafrika kumbe si kweli, wazungu walitambua hivyo kwamba kilichokizuri kwa Afrika Kusini ndio kizuri kwa wazungu na ndio kizuri kwa weusi. Yaani kilicho kizuri kwa Zanzibar mpya ndio kizuri kwa CCM, ndio kizuri kwa CUF na ndio kizuri kwa kizazi kijacho.

Mhe. Spika, kwa hivyo, hoja hii mimi nilipokuwa nikiisoma nilikuwa siisomi kama hoja ya CUF wala siisomi kama hoja ya CCM. Hii ni hoja inayobadilisha mfumo mzima na muundo wa utaratibu wa kubadilishana madaraka Wazanzibari kwa amani na utulivu kutoka kizazi kimoja kwenda kingine. Haiwezekani kabisa kwamba Wazanzibari kila miaka mitano kwanza wauwane, wagombane ndio tupate Rais aibu. Sisi tunasifiwa kwa uungwana, hakuna uungwana mkubwa kama kuishi kwa amani na utulivu.

Kwa hivyo, kwa mimi Mhe. Spika, lililo muhimu kuliko yote ni amani ya watu wetu na kizazi chetu. Tatizo tulilonalo na ndio maana hii kura ya maoni ikaambiwa ije kabla ya uchaguzi, ni kwamba tutayarishe mazingira yanayoruhusu wanaita *level playing field*

Mhe. Spika, haitowezekana katika mfumo uliopo sasa kumpata Rais wa 2010 akajenga serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa mfumo huu tulionao. Mfumo wa kumpata Rais kwa vurugu huwezi ukapata Serikali ya Umoja wa Kitaifa yenye amani. Mfumo utakaotuletea Serikali ya Umoja wa Kitaifa yenye amani na mshikamano ni mfumo uliokuwa unaruhusu mazingira hayo.

Na walichokiona viongozi wetu ni hicho, kwamba badala ya kuongejea mpaka tumeuwana halafu tena ndio turudi juu ya meza. Yaliyopita tumeshayaona yanatosha. Tushirikiane tujenge nchi yetu. Amani ni bora kuliko Katiba, kuliko uchaguzi, kuliko chochote. Vyote hivi havina maana kama hakuna amani.

Sasa nimalizie kwa sababu na wenzangu wanataka kusema, nimesema hapa suala la kura ya maoni kwamba Mhe. Abubakar Khamis amesema kuwa “au liweke utaratibu mwengine kwa njia ambayo Wazanzibari wenyewe kwa kupitia Wawakilishi wao waliowachagua wataona inafaa. Wengine wanasema aah! Musiende huko. Yote haya mtu anatizama eeh! Itakuwaje bora hili. Jamani Katiba hii imepitishwa mwaka 1979, sisi tumeikuta. Mfumo mzima tunaotayarisha hivi sasa tunategemea pengine uwepo mwaka 2025, 2030.

Kwa hivyo hapa tusimueke mtu mbele, Juma Duni atakuwa nani. Kwa hivyo hiki ninakikataa. Babu Ali Juma Shamuhuna atakuwa wapi, kwa hivyo hiki ninakikubali. Hiki si cha mtu. Hiki ni cha wananchi wa Zanzibar kwa ajili ya Zanzibar yao. (Makofi).

Hakuna hata mmoja aliyeota kwamba siku moja Nahodha angekuwa Waziri Kiongozi. Nani uliota Babu? Hatumjui nani Mwenyezi Mungu amemueka keshokutwa atakuwa Rais, hatumjui lakini lazima tuwatayarishie mazingira ya watu kurudia kwenye kumbukumbu kwamba hiki ndicho kilichowekwa na wazazi wetu.

Mhe. Spika, Mhe. Mugheiry, samahani Mhe. Samia na wengine humu ni wanafunzi wangu nimewasomesha na wengine wananiambia humu hata siwakumbuki. Mhe. Mwinyihaji tulikuwa tunakaa wote pale Rahaleo tunasoma, leo yeye doctor sijui wa kitu gani, mimi nipo hapa. Lakini tupo hapa tuna mchango wa kutayarisha hatma ya vijikuu vyetu. Kila mmoja ana mchango wake. Uwezo wangu mimi ni tofauti na wa Bi. Asha Abdulla, uwezo wangu mimi ni tofauti na Mhe. Mulla lakini sote ni sehemu ya Zanzibar mpya. Zanzibar mpya yenye matumaini mapya kwa kizazi kipya.

Mhe. Spika, ninakushukuru. (Makofi).

Mhe. Spika: Ninafikiri tunaelekea pazuri. Sasa nimkaribishe Mhe. Machano Othman Said – Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi na baadae tumsikilie Mhe. Said Ali Mbarouk.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi ninaomba nichukue nafasi hii, kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake na rehema zake ambazo zimetufanya leo hii siku ya Ijumaa ni siku tukufu kuwa hapa kuchangia hoja hii.

Lakini pia nikushukuru na wewe binafsi kwa sababu tangu jana tumekuwa tukiomba sana nafasi hii ili tuweze kuchangia na Mhe. Asha hapa anasema akikosa anasikitika sana.

Mhe. Spika, nianze hoja hii kwa kumpongeza sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Dr. Amani Karume kwa kutekeleza kwa vitendo dhana ya amani na mshikamano lakini pia na maendeleo. Kwa sababu lazima unapokuwa na amani na mshikamano lazima uwe na maendeleo. Sasa tumshukuru basi Mhe. Rais wetu kwa kutufikisha katika hatua hii ambayo ninafikiri kila Mzanzibari anajivunia na maendeleo yameonekana.

La pili Mhe. Spika, na mimi nianze kwa sababu muda wenyewe ni mdogo, niseme mimi ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM. Kwa hivyo ile dhana ya watu kwamba tuseme hapa chama tuweke pembeni, mimi kwangu hainiingii sana kwa sababu kila ninapotembea na U-CCM wangu ninao lakini nitazungumza kwa maslahi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nina ombi mimi. Ombi langu ni kwamba hoja ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary, ina vifungu karibu 9. Inavyoelekea vifungu vyengine vitakubaliwa na vyengine havikubaliki. Nimshukuru sana Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban - Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora.

Ningeliomba basi Baraza hili pengine vile vifungu vya Mhe. Ramadhan Abdulla alivyovitaja mwanzo viingizwe katika hoja wakati wa kuifania majumuisho, ili navyo tuangalie uzito wake na tunachokikubali hapa, tunakubaliana na kipi. Lakini na Mhe. Samia naye kazungumza na mimi ninaunga mkono yale mambo sita ambayo yalikubaliwa mwanzo kwa Azimio la Butiama.

Pale kuna kifungu chengine cha ziada ambacho na mimi ninahisi tunapozungumza tukifikirie sana katika utaratibu wa hiyo Serikali Shirikishi. Kinazungumza kwamba hili jambo ambalo tunazungumza leo na ambalo lilikuwa miaka miwili nyuma limezungumzwa basi liwe linafanyiwa mapitio kila baada ya miaka mitano.

Kwa hivyo hili mimi ninaliunga mkono. Inawezekana baada ya huko miaka ya mbele kama alivyosema Mhe. Juma Duni kwamba ikawa hakuna haja tena hata pengine ya kukaa kujadili mambo haya.

Jengine Mhe. Spika, ambalo Mhe. Ramadhan Abdulla alilitolea ufafanuzi wake lakini mimi hili ninahisi nitoe ufafanuzi wangu au maoni yangu. Ni kuhusu kubadilishwa kifungu cha Katiba cha 61. Mimi ninahisi kwa sababu bado tunaendelea na Rais mtendaji, ninahisi tusifanye marekebisho kwenye kifungu hiki cha Wakuu wa Mikoa. Tuendelee kumpa Rais dhamana ya kuteuwa Wakuu wa Mikoa, tumuamini kwa nia njema na hafungwi kwa sababu kifungu hakisemi kwamba asichaguwe mpinzani, akitaka atachagua. Lakini tukumbuke kwamba katika nchi yetu ya Tanzania na sisi Zanzibar tukiwemo tuna vyama 19 vya siasa, tuna mikoa 5 ya kiutawala.

Kwa mfano itokezee tu, kwa sababu tunapozungumza hapa tusizungumze katiba kwamba itakuwa na vyama viwili tu, tuzungumze chama chochote katika hivyo 19 kinaweza kikawa na wajumbe ndani ya Baraza la Wawakilishi. Tuna mikoa 5, ukiwa na vyama 19 humu ndani nani utampa mkoa na nani umwache. Kwa hivyo, mimi nahisi hili linaloendelea humu ndani ni jambo

jema, Rais aendelee kuwachagua wakuu wa mikoa, aendelee kuwachagua wakuu wa wilaya na wafanyekazi zao za kiserikali kama ilivyopangwa.

Mhe. Spika, kuhusu kura ya maoni naungana na wale wenzangu wote waliosema kwamba twende kwa wananchi na katiba ya Zanzibar inasisitiza hivyo, katika kifungu cha 9 katiba, kwamba Zanzibar itakuwa ni nchi ya demokrasia na haki za kijamii. Kwa hivyo, inaelezwa rasmi kwamba mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe, ambapo nguvu na uwezo wowote wa serikali kufuatana na katiba utatoka kwa wananchi wenyewe. Usalama na hali nzuri kwa wananchi itakuwa ndio lengo kubwa la serikali.

Mhe. Spika, naomba tusikibadilishe kifungu hiki na wala tusikiongeze yale maneno Mhe. Abubakar anayopenda kuyaongeza, kwa sababu ukisoma kifungu nambari 10 cha katiba hii inaondoa haja ya yale ambayo Mhe. Abubakar kayasema. Kwa sababu kifungu nambari 10 kimeeleza kila kitu kuhusu uendeshaji wa serikali na madhumuni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwahudumia wananchi. Sasa ukikirekebisha kifungu cha 9 na hicho kifungu cha 10 unakiuwa na kitakuwa hakina maana. Kwa hivyo, mimi nahisi tusibadilishe nambari 9 na nambari 10 kiendelee kuwepo kama kawaida.

Mhe. Spika, kuhusu uwiano wa waziri kwamba pengine kura za Urais ndio zitumike kupata mawaziri. Mimi nafikiri Baraza la Wawakilishi tuna utaratibu mzuri sasa hivi wa kuwapata Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa viti maalum. Kwa hivyo, tutumie utaratibu ule ambao upo sasa hivi katika kufanya mambo yetu yote ambayo tutakubaliana katika Baraza hili la Wawakilishi kwa kupitia kwa wananchi.

Mhe. Spika, Zanzibar tunaendelea, lakini sote tuna vyama vyetu vya kitaifa. Kwa hivyo, tunapozungumza hapa tunawakilisha Wazanzibari wote, lakini pia tunawakilisha vyama vyetu vyote ambavyo vipo. Kwa hivyo, kuna umuhimu wala sio kwa kupuuza nina hakika mimi hii hoja ya Mhe. Abubakar japo kuwa watu wanasema sio ya chama, lakini sijui kama chama chao hawakuiona hata kidogo, lazima watakuwa wameiona. Sisi tuliunda kamati mbili za muafaka na mazungumzo, tukaletewa mazungumzo yale Butiama tukayapitia na tukayabariki tuliyoyabariki na tunaomba tukubaliane yaende mbele yafanyekazi.

Mhe. Juma Duni alizungumza kwamba muafaka wa mwaka 2001 haukufanya kazi kwa sababu ulisimamiwa na serikali. Lakini mimi naelewa kwamba muafaka ule ulifanikiwa sana na mambo mengi yalitekelezwa wakati tuko katika chama kimoja. Kulikuwa na wasimamizi wa pande mbili, sijui kama nitakuwa niko sahihi au si sahihi, lakini kwa CCM waliokuwa kwenye tume ya muafaka, kwanza Mhe. Asha alikuwemo, Mhe. Mapuri alikuwemo ambaye ni

kiongozi alikuwa, Mhe. Vuai Mwakiembe na Mhe. Feruzi na baadae akaingia Mhe. Shamuhuna.

Kwa upande wa CUF na wao walikuwa na watu wao watano, Mhe. Fereji alikuwemo na akajenga siasa nzuri ndio akaingia Barazani baadae, Mhe. Jussa, Mhe. Abubakar alikuwemo, Mhe. Makame marehemu huyu na Mhe. Nassor.

Katika muafaka huu tulibadilisha katiba kutokana na mapendekezo ya tume ya muafaka. Mabadiliko ya 8 ya katiba ya Zanzibar amabyo yalifanyika 2002, yalitokana na mapendekezo ambayo sasa wao wenyewe tume alipeleka serikalini na wakasema wao wenyewe kwamba baadae wapelekwe kwao kuyafanyia marekebisho na yalipelekwa, yakaletwa kwenye Baraza la Wawakilishi tukakubaliana nayo. Ndio Tume ya Uchaguzi ikarekebishwa, ikaanzishwa tume ya uajiri mahakama, afisi ya mwendesha mashtaka yote yalitokana na muafaka huu.

Mhe. Spika, nazungumza haya kwa sababu sisi kama wana siasa msingi wetu ni watu na sisi tusiogope kwenda kwa watu, kwa sababu ilivyokuwa hili ni jambo jema basi na watu watalitaka tu, kwa sababu hakuna Mzanzibari ambaye hataki jambo jema. Tutakwenda tutafanikiwa, tutarudi na tutatengeneza mambo yetu vizuri.

Mhe. Spika, kama tulivyosema haya mambo tusiyawekee muda mdogo, lakini tumalizie kabla uchaguzi wa Oktoba 2010, ili tukienda kwenye uchaguzi kila mtu apate haki yake halafu baadae tuangalie tunafanya nini. Sasa haya mambo ya pande mbili tusitiliane mashaka huku wala tusitiliane hofu huku. Mimi nahisi mambo makubwa ambayo tumekubaliana mwanzo na Mhe. Ramadhan aliyasema na Mhe. Samia Suluhu, bahati nzuri Mhe. Samia ni mjumbe wa kamati kuu ya Chama cha Mapinduzi.

Kwa hivyo, Mhe. Abubakar atakapokuja kufanya majumuisho yake, tusije tukafika pahala tukasema hilo halikuwemo halikuwemo, bora yangeandaliwa yale katika kipindi cha mchana yale ambayo tunasema haya yaingizwe, tulipitie moja baada ya moja. Mhe. Spika, kama kanuni zimekaa vibaya tuweke kando kanuni, lakini hoja iwe inajadiliwa namba moja tukikubaliana, ije namba mbili tukikubaliana ije namba tatu, lakini tusije tukakubaliana hoja yote ilivyo halafu tukaja tukasema aah! Hatukukubaliana hivyo, tulikubaliana hivi. Mimi nafikiri tukifika hapo basi haya mambo yatakaa vizuri na tutakuwa katika salama.

Mhe. Spika, kwa sababu wenzangu wengi na wao wanataka kuchangia, naomba nimalizie hapo. Nakushukuru sana.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii muhimu sana kwa mustakabali wa nchi. Mhe. Spika, jana ulifanya *preemption* ya mchango wangu. Pale uliposema kwamba wewe ulifanya jitihada kubwa ya kuunganisha Wazanzibari baada ya uchaguzi wa mwaka 1995. kwa kweli ile ilikuwa ndio dibaji ya mchango wangu.

Mhe. Spika, katika mtu ambaye anaangalia kwamba Zanzibar inapata mustakabali mzuri, Wallah nakuheshimu sana. Ni kweli wakati ule ambapo sisi hata hatusemi vizuri, wawakilishi katika Baraza basi ulifanya jambo moja zuri sana la kijasiri. Wewe mwenyewe ulisema ulifanya vile bila ya kutumwa na chama chako, lakini uliona ule ni wajibu wako. Ulifunga safari ukaja tukazungumza sana. Ile mimi naiona kwamba ndio *first engagement to advice process.* Kwa kweli ndio ambayo imezaa mambo yote haya.

Lakini mtu wa pili ambaye nataka nimuheshimu sana ni Mhe. Ramadhan Nyonje, kwa dhati ya moyo wangu. Kipindi kile ambacho hali ni mbaya sana wawakilishi tunapishana kama dau, basi alinialika mimi na Mhe. Haji Faki Shaali kufuturu nyumbani kwake, *at that time* na akatuchukua kwa gari hapa tukenda tukafutari tukarudi. Kwa kweli ni mtu wa aina yake sana, mimi namuheshimu sana.

Mhe. Spika, pongezi nyingi zinahitaji viongozi wa Serikali wa Jamhuri wa Muungano, Dk. Aman, viongozi wetu wa vyama, Maalim Seif na wengine ambao wameandaa mazingira ambayo leo tunajadili jambo zito na muhimu. Mimi naomba sana kwamba mazingira haya yatufikishe pale ambapo Wazanzibari wanapahitaji. *Inshaallah* kwa Ijumaa ya leo basi kheri itapatikana.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye hoja moja kwa moja. Nina mchango mdogo sana Mhe. Spika, usiangalie sana. Katika pendekezo linalohusiana na kifungu cha 42 cha katiba ambacho kinahusiana na upatikani wa mawaziri. Mimi ningewashauri wenzangu tukubaliane na hoja ya Mhe. Abubakar kwamba mawaziri waje wapatikane kwa kura za uwiano wa Rais. Sababu yangu nzito ni kwamba tukienda na viti tu ndani ya Baraza, basi tutauwa vyama vidogo. Kwa kweli vyama vidogo vinahitaji kulelewa na hatimaye kuwa ni sehemu ya Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, mimi ushauri wangu ni kwamba ifanywe mipango ya mabadiliko ya sheria au katiba, ili chama chochote ambacho kitapata kura baina ya asilimia 5 na 10 ya kuwa na Rais, basi hicho chama kipatiwe nafasi ya kuteuliwa kipate mwakilishi katika Baraza na halafu ateuliwe kwa nafasi. Kwa sababu chama kupata asilimia 10 ya kura za Rais halafu tukakiwacha nje ya mstari, kwa kweli sio jambo zuri. Kama kuna vyama viwili au vitatu vimepata asilimia 10 kila

kimoja, yaani jumla asilimia 30 kisha tukawaacha nje tu kwa sababu hawana kiti ndani ya Baraza, tutakuwa tunaviuwa na tunavilemaza.

Kwa hivyo, mimi nashauri kwamba hivi vyama katika utaratibu ambao utawekwa. Ushauri wangu ni kuwa vyama hivi ambavyo vitapata baina ya asilimia 5 na asilimia 10 kama ni viwili, basi vile viti viwili vya upinzani wapewe wao ili waingie katika Baraza halafu wachaguliwe kwa nafasi za uwaziri. Kama ni zaidi ya viwili basi zile nafasi 8 za Rais ziangalie kusaidia katika hili, kwa sababu tukiviweka nje vyama hivi basi vitakuwa ni waangalizi katika *process* ya kidemokrasia, lakini hawatapata nafasi ya kuingia katika vyombo hivi muhimu na wao wakajijenga ili baadae wakapata nafasi vizuri zaidi. Kwa hivyo, ushauri wangu ni huo.

Mhe. Spika, kuhusu suala la pendekezo la makamo wawili wa Rais kama maamuzi ya Butiama. Suala hili namuomba mtoa hoja, kwa sababu tumezungumza na wenzetu wengi basi akubaliane na hoja hii na ile ya uwaziri kiongozi ai-*drop*. Kwa sababu katika mambo haya Mhe Spika, kuna *give and take*, unawaangalia wenzako wengi wanasema nini, unasema *ok* hii hoja ina nguvu. Kwa hivyo, mimi nashauri kwamba akubaliane na hoja hii, ile yake waziri kiongozi ai-*drop* tukubaliane na hii inayotoka kwa wenzetu. *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kifungu cha 61 cha katiba kuhusiana na uteuzi wa wakuu wa mikoa na wilaya. Hapa zimetoka hoja namna mbili. Kuna wengine wanasema wakuu wa wilaya wasihusishwe na kuna wengine wanasema wakuu wa mikoa na wilaya wasihusishwe. Mimi ningeshauri kuwa mtoa hoja akubaliane kwamba wakuu wa wilaya wasihusishwe kwa sababu hawa, na mimi nimeshawishika na hoja zao kwamba hawa ni *administrator* zaidi kuliko wana siasa, wanazungumzia zaidi utawala kuliko wanasiasa. Lakini wakuu wa mikoa wana *roll* mbili, wana *administrator* na pia ni wanasiasa wanaingia Barazani.

Kwa hivyo, mimi ningeshauri kwenye hoja hii wangekubaliana na hoja ya Mhe. Abubakar kwamba Rais ashauriane na wenzake katika kuangalia hili. Au labda kuwe na hoja kwamba kama labda walivyokuwa Bara, wakuu wa mikoa wasiingie Barazani hapo ndio tunaweza tukajadili vingine, kama kuna hoja hiyo mimi sina tatizo. Kama tunakubaliana kama Bara kuwa wakuu wa mikoa wawe ni *absolutely* ni *administrator officer* katika *respectively* zao, mimi hilo sina tatizo. Lakini kama na wanasiasa wanaingia humu basi ni lazima tukubaliane na hoja ya Mhe. Abubakar.

Mhe. Spika, kuhusu pendekezo la kuunda kamati ya wajumbe 6. Hili mimi naona ni muhimu, kwa sababu moja. Mhe. Spika, hivi sasa hii hoja ni ya Mhe. Abubakar Khamis kama ni Mwakilishi wa Mgogoni, tukiikubali itakuwa ni

hoja ya Baraza la Wawakilishi, kama tutaikubali na ninaona kwa anavyonitazama Mhe. Tafana Kassim anahisi kama tutaikubali. Sasa kama tutaikubali, itakuwa ni hoja ya Baraza la Wawakilishi. Sasa ikiwa ni hoja ya Baraza la Wawakilishi Mhe. Spika, ili itekelezwe na serikali, basi kuna umuhimu wa kufanya ile inaitwa *oversight roll* ya Baraza. Ikiwa ni hivyo, basi umuhimu wa uwindaji wa *enter parliamentary committee* ya ku-*exercise* hiyo *oversight roll* ni muhimu sana katika hoja hii, tusiangalie masuala ya vyama. Tuangalie kwamba hii hoja itakapopita itakuwa ni hoja ya Baraza la Wawakilishi na kama ni hoja ya Baraza la Wawakilishi, basi lazima sisi kama Bunge lazima tuangalie tuna *roll* yetu ya Kibunge ya kuiangalia serikali utekelezaji wake.

Mhe. Spika, katika suala hili ni lazima tuunde kamati ndogo. Mimi nilidhania labda mapendekezo ambayo yangekuja, labda kamati ndogo au kamati kubwa itakuwa na gharama, tuseme kamati kubwa basi ingependekeza watu 4 badala ya watu 6. Umuhimu wa kuwa na kamati ya kuiangalia *oversight roll* ya suala hili muhimu Mhe. Spika, ni jambo muhimu sana na kwa kweli mimi nawaomba sana wenzangu katika hili Mhe. Spika, tukubaliane kuwa ni muhimu sana kuwa na kamati.

Vile vile nilikuwa na dhana kwamba ingekuwa serikali inahitaji wao walitekeleze moja kwa moja. Hii hoja imepelekwa karibu siku 10 nyuma. Kuna utaratibu hapa wa kuteka nyara hoja. Mhe. Spika, mara moja hapa Mhe. Abubakar alipeleka hoja ya bendera. Ghafla serikali ikaiteka nyara hoja wakaipeleka wao. Sasa katika hali ile Mhe. Abubakar asingesema kama na mimi nishirikishwe kwa sababu hoja imetekwa nyara na serikali na wameipeleka wao. Sasa katika hoja hii ingekuwa serikali ina hamu ya kuisimamia wao moja kwa moja, basi serikali ingeiteka nyara siku ya pili tukamuona Mhe. Dk. Mwinyi anaiwasilisha. Kwa hivyo, Bunge au Baraza hili lingelikuwa halina sababu ya kusema na sisi tushirikishwe kwa sababu hoja tayari imeshatekwa nyara na serikali na wameshapeleka wao.

Lakini hata hivyo, Mwenyezi Mungu akijaalia, kama yalivyo mategemeo yangu, itakuwa ni hoja ya Baraza, basi umuhimu wa kuwa na *oversight responsibility* yetu kuona kwamba yale ambayo yameagizwa yametekelezwa kabla ya uchaguzi unaokuja. Mhe. Spika, mimi naomba hili tukubaliane.

Namaliza kwa kusema kwamba Mhe. Spika, kama nilivyokuambia naafiki kuwa twendeni kwa wananchi kabla ya kufanya uchaguzi, ili tuandae utaratibu maalum ili tuangalie mambo mazuri.

Mhe. Spika, namaliza kwa kusema kwamba Mhe. Dk. Aman ni Rais wetu hivi sasa, ana wajibu wa kuona kwamba anaondoka na kuiwacha nchi hii ikiwa

katika hali nzuri yenye utulivu wa kutosha na utulivu wake uwe unaendelea sana. Sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuna wajibu mkubwa wa kumsaidia Rais wetu, ili kuona kwamba kazi hiyo muhimu ya kikatiba anaifanya, na kwamba maamuzi yetu tutakayoyafanya leo jioni Mhe. Spika, naomba tusiangalie kwa miwani *green* au *blue.* Tukiangalie kwa *green* ya Kisiwandui au *blue* ya Mtendeni, kwa kweli tutakuwa hatufiki. Tuiangalie na tufanye maamuzi hoja hii kwa miwani yenye vioo viwili, *green* na *blue*. *Green* ya ardhi ya Zanzibar na *blue* ya bahari ya Zanzibar. Mhe. Spika, nakushukuru sana. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hiyo na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuniweka hai mpaka leo nikaweza kupata nafasi hii, kwa sababu jana pia sikulala, nimeomba hii nafasi mpaka ninalia machozi ya damu.

Mhe. Spika, naanza kwa kifua mbele kabisa kwanza kumpongeza Rais wa Zanzibar Dk. Aman Abeid Karume kwa kutuongoza vizuri na kutufikisha katika hatua hii ya maelewano, maridhiano na mategemeo ya mustakbali wa maendeleo ya Zanzibar yetu njema tuitakayo yenye amani na utulivu.

Natoa pongezi pia kwa Mhe. Rais Kikwete kwa uongozi wake na pia akiwa Mwenyekiti wa chama kusimamia jambo letu hili. Pongezi nyingi sana kwa katibu mkuu wa chama cha CUF Maalim Seif Sharif Hamad bin Mjaka au Sheikh Mjaka, kwa kufikia maridhiano hayo pamoja na Mhe. Aman. Lakini kwa dhati pia nampongeza Katibu Mkuu Rajab Yussuf Makamba wa Chama cha Mapinduzi, kwa jinsi alivyoshirikiana na kamati hii ya mazungumzo ambayo imefanya kazi nzuri sana na ambayo kwa busara na hekima za Mhe. Aman na kwa kuonesha kuwa Mhe. Aman hana upendeleo wala ubaguzi, akatukumbuka na sisi wanawake na ndio tukampata Mhe. Zainab kuwa katika kamati ile. Mhe. Zainab hongera sana.

Mhe. Spika: Twende kwenye *point* moja kwa moja.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, tutakwenda huko, lakini lazima hii ni *acknowledge*, kwa sababu haiwezekani hapa tulipofikia tusingefika kama hivi. Nakushukuru sana kwa maelekezo yako na nakuridhia na kukubalia yote.

Mhe. Rais ana nia njema na alianzia mbali, tulianzia kule alikosema Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi katika utekelezaji na kuridhia masuala ya muafaka, kwa ajili ya usalama na utulivu wa nchi yetu na tukawa na ile tume, ambayo imifanya kazi nzuri.

Tukiangalia baadhi ya mambo yale likiwemo lile la kurekebisha Tume ya Uchaguzi, kuanzisha Daftari la Kudumu la wapigakura na kuunda Afisi a Mkurugenzi wa Mashtaka. Sasa masuala haya yote mazuri yamefanywa kwa nia njema ya Mhe. Rais na tukafika hapa tulipo, leo tunalo hili jambo ambalo limetokana na chama chetu baada ya mazungumzo na makubaliano, yaliyopelekea kuzaliwa hoja hii ambayo Mhe. Abubakar Khamis Bakary ameiwasilisha.

Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Abubakar Khamis Bakary ni mtu muhimu sana pamoja na zile sifa ambazo amepewa na Mhe. Ali Mzee Ali, basi na nyengine nazo. Kwa mfano, Mhe. Abubakar Khamis Bakary aliwahi kuwa Mwenyekiti Mwenza wetu na alituongoza vizuri sana kwa kushirikiana na Mhe. Ramadhan Omar Mapuri. Hayo ndiyo matunda na sisi wengine tulifanyakazi kwa bidii ndio maana tulipata *promotion* mimi na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji tukawa hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, tukija kwenye hoja yenyewe kwanza naunga na kukubali kwa dhati kabisa maelezo, miongozo pamoja na mchango uliotolewa na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora, Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji, kwa sababu hayo ndiyo maelekezo ya Chama chetu cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nakubaliana na hayo, lakini naongeza machache kidogo. Katika suala namba moja Mhe. Rais ndiye atakayekuwa na mamlaka ya mwanzo kabisa. Kutokana na hali hiyo, kile kifungu ambacho tunasema mawaziri watokane na viti, basi tunaweza pia kumpa nafasi hiyo tena Rais atakayekuja afanye uteuzi wa mawaziri.

Nadhani hili litasaidia sana Mhe. Spika, kwa sababu huyu akiwa ndiye Kamanda Mkuu na kuweza kuchagua wale watu. Kwa kweli kwa hali hii ambayo tunayo na maelewano pamoja na maridhiano, basi Rais atayekuja ataweza kufanya uteuzi mzuri wa mawaziri. Kwa hiyo, serikali itakwenda vile tulivyokusudia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu suala la Wakuu wa Mikoa. Jambo hili pia nafikiri tumuachie Mhe. Rais kwa vile atakuwa na uwezo na hawa Wakuu wa Mikoa ndio watendaji, yaani ndiyo mikono yake kule ni vyema kuwa na uwezo. Kwa hivyo, yeye apate nafasi ya kuteua wale wasaidizi kwenye mikoa, ambao ataona wanafaa.

Kwa mfano, watu hawa wasiwe wanatokana na chama, kwa sababu tunaweza kurudia kule ambako hatukutaki.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nakuomba umalizie.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, namalizia. Ninachotaka kusema pamoja na hayo yote wazo la Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi la kupitia kifungu kwa kifungu ni muhimu nadhani tukifanya hivyo tutaepuka kwamba hili tulitaka liwe hili na lile vile, yaani tutakuwa tumekwenda vizuri sana.

Lakini hii hali ambayo tupo nayo, kwa kuwa unanilazimisha nipunguze na mimi nakukubalia, kwa sababu wewe ni mkubwa wangu katika Baraza hili. Kwa kweli hali hii ya maridhiano na makubaliano, ni hali ambayo itatujengea heshima kubwa sana na watu wanaweza kuja kusoma hapa kwetu jinsi tulivyofikia maridhiano haya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kusema kitu kidogo tu kwa ajili ya kuunga na Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Siku ile ya uzinduwi wa Kituo cha Utafiti wa Malaria pale Mwanakwerekwe, ilikuwa ni siku ya furaha sana pamoja na mvua ilikuwa nyingi, lakini hatukujali hivyo. Ujumbe wa pale ulikuwa mkubwa sana, yaani mimi nilikuwa nimekaa na Maalim Seif Sharif Hamad (Sheikh Mjaka).

Sasa kuna watu walimuuliza Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwamba, yule aliyekaa pale na kuzungumza na Maalim Seif Sharif Hamad, basi Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii alishtuka na kusema wewe humjui waziri wako, kwa sababu walikuwa ni wafanyakazi wa wizara yake.

Kutokana na hali ile basi Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa ushawishi wake alimwita shawishi mkubwa Dk. Malik akamwambia sikiliza wewe unavyosema, basi Dk. Malik moja kwa moja alikwenda kwa Maalim Seif Sharif Hamad na kumwambia watu wanauliza huyu bibi hapa ndiye mkeo, yaani jinsi yale mahaba na maridhiano, basi nilisema wananitafutia balaa kwa bibi Awena. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa sababu mimi ninayemchumba wangu huko Chama cha CUF anaitwa bwana Juma au Jusa. Lakini huyu namuweka mwisho mpaka siku ile ambayo tutakubaliana na kufanya uchaguzi kwa amani na kuweza kuunda serikali zetu katika hali ya amani. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hivyo, hapo ndio harusi yetu na bwana Jusa itakuwa, ikiwa mimi nitaendelea kupata ile wizara yangu niliyopewa ambayo imeundwa mitaani, yaani Wizara ya Elimu na yeye atakuwa Wizara ya Tawala wa Mikoa na Vikosi, basi mambo yatakuwa mazuri.

Mhe. Spika, hali hii inaonesha jinsi gani watu wa Zanzibar tulivyo wamoja na kupendana na lazima tuendeleze hilo, ambalo tutafikia kwa kuunga mkono hoja hii ya kwenda kwa wananchi, kwa ajili ya kupata Serikali ya Umoja wa Kitaifa au Shirikisho.

Kwa sababu sisi hatuwezi kuwa tofauti na watu wengine katika dunia, yaani dunia yote inahitaji maridhiano pamoja na masikilizano. Kwa mfano, tunapokwenda huko kwa wakubwa wanatuuliza nyinyi vipi huko Zanzibar, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete anasema watayamaliza wenyewe, hivi ndio tunayamaliza katika hali ya kupenda, tushirikiane pamoja na kujenga nchi yetu kwa usalama na amani.

Kwa hivyo, wananchi wasiwe na wasi wasi na wala hoja hii si mbaya, hivyo mutusikilize na watu wote wanataka kuwa na maendeleo na maendeleo yoyote hayaji kama hakuna amani na utulivu. Kwa hiyo tutakwenda huko na wala msiwe na wasi wasi kwa kuanza kuimba nyimbo mbaya kwa ajili ya kubembelezea watoto haifai. *(Makofi)*

Isipokuwa mambo yote yatakwenda vizuri chini ya uongozi wa Rais wetu, kwa kuwa sisi wenyewe tuko *committed* hatutaki mambo yale yarejee tena.

Mhe. Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii japo sio haki wengine walipata 20 na mimi nipate 7, lakini nimepokea kwa sababu ni amri yako.

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai leo na kuniwezesha kuja kuchangia nikawemo katika historia ya kusema machache kwenye hoja hii.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana mtoa hoja na kwa sababu nampongeza hii kazi ilifanywa miezi 14 au zaidi lakini haikufikia mwisho na ilifika katikati. Sasa yeye kwa uoni wake na kwa kuona Zanzibar pamoja na kuitakia mema Zanzibar, aliona bora ailetee hoja, ili hili jambo lifanyike na litekelezeke. Mhe. Abubakar Khamis Bakary tunakushukuru kwa kuitakia mema Zanzibar. *(Makofi)*

Vile vile nimshukuru Mhe. Rais pamoja na Katibu Mkuu wa CUF Maalim Seif Sharif Hamad, kwa kweli wote hao ni watu wangu wa karibu sana tena wanawafahamu vizuri sana. Kwa hivyo, nawaamini sana kwamba wakiamua kitu wanaweza kutekeleza. Kwa maana hiyo, sina kabisa katika moyo wangu

kwamba nitaogopa hili halitekelezeki, kwa sababu waliolianza wanaweza kufanya kadri Mwenyezi Mungu alivyowajaalia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sisi tunafahamu kwamba mbele yetu yupo Mwenyezi Mungu, ambaye anaweza kuamua jambo wakati wowote na likawa. Kwa kweli siku zote miafaka imepita na haya yameshindikana, lakini siku moja tu Mwenyezi Mungu alisema sasa leo kutaneni, ili Zanzibar ibaki katika hali ya salama na Mwenyezi Mungu amefanya hilo na limekua *alhamdulillah*.

Kwa hivyo, ninachokiomba kwa wenzangu kwamba tusiweke kitu chochote mbele zaidi ya Mwenyezi Mungu, yaani tukiweza kumuweka Mwenyezi Mungu basi hakuna litakaloshindikana hata moja au kutofanyika. Kwa sababu haya yote yamekuja kwa sababu ya Mwenyezi Mungu na sisi siku zote tunaomba dua, hapa tunaomba pamoja na sehemu nyengine tunaomba, ili Zanzibar yetu ibaki salama kama ilivyokuwa zamani.

Mhe. Spika, Serikali za Umoja wa Kitaifa zimeanza tokea wakati wa Mapinduzi na haidhuru kwa Chama kimoja cha *Afro Shirazi Party*, lakini ilikuwepo Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kwa sababu mlikuwa na rangi tofauti ndani ya Baraza la Mawaziri. Kwa hivyo, leo sijui tunakiogopa nini?

Nadhani tutakwenda kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kuchanganyika pamoja, kwa ajili ya kufanyakazi kwa maslahi ya wananchi wetu. Hivi sasa nchi yetu imekaa au inaning'inia kama uzi, yaani kitakapokatika kile kijizi kidogo basi nchi hatuna tena. Lakini tutakaposhirikiana nchi yetu itarudi na tutakaa na kuweza kujenga nchi yetu kwa pamoja kwa ajili ya maslahi ya Wazanzibari.

Kwa sababu leo Wazanzibari wote wako macho pamoja na masikio wazi kwa ajili ya kutusikiliza sisi. Kwa mfano, hapa asubuhi magazeti yametoka na kuandika kuwa "*CUF imekwaa kisik"i*. Mhe. Spika, nataka niwaambie waandishi wa habari kwamba CUF haijakwaa kisiki, isipokuwa CUF imeruka kisiki na CCM vile vile na tutakaa pamoja kwa ajili ya kuamua hatima ya Wazanzibari. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tuache kukaa kitako na kutudhania mambo ambayo hayapo, ikiwa CUF wameleta hoja Barazani au Mhe. Abubakar Khamis Bakary ameleta hoja Barazani na yeye ni CUF. Kwa kweli CCM tokea jana sijamsikia mtu ambaye amepinga na haidhuru jamaa yangu Mh. Haji Mkema Haji kwanza alisema sikubali hoja, lakini mwisho alirudi na kusema anaikubali hoja, kwa ajili ya kwenda kwenye marekebisho.

Pamoja na hayo Mhe. Abubakar Khamis Bakary alipoleta hoja hakusema kwamba lazima fuateni hili, isipokuwa alileta *option* mbili, ambapo tukiiona moja inaturidhisha basi tuifuate.

Kwa hivyo, nadhani kama sote tunaona marekebisho ni bora, basi twende kwa wananchi, kwa sababu wananchi ndio waliotuleta hapa na sisi kwa upande wetu hatujakataa na wala hatusemi hatuyataki marekebisho ya Katiba, kwani sisi tumeletwa na wananchi. Hivyo, tutafanyakazi kwa ajili ya Wazanzibari na tutashikana pamoja na kusimama wima ili kuitetea Zanzibar.

Mhe. Spika, Zanzibar itabaki Zanzibar milele kama alivyoiumba Mwenyezi Mungu na wala hakuna zaidi kuliko Mwenyezi Mungu. Kwa maana hiyo, wale wote wasioitakia mema Zanzibar, basi Mwenyezi Mungu atawashtaki na kuwahukumu kwa ile nia yetu ambayo ni safi na yeyote ambaye yumo humu ndani ya Baraza hili hana uhakika na anachokisema, basi Mwenyezi Mungu atamhukumu, kwa sababu haitakii mema Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa kweli tulikaa Wazanzibari sote kwa pamoja na kuomba dua siku ya Ijumaa na wala tusidhani kwamba lile jambo lilikuwa dogo. Jambo lile ni kubwa sana na tulimwelekea Mwenyezi Mungu na kumwambia Mwenyezi Mungu tusaidie, ili Zanzibar yetu isimame na kubaki na Mwenyezi Mungu alituambia *Inshaallah*, mimi kama Mwenyezi Mungu nitakusaidieni na Zanzibar itabaki kama Zanzibar.

Sasa sisi tuondoshe zile amekwaa kisiki au jiwe na wala haitusaidii chochote. Isipokuwa sisi tupo hapa kwa ajili ya Wazanzibari na tutaamua maamuzi yatakayowaridhisha Wazanzibari na wala si jambo jengine. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nawaomba waandishi wa habari kama alivyoomba Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu kwamba, mkituona au ndugu wanapogombana basi chukua jembe ukalime na wanapopatana kuchua kapu ukavune, ndipo utakapopata maslahi ya kuandika gazeti lako. Lakini sisi tukeshagombana hapa na kutofahamiana na kupigana kwa viti wewe utaandika nini?

Mhe. Spika, napenda kuwaambia hivi waandishi wa habari tusikilizeni tunalolisema na mliseme ambalo limesemwa na wala msiseme yasiyosemwa. Kwa maana hiyo, mfanyekazi kwa maslahi ya Wazanzibar, kwani sisi ni Wazanzibari tumeshakaa pamoja na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatujaalia tutakubaliana na kwenda kwenye msimamo mmoja, Mwenyezi Mungu atatufikisha salama na leo siku ya Ijumaa na wakati wa sala. *(Makofi)*

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe nakushukuru sana kwa kuweka nidham vizuri ya kutumia dakika saba. Sasa kulikuwa na viongozi wawili hapa na niliwaambia nyote haiwezekani, isipokuwa jichagueni mmoja aje aseme. Kwa hivyo, namkaribisha Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi pengine ndiyo ya mwisho kwa hoja hii ambayo imeletwa na Mhe. Abubakar Khamis Bakary. Hoja ambayo ni muhimu tena ni mzito yenye kutuhusu sote, kutokana na majadiliano yalivyokwenda hakuna aliyeikataa hoja hii, maana haikataliki.

Mhe. Spika, naiunga mkono hoja hii pamoja na marekebisho yake ambayo Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora, Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji pamoja na wengine walivyopendekeza. *(Makofi)*

Kwa kweli nilikuwa nimejitayarisha kuchambua chambua kidogo, lakini kwa muda mfupi uliobakia nitashindwa kufanya hivyo, isipokuwa nitayachambua yale ambayo nitakayoweza kuyachambua.

Mhe. Spika, kwanza hoja ya kufanya refrendum hii kama ilivyozungumzwa kwamba kuunga mkono, maridhiano au mazungumzo ya Rais wetu wa Zanzibar Mhe. Amani Abeid Karume pamoja na Maalim Seif Sharif Hamad tuyaunge mkono na tuyape baraka zetu.

Nitatoa siri kidogo kwa ajili ya kuthibitisha kwamba kutoka siku ya mwanzo mimi niliunga mkono, yaani ilipotoka taarifa hii kwenye vyombo vya habari, basi nilimpigia simu Maalim Jusa ndiye Maalim Seif na Maalim Seif ndiye Maalim Jusa. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa kweli ilithibitika hivyo, maana nilimpigia simu na kumwambia bwana nakupongeza sana, mwambie Maalim ninampongeza sana kwa hatua hii aliyoichukua ya kumtambua Rais wetu, baada ya kukaa kwa muda wa miaka sita na kumbughudhi na kila kitu, lakini sasa amemtambua rasmi.

Kwa hivyo, twende mbele na waliyoyazungumza hawakutwambia, lakini tutaambiwa bila ya shaka na kama lengo ni kuweka umoja, amani na utulivu tutafanikiwa.

Mhe. Spika, Maalim Jusa aliniambia ah! Maalim Seif huyu hapa zungumza naye, basi alimpa simu na tukazungumza. Kwa hivyo, wao wako hai na tunaweza kwenda kuwauliza na kuthibitisha. Baadaye tulikutana tena katika sherehe fulani sizikumbuki, aliniambia nakushukuru na ulionesha msimamo

katika suala la Zanzibar si nchi pamoja na lile la mafuta. Kwa hivyo, nadhani na hili kauli yako itakuwa ni sahihi na wala sina sababu ya kuikataa au kuwa na wasi wasi nayo. *(Makofi)*

Kuanzia hapo kila lipotokea zito ambalo linasababisha bugudha basi tunawasiliana. Sasa nimesema niseme hilo kwa sababu ni zito na siri zetu lakini nimelitoa.

Jambo jengine mimi nilibahatika kuwa Mjumbe wa Tume ya Muafaka ya Kwanza na Pili ya 1999 na 2001. Katika tume ya pili tulifanyakazi na Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Mhe. Omar Ramadhan Mapuri, Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto Mhe. Dk. Herison Mwakiembe, nadhani wanatosha. Kwa kweli kila wakati tulikuwa tukikaa pamoja kwa ajili ya kubadilishana mawazo na ndugu yangu ambaye ni rafiki yangu mpenzi Jusa alikuwemo.

Tulifika pahala na kusema tuandike waraka wa kuupeleka serikalini unaozungumza Serikali ya Umoja wa Kitaifa, yaani mashirikiano, basi kazi hiyo tulipewa mimi na Jusa, tuliifanya na kuiwasilisha kwenye kamati yetu. Mhe. Balozi Omar Ramadhan Mapuri kwenye mkutano wa kamati alisema Mhe. Ali Juma Shamuhuna sikutegemea kama utakubaliana na Maalim Jusa kuandika waraka huu mzuri.

Lakini kwa sababu Mhe. Haji Faki Shaali ameshaingia, basi nimtaje kama alivyonitaja kwa ajili ya kuthibitisha. Kwa sababua lilipokuja suala la utaifa, basi kama kuna watu ambao walijisifu wao ndio wataifa wakubwa na mimi nimo. Mhe. Haji Faki Shaali sikujua kwamba tunao uhusiano wa kidamu, lakini tunao uhusiano.

Kwa hivyo, aliniambia Mheshimiwa nyumbani kwako Donge Eneani wako wanawake wawili hawa mimi ni jamaa zangu, wapo mpaka leo nyumbani kwako, basi naomba uniazime gari kwa ajili ya kwenda kuwaangalia au kuwaamkia. Mhe. Spika, sikusita na kuanzia pale nikawa ninamkumbusha ile gari unaihitaji lini, siku ilipofika nilimkabidhi gari na kwenda kuonana nao na kurejea. Baada ya kurejea alinipa taarifa kwamba bwana nakushukuru sana.

Kutokana na hali ile, nilimwambia siku nyengine yoyote unapotaka kwenda kuwangalia niarifu. Kwa kweli ni kuthibitisha mambo haya yameanza zamani, udugu huu upo zamani na umoja huu upo zamani, isipokuwa ni tofauti za kisiasa za shetani mbaya aliyotuingilia kati na kutufarakanisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka nigusie kitu kimoja tu cha *referendum* kuweka sawa. kwa kweli nataka nitoe *quotation* moja ya bwana Korein ya 1988 naomba kunukuu kwa lugha ya Kiingezera Mhe. Spika.

Quotation ya Bwana Korein mwaka 1988 inayosema hivi:-

"*Referendum is the devices of direct democracy and anable voters to decide issues themselves*."

Mhe. Spika, *to underline the word direct democracy*. Tunapozungumza uwakilishi katika Baraza la Wawakilishi kwamba tutaamua kwa niaba ya wenzetu hii inakuwa uwakilishi na wala sio *direct democracy*. Kwa lugha nyengine hiyo itakuwa *indirect democracy*. Kwa hivyo, kama tunahimizama masuala ya *democracy* na mengine kwa nini tusiende kwenye *direct democracy* na kwa maana hiyo twende kwenye *referendum*. *(Makofi)*

Kwa sababu wapo wenzetu ambao wana wasi wasi na Mhe. Rais Kikwete siku moja alisema kwani nilimsikia na wala simsemei, yaani alisema na mimi nilikuwepo. Tatizo la Wazanzibari hawataki kufikia walikokusudia, maana hawa wameshakusudia na tayari wameshakubaliana kwa mujibu wa mazungumzo yao, lakini wanaogopana na wala hawaaminiani.

Mhe. Spika, nadhani tumefika pahala sasa kama hatukuogopana wakati tulipozungumza habari ya nchi au pale mafuta yetu na *Inshaallah* mafuta yatakuwa yetu. Kwa nini tuogopane sasa kwa sababu tunazungumza maslahi ya nchi yetu, hakuna sababu. *(Makofi)*

Kwa kweli Rais wangu nimemsikia si mara moja wala mbili na nikisema Rais wangu nakusudia Rais wa Zanzibar Mhe. Amani Abeid Karume, amefanya *reference* ya tuliyazungumza sasa ni kwamba yaliandikwa katika *Referendum* ya *Afro Shirazi Paryt*. Kwa hivyo, Mzee Abeid Amani Karume baada ya Mapinduzi alitekeleza maamuzi au *Referendum* ya *Afro Shirazi Party* ya kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa. *(Makofi)*

Sasa alichokifanya yeye na Maalim Seif Sharif Hamad si kipya isipokuwa kinatokana na huko. Mhe. Spika, kama historia inatufundisha basi nadhani sasa tunarudi kwenye historia na wala hakuna matatizo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nirudie kwenye *referendum* nani walifanya hiyo na iliwasaidia vipi. Kubadilika kwa *Episite* na kuingia katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilifanywa *Referendum* ya kubadilisha Katiba na baadaye katiba ilibadilishwa, wenzetu wanaingia na kuunda Serikali ya Umoja ya Kitaifa.

East Timor ilifanya *referendum* na Serikali ya Indonesia, ili East Timor itoke kwenye mamla ya Indonesia. Kwa hivyo, waliamua kwa makubaliano na kufikia kwenye maamuzi na hivi sasa East Timor ipo mbali na Indonesia pia iko mbali.

Lakini nchi maarufu kwa *referendum* kama vile Australia, Denmark, Ufaransa, Newsland na maarufu zaidi Switzerland. Kwa kweli hizi ni nchi ambazo katika masuala yao ya kurekebisha katiba wanazungumza *referendum* na wanakubaliana kwa pamoja na baadaye wanatengeneza yale waliyoyakusudia.

Kwa nini tuchukue muda hapa wa kupeana vionjo na kufundishana pamoja na kufanya mambo mengine, tayari tumeshakubaliana jamani. Pamoja na hayo, CCM ndiyo iliyokubali mwanzo na hili lazima tuliseme na libakie kwenye *record*.

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu amemleta Sheikh Mhe. Abubakar Khamis Bakary kutuambia kwamba anatuletea hoja kuhusu yale waliyokubaliana Maalim Seif na Rais Karume tuyajengee utaratibu pamoja na mustakbali mzuuri, ili tuelekee huko. *(Makofi)*

Kwa kweli sote tuliosema hapa na mimi ninamalizia nasema kwa niaba ya watu walionileta hapa kutoka Donge kwa ajili ya kuwasemea pamoja na kuwatetea naunga mkono hoja. Vile vile kwa niaba ya taifa langu katika kulenga mambo ya mustakbali wa nchi yetu naunga mkono hoja pamoja na marekebisho yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia namshukuru sana Mhe. Said Ali Mbarouk kwa mazungumzo yake aliyomuomba Mhe. Abubakar Khamis Bakary. Kwa kweli ninavyomfahamu Mhe. Abubakar Khamis Bakary ni mtu mstaarab ambaye ni msomi mwenye kupima hoja, basi naamini atamkubalia.

Isipokuwa nataka niongeze langu dogo kutokana na lile la Mhe. Said Ali Mbarouk, kama tutaona ni vigumu kumuachia Rais wetu achague Wakuu wa Mikoa na Wilaya, basi tumuachie Wakuu wa Wilaya awachague. Ikiwa shida ndiyo hiyo, basi Wakuu wa Mikoa wasiingie kwenye Baraza la Wawakilishi na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa mtanisamehe na wala sikutakieni mabaya na wala msende mitaani na kunimaliza. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa kweli hiyo ni *alternative* ya pili na ile ya kwanza ni kwamba Rais apewe madaraka, kwa sababu yeye si mtendaji, apewe madaraka ya kuchagua Wakuu wa Mikoa na Wilaya, ili wamsaidie katika kutawala nchi yake katika level hiyo ya Mkoa na Wilaya.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Kwa hivyo, natamka tena hoja naikubali pamoja na marekebisho yake yaliyotolewa na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora na Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana kwa kunisaidia katika kuendesha kikao hiki. Kwa kweli Waheshimiwa Wajumbe wengi waliomba kuchangia lakini nilishindwa kwa sababu ya muda ulivyotukwazwa.

Isipokuwa nimejaribu na kujitahidi, ili kuona tunapata wachangiaji wengi kiasi, lakini wote haikuwezekana. Sasa wale ambao waliomba lakini nilishindwa kuwapa nafasi kutokana na muda, basi niwataje kwa ajili ya kuwaomba radhi na wanikubalie kwa kuomba radhi huko. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, kati ya waliokosa kuchangia ni pamoja na Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin, Mhe. Hamad Masoud Hamad, Mhe. Mkuu wa Mkoa Mjini Magharib, Mhe. Ali Denge Makame, Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Asha Moh'd Hilali.

Wengine ni Mhe. Ali Moh'd Bakari, Mhe. Haji Omar Kheir, Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Mhe. Fatma Abdalla Tamim, Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezi, Mhe. Waziri Kiongozi. *(Makofi)*

Kwa kweli nawaomba radhi sana, kwa sababu muda ulikuwa umetukwaza mno, nimejitahidi sana kuona kwamba wachangiaji wengi wamepata kuchangia hoja hii muhimu.

Waheshimiwa Wajumbe tunakwenda kupumzika pamoja na kusali sala ya Ijumaa na dua nyingi nyengine za kulimaliza jambo hili salama. Kwa sababu kuna mambo ambayo tumekubaliana na sote tumesikia hapa, pia kuna mengine ambayo tumefanya marekebisho humu humu na tutamsubiri Mhe. Abubakar Khamis Bakary mwenyewe.

Lakini jambo la muhimu ambalo nataka kulisema ni kwamba mwisho wa habari hii wananchi wanatusubiri tunawapelekea nini. Kwa sababu kile tutakachowapelekea ndicho kitakachoendesha mazungumzo ya kule, hivyo hatuwezi kupeleka vitu huko na kule watababaika. Waheshimiwa Wajumbe, kazi moja ya kiongozi ni kumuongoza mwananchi, ili aelekee pahala ambapo patakuwa salama kwa manufaa yake pamoja na taifa kwa jumla. *(Makofi)*

Hivyo, tutakaporudi kusali sala ya Ijumaa na wengine kupumzika kwa wale wasiokwenda huko, basi tutafakari hilo kwamba tunakuja kumaliza shughuli ambayo wananchi waliotuleta humu wanatusubiri, kwa ajili ya kuwaelekeza nini sisi wawakilishi wao na jambo gani wafanye kwa manufaa yao pamoja na nchi hii kwa jumla.

Waheshimiwa Wajumbe, nakuombeni sana tukatafakari kwa makini sana, ili tuje tuamue kitu ambacho kitakuwa madhubuti tena kizuri.

Kwa hivyo, jioni moja kwa moja tutakwenda kwa mtoa hoja, ili kufanya majumuisho baada ya hapo na kupitisha jambo hili kwa kadri ya hali itakavyokuwa. Hivyo, tutafanya Uchaguzi wa Mwenyekiti kwa mujibu wa marekebisho yetu ya Kanuni na patakuwa na muda mdogo wa mapumziko kwa ajili ya kungojea matokeo ya uchaguzi na baadaye kumuomba Mhe. Waziri Kiongozi atoe hotuba ya kumaliza shughuli zetu za mkutano huu.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo machache naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Tulikuabaliana mapema kwamba mjadala uwe tumeusitisha pale kipindi cha asubuhi na jioni hii twende moja kwa moja kumsikiliza mtoa hoja. Kwa hivyo, sasa naomba kumkaribisha Mhe. Abubakar Khamis Bakary kufanya majumuisho.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, napena kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kufika hapa jioni hii ili kujumuisha majadiliano yote ambayo tuliyafanya kuanzia jana.

Mhe. Spika, shukurani nyengine napenda sana nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa uendeshaji wako wa kikao hiki na zaidi katika kuliendesha Baraza katika wakati huu ambao tulikuwa tunajadili hoja hii ambayo ni muhimu kwa taifa letu.

Mhe. Spika, uendeshaji wako mzuri naamini kwamba huo na wewe utakuwa ni mchango wako hata kama hukuchangia moja kwa moja.

Lakini shukurani za pekee naomba ziende kwa Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete ambaye yeye ni kama Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na ni Rais wa Jamhuri ya Muungano. Alisema wazi wazi kuanzia Disemba, 2005 kwamba tatizo hili la mpasuko huu Zanzibar linamkera na kwa vyovyote vile, angelipenda suala hili likamalizika. Naamini kwa ushirikiano wetu na kwa kupata baraka zake tatizo hili Inshaallah kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu litamalizika.

Mhe. Spika, sasa napenda niwashukuru Wajumbe wote waliochangia, kwa kweli ni wajumbe wengi sana na bahati mbaya wengine hawakupata kutokana na muda, lakini wajumbe ambao wamechangia ni wajumbe 27. Hawa walichangia kwa kuzungumza, lakini wajumbe wawili Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na Mhe. Hamad Masoud Hamad wao walichangia kwa maandishi. Naomba sasa nichukue nafasi hii kuwataja wale wote waliochangia hoja hii.

1. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora
2. Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji
3. Mhe. Abass Juma Muhunzi
4. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
5. Mhe. Asaa Othman Hamad
6. Mhe. Haji Mkema Haji
7. Mhe. Omar Ali Shehe
8. Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii
9. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji
10. Mhe. Ali Suleiman Ali
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman
12. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba
13. Mhe. Zakiya Omar Juma
14. Mhe. Thuwaybah E. Kissasi
15. Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi
16. Mhe. Ahmed Nassor Mazrui
17. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
18. Mhe. Zahra Ali Hamadi
19. Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu
20. Mhe. Haji Faki Shaali
21. Mhe. Ali Mzee Ali
22. Mhe. Juma Duni Haji
23. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi
24. Mhe. Said Ali Mbarouk
25. Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto
26. Mhe. Aziza Nabahan Suleiman

27. Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo

Hawa ndio waliochangia kwa kuzungumza na Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na Mhe. Hamad Masoud na wao walichangia kwa maandishi.

Mhe. Spika, kazi yangu itakuwa ndogo sana kwa sababu wajumbe wote hao napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru tena sana sana, michango yao yote ilikuwa ni ya kujenga na atakriban wote tulikubaliana kwa ile hoja, ingawa wengine kama ulivyo utaratibu walisema kwamba aa, hoja hii ibadilishwe au irekebishwe kwa misingi hii. Huo ni utaratibu mzuri na mimi naukubali. Kwa sababu hoja ambayo mtoa hoja amezungumza haji-*claim* kwamba yeye ndiye *perfect* kuwa kila alichokitoa hoja ndio hicho hicho, bila shaka mawazo ya wengi lazima yazingatiwe na yashughulikiwe.

Kwa hivyo, kuna mambo matatu, ambayo kwanza tumekubaliana na zile hoja ambazo tumezizungumza, lakini pia katika hoja hizo kuna baadhi ya marekebisho ambayo yalipendekezwa kwa lengo la kujenga zaidi. Zaidi suala moja muhimu lililozungumzwa hapa ni kwamba walisisitiza umuhimu wa umoja na mshikamano wa kuwa na kitu kimoja ambacho sote kwa lengo moja tunaweza tukajenga nchi hii. Kwa hivyo, hayo nafikiri ndio mambo matatu ambayo ni muhimu kuyazungumza.

Mhe. Spika, mimi sitokwenda katika kumjadili kila mtu, kwa sababu wote kama nilivyosema wamelenga katika suala lile lile ambalo tulilizungumza. Nitalizungumza kwa ujumla na pale ambapo itataka ufafanuzi basi nitatoa ufafanuzi ili kuweka mambo zaidi.

Katika ufafanuzi huu, kwanza nizungumzie suala la amani, umoja na uzalendo ambapo mambo haya matatu ndio msingi mkuu wa Uzanzibari wetu, ndio msingi mkuu wa kuweza kuendeleza nchi yetu. Sasa katika kufanya hivi naomba nimnukuu aliyekuwa Rais wa Marekani Bw. Abraham Linkon, wakati huo alisema, naomba nimnukuu kwa Kiswahili ingawa yeye alisema kwa Kiingereza. Alisema, “nyumba iliyogawika ndani yake haiwezi kusimama, naamini serikali hii haiwezi kuishi na kudumu huku ikiwa ni nusu huru na nusu ni utumwa”. Hayo ndio maelezo ya aliyekuwa Rais wa Marekani katika mwaka wa 1858.

Sasa dhana hii ya aliyekuwa Rais wa Marekani ndio hasa dhana inayohusiana na uzalendo kwamba ikiwa tumegawanyika nyumba moja kwa hivyo nyumba ile haiwezi ikasimama. Ni falsafa kubwa sana hiyo, na hapo ndipo inapochimbuka dhana ya uzalendo.

Uzalendo huu kama tunavyojua hili neno la Kilatini na maana yake hasa ni Peta, peta maana yake ni baba na baba kwa Kilatini sio baba mzazi lakini ni nchi. Kwa hivyo wao wakasema Walatini hao, kwamba lazima mtu awe *patriotic*, yaani awe ni mzalendo kwa nchi yake aipende nchi yake. Kwa hivyo, kwanza inakuja nchi na halafu ndio anakuja yeye. *(Makofi)*

Lakini masomo haya pia yako hata katika dini Mtume wetu Nabii Ibrahim wakati alipokuwa akiiombea nchi yake. Kwanza alimuomba Mwenyezi Mungu wake kwamba anaomba amani katika nchi na baadaye kumuomba Mwenyezi Mungu nchi ile airuzuku baraka na vipando. Kwa maana hiyo, suala muhimu hapa ni jambo la amani kwanza, baada ya amani ndio inakuja suala la kuruzuku matunda na mambo kama hayo.

Kwa hivyo, pale aliposema Nabii Ibrahim kwamba Mwenyezi Mungu ijaalie nchi ya Makka iwe nchi ya amani na ijae matunda. Kwa kweli somo kubwa tunalolipata na Mtu Ibrahim (AS) kwamba, lazima kwanza kuwe na amani na baadaye ndipo ipatikane baraka ya matunda, bila ya shaka ni mazao, kwani kuwa na mazao ndio maendeleo katika nchi.

Kutokana na hali hiyo, maendeleo hayawezi kuja katika nchi bila ya kuwa na amani. Mhe. Spika, nadhani hilo ni fundisho kubwa ambalo tumepata hata kwa viongozi wetu wa kidini.

Isitoshe tukiangalia na nimejaribu kufanya utafiti katika vitabu vya Kikiristo Wafilipi aya ya 4 mstari wa sita na wasaba na tukiangalia Yohana mstari wa 14, kwa kweli zote zimeelezea umuhimu wa kutunza amani, ili baraka iweze kushuka kutoka kwa Bwana Mungu. Kwa hiyo, hayo yote ni mambo ambayo yanatuonesha kuwa, amani ni jambo muhimu sana na baada ya kupata hiyo amani ndio tunaweza kufanya mambo mengine.

Mhe. Spika, tunaweza kusema utulivu tukiweza kuutekeleza utulivu basi utazaa amani na amani italeta maendeleo. Kwa hivyo, sote tunawajibika katika suala hilo, pia sote tunatarajia kwamba tutakuwa na msimamo huo, ili nchi yetu kwanza iwe na amani na baadaye maendeleo yaweze kupatikana.

Kwanza nilisema niseme hayo, ili kwa kujua kwamba sisi tunao wajibu kwa pamoja kuwa na *patriotic* ya nchi yetu kwa ajili ya kuleta maendeleo katika nchi yetu. Mhe. Spika, hapa niliguswa kidogo na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji alipotoa mfano wa nchi ya Singapore. Kwa bahati nzuri niliwahi kwenda kiasi ya miaka miwili au mitatu nyuma, kweli Singapore ni nchi au mji nchi, yaani wanaita *City State*, lakini maendeleo yao yamekuwa makubwa sana, kwa sababu gani.

Wakati tulipotembelea Bunge lao walisema kwamba sisi tunavyo vyama vinne ndani ya Bunge, lakini sote kwa pamoja tumeshirikiana kwa ajili ya suala la nchi kwanza, halafu ndio suala la vyama na hapo ndio maendeleo yanaweza kuja. Mhe. Spika, leo kama alivyosema Mhe. Fatma kwamba Singapore ni nchi ya tano kwa utajiri duniani, kwa kweli ni kitu cha kupigiwa mfano. Sasa je sisi Zanzibar kweli tutashindwa kama tukishirikiana kwa pamoja na kuwa kitu kimoja katika kujenga nchi yetu. Sidhani kama tutashindwa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, sasa niende kwenye hoja ambazo tumezitoa. Hoja iliyokuja na wenzetu sana Upande wa CCM walisema kwamba hoja hii ni yetu, ambayo inatoka Butiyama na mambo kama hayo. Kwa kweli mimi sipingi hata kidogo, lakini nadhani tusiende huko sana, kwa sababu hii chimbuko lake sote tunajua ni Bagamoyo, pale tulikuwepo vyama viwili.

Kwa hivyo, hoja hii hasa ni kutoka Bagamoyo, yaani ni hoja ya CUF na CCM. Lakini mimi siko huko hata kama hoja italetwa na CUF au CCM au vyama vyengine, wakati ni hoja ya kujenga nchi, ambayo inataka kutela umoja kwa ajili ya manufaa ya Wazanzibari, basi nitaikubali na kuiunga mkono. Kwa maana hiyo, hoja hii ni yetu sote, nafikiri tukisema yetu sote ndio tunakuja kwenye lile suala la patriotism kwamba nchi ni mwanzo na halafu sisi tunakuja namba mbili.

Mhe. Spika, tukiangalia kwenye hoja hii ya Bagamoyo au baadaye ilipofika Butiyama ilizungumza kwa kirefu suala la Serikali Shirikishi kama alivyosema Mhe. Mjumbe mmoja kule, ikatoa utaratibu wake kuwa Rais atakuwa vipi, Makamo wa Kwanza wa Rais atakuwa vipi, yaani nguvu zake zitakuwa vipi, Makamo wa Pili atakuwa vipi pamoja na nguvu zake, kutakuwa na mambo gani mengine. Kwa hivyo, yote hayo ni mambo ambayo yalikubaliwa na yalipelekwa Butiyama na kukubalika.

Kutokana na hali hiyo nashukuru kwamba hoja hii ambayo tunaizungumza hapa ni hoja ya pamoja, yaani wenzetu Butiyama waliikubali na wala mimi hainipi shida, kwa sababu lengo langu ni suala la kujenga nchi, umoja pamoja na kuangalia kuwa Zanzibar yetu iko nyuma na tushirikiane, ili tuweze kwenda mbele.

Mhe. Spika, kwa mantiki hiyo, mimi nilileta hoja katika Baraza na hoja hii ilikuwa na vifungu tisa. Nashukuru Wajumbe wote walizungumza vifungu hivyo na wengine walivikubali na wengine kufanya marekebisho na wengine kusema hivi tufanye marekebisho haya na yale na huo ndio uzalendo unaotakiwa. Kwa sababu wote wamefanya hivi kwa ajili ya kujenga. Kwa hivyo, wale wote waliofanya hayo nawashukuru na pia nawapongeza sana kwa kunisaidia hii kazi, ambayo mwanzo niliianzisha peke yangu. *(Makofi)*

Sasa kutokana na hoja hii nimefikiria kwamba wako wenzetu wengine ambao wameseme tubadilishe kwa faida ya kujenga na wengine walisema vifungu hivi tuvirekebishe. Mhe. Spika, hapo nilikwenda tena kule wakati tulipokuwa vyuoni na madarakasani, nakumbuka walimu wetu Mtume wetu Muhammad (*S.A.W*) alituonesha mifano ya kujenga kwa nini na sisi hatufuati huko, tukifuata huko ndio tutakuwa waungwana, kwa namna gani.

Kwa mfano, tuangalie mikataba mingi lakini Mkataba maarufu wa Hudaibiya alipoambiwa Mtume Muhammad (*S.A.W*) alipoambiwa asiandike *Bismillah Rahman Rahim*, alisema sawa na ikaandikwa Bismika Allahhuma, lakini kwa ajili ya kujenga baadaye mafanikio tukayaona. Vile vile aliambiwa usijiite Muhammad Rasuluallah, lakini ujiite Muhammad mtoto wa Abdillah kwa ajili ya kujenga.

Sasa mafunzo hayo Mhe. Spika, ni mafunzo ambayo na sisi lazima tuyachukue na tuyatekeleze, ikiwa suala limeletwa kwa sababu ya kujenga mimi sioni haja au sababu kwa nini tusilikubali, hata kodogo, lazima tulikubali kwa vile ni suala la kujenga. Kwa mantiki hiyo Mhe. Spika, naomba niseme yafuatayo:-

Hoja hii iliyotolewa ambayo ina vifungu tisa, cha kwanza kilikuwa kinazungumza kwamba ni kulitaka Baraza hili tukufu lifanye marekebisho ya vifungu vya 9, 39, 42 na 61 vya Katiba ya Zanzibar.

Kifungu cha 9(3) wengi wakasema ni kizuri lakini ile (a), (b), (c), (d), (e) zile ziondolewe kwa sababu zimepitwa na wakati, zina mambo haya na haya. Mimi sioni sababu kwa nini nikatae. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nakubali kwamba kifungu kile kiondolewe kwa mantiki hiyo kwa sababu kufanya hivyo ni kujenga.

La pili nitamke kwamba muundo wa serikali Zanzibar uwe ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa utakaohusisha vyama vyote vya siasa vilivyomo katika Baraza la Wawakilishi na kwamba viongozi wakuu wa serikali watokane na uwiano wa kura za Rais katika uchaguzi mkuu.

Hili pia lilikuwa na marekebisho, Waheshimiwa Wajumbe wengine wakasema kwamba kwa suala la Rais basi kura za Rais zitumike, lakini kwa suala la Mawaziri basi suala la viti litumike. Sasa hapa ningeliomba kitu kimoja, nakubali kwamba kwa suala la Rais kura za Rais zitumike, lakini kwa suala la mawaziri mimi ningeliomba sana wajumbe wakatizama ule uwezekano. Kwa sababu wawakilishi watakaoingia katika Baraza tunaamini pengine watakuwa ni vyama zaidi ya viwili wakati huo, sasa ikiwa zaidi ya viwili pale *issue* itakuwa ni suala la kura zilizowaingiza mule.

Sina *objection* sana ya viti lakini nilikuwa nahisi katika uteuzi wa mawaziri ile idadi ya kura za wawakilishi ambazo zimo ndani ya Baraza kwa idadi ya wale wawakilishi basi zile zi-*determine* ile *percentage* ili kuwapa nafasi vyama vyengine kama vitakuwepo au kama vitapata nafasi. Lakini vyenginevyo *I am very happy* kwa wazo hili ambalo lilitolewa na wenzetu. Lakini nilikuwa napenda litizamwe kwa misingi hiyo.

Mhe. Spika, katika pendekezo la tatu ni kwamba litamke kuwa Serikali hiyo ya Umoja wa Kitaifa itakayoundwa itaendelea kuheshimu na kuthamini misingi mikuu ya Mapinduzi ya tarehe 12 Januari, kama ilivyotangazwa na Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume hapo tarehe 8 Machi, 1964. Mimi nafikiri hili sote tulikubaliana na tulisema kwamba vile vifungu vya (a), (b), (c), (d) na (e) tuviondoe na tumekubali kuviondoa.

Pendekezo la nne tulisema kwamba Baraza liweke utaratibu utakaowezesha wananchi wa Zanzibar kushiriki kwa njia ya moja kwa moja kutoa ridhaa yao kuunga mkono mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa njia ya kura ya maoni (*referendum*) na kwamba kura hiyo iwe imeandaliwa na kufanyika si zaidi ya mwezi wa Mei, 2010 au liweke utaratibu mwengine kwa njia ambayo Wazanzibari wenyewe kwa kupitia wawakilishi wao waliowachagua wataona inafaa.

Tumeona maoni ya wengi kwamba tufanye *referendum* na *referendum* hiyo tuhakikishe kwamba inafanywa kabla ya uchaguzi mkuu. Sioni kwamba kuna tatizo na nakubali pendekezo hilo.

Tano ni kwamba Baraza liagize serikali ndani ya siku saba kuandaa na kufikisha mbele ya Baraza hili tukufu Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar Nam. 11 ya mwaka 1984 kwa madhumuni ya kuweka utaratibu, masharti na namna ya uendeshaji wa kura ya maoni na pia kuipa mamlaka Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar mbali ya majukumu yake iliyonayo sasa. Pia kusimamia na kuendesha kura ya maoni kwa yale masuala mazito yanayohitaji maamuzi ya wananchi.

Hapa suala kubwa lilikuwa kwa nini tuiagize serikali na kuipa muda. Hapa tulisema ndani ya siku saba, tusiifunge serikali namna kama hiyo. Mimi nakubali kwamba tusiifunge serikali. Tuseme tu, Baraza liagize serikali katika tarehe ya mapema kama serikali itakavyoona inafaa. Sasa hiyo nakubali tufanye hivyo.

Mhe. Spika, katika kifungu cha sita tulisema kwamba Baraza liagize serikali kufanya mawasiliano na nchi rafiki, washirika wa maendeleo na jumuiya ya za

kimataifa kwa lengo la kuona uwezekano wa kusaidiwa gharama za uendeshaji wa kura hiyo ya maoni ili kupata ridhaa ya wananchi katika suala hilo.

Mhe. Spika, nalo hili ni suala ambalo lilijadiliwa kwa kirefu na wenzetu wakasema kwa nini tuwaambie kwamba tuiagize serikali na hizi ni kazi zao. Ndio kazi za serikali kutafuta misaada, sasa kitu kimeshakuwa wazi kama hivyo kwa nini kufanya ukaidi. Kwa hivyo, nakubali kwamba suala hili nalo liondoke. Serikali itafanya mawasiliano yake yenyewe kwa utaratibu wake naamini ni kwa njia ambayo wataona inafaa kwa maslahi ya taifa na kwa maslahi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, katika kifungu cha saba tulisema kwamba pale itakaporidhia hoja hii basi livitake vyama vyote vya siasa vyenye wajumbe katika Baraza hili tukufu kujikubalisha kuunga mkono hoja itakayopelekwa kwa wananchi ya kuwaomba kuidhinisha uanzishwa wa mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Hapa napo palikuwa na maelezo kidogo. Hoja kama nilivyosema, hoja hii ukitizama *origination* yake ni Bagamoyo; ni vyama viwili vya CUF na CCM. Kwa hivyo, ikiwa hapa katika Baraza hili ni vyama hivyo hivyo viwili lakini tufikirie pengine labda kutakuwa na vyama vyengine ambavyo navyo vitawajibika kufanya haya yatakayofanywa na serikali. Sasa mimi sina tabu sana ya kusema kwamba Baraza livishauri vyama vyote vya siasa vyenye wajumbe katika Baraza hili na vile vyama ambavyo havimo katika Baraza kulisimamia suala hili. Kwa sababu sote ni wananchi, ni Wazanzibari na tunajenga kwa faida ya Zanzibar. Kwa hivyo, hiyo itakuwa ni *inclusive* ya vyama vyote.

Lakini wale waanzilishi CCM na CUF lazima wachukue wanasema *key position*, *leading role* ya kuhakikisha kwamba masuala haya yanakwenda vizuri. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi sioni kwamba hilo ni tatizo na kusema kwamba tusiwalazimishe serikali au lisivitake vyama kwa njia ya kulazimisha. Lakini tuvishauri, ni suala la kushauriana na vyama katika kufanikisha hayo. Mimi nafikiri hii itakuwa ni njia ya ushauri zaidi kuliko kusema lilazimishe hiyo itakuwa tumekwenda mbali kidogo kama walivyosema wengine na suala hili kama tunavyojua ni suala la maridhiano. Kwa hivyo, huwezi kumlazimisha mtu *at that stage*, lazima tushauriane ili tukubaliane. Sasa tushauriane kuwa livishauri vyama vyote vinavyohusika.

Kifungu cha nane Mhe. Spika, hiki kulikuwa na mambo mawili, kinasema kwamba chini ya kanuni ya 48(6) na 78(3) ya Baraza lijadili rasimu ya Mswada wa Marekebisho ya Katiba ya Zanzibar kwa vifungu vinavyohusika ambavyo kwao vimeambatanishwa na hoja hii na ambavyo ni sehemu ya hoja yenyewe ili baadae kupelekwa serikalini kama ni Mswada wa Serikali.

Sasa hapa Mhe. Ali Mzee Ali *profesor* wangu alisema kwamba mbona najikanganya kwa sababu nimesema mambo mawili kwa pamoja hapa. Kwanza ni kuandaa ule mswada ambao nimeupeleka mimi katika Baraza, lakini halafu tuupeleke serikalini. Kwa hivyo, akauliza *which is which*? Kiutaratibu na kikanuni za *Constitutional Law* hapa nilifanya hivi na sikusema kwamba baadae huu mswada uletwe na mjumbe binafsi, kwa sababu *constitutional law* utaratibu wake kitu kama hiki lazima kipitie serikalini na ndio maana nikasema kwamba baadae iende serikalini.

Sasa ili kuondoa hii mimi nilikuwa napendekeza hivi, Baraza liagize serikali kuandaa na kuwasilisha mbele ya Baraza hili tukufu Mswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya marekebisho ya Zanzibar kwa vifungu vinavyohusika kwa lengo la kuingiza mfumo huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa kuzingatia yale mapendekezo yetu yaliyomo katika rasimu ya makubaliano ya CCM na CUF yaliyofikiwa katika mazungumzo yao, na kwamba serikali baadae kwa kutumia utaratibu uliowekwa kikatiba na kwa mujibu wa Kanuni za Baraza iwasilishe mswada huo katika Baraza lako tukufu chini ya Kanuni za Baraza.

Kwa hivyo, itakuwa hii tumesha-*shift* ile *burden* kutoka kwa mjumbe yeyote kwenda kwa serikali. Sasa serikali wakati ambapo itaona inafaa wakati muafaka pale italeta mswada ule na inategemea sasa kwa mujibu wa Kanuni za Baraza ama italeta *under certificate of urgency* ikiwa wanataka hivyo, au wataleta kwa njia za kawaida kulingana na lini au kipindi gani ambapo mswada ule utaletwa. Kwa hivyo, hilo ni jukumu ambalo tunaliachia serikali moja kwa moja.

Mhe. Spika, suala la mwisho ni suala la kamati. Tulisema kwamba Baraza liunde kamati ya wajumbe sita, watatu kutoka upande wa serikali na watatu kutoka upande wa upinzani kwa madhumuni ya kusimamia hatua zote zinazopendekezwa na hoja hii hadi kukamilika kwake.

Mhe. Spika, kifungu hiki kilikuwa na mawazo tofauti, kulikuwa na mawazo ya wale ambao walihisi kuwa kamati hii pengine isingelikuwepo, lakini kulikuwa na mawazo ambapo wengine walikuwa wanasema ni nzuri. Mimi *personally* na hili naomba niwaombe wajumbe wenzangu wote kwamba *argument* yangu hii ninayoitoa ni kuonesha tu kwamba ule umuhimu wa kuwepo kamati hii tusiutizame kwa uhafifu. Kwa sababu nimechukua historia na hapa napenda nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kanisaidia hii kazi kidogo kwa njia moja.

Kwa sababu tulianza na *IPC*. *IPC* ilikuwa na wajumbe kutoka vyama viwili sawa sawa, tukaja na *JPAC* tulikuwa na wajumbe kutoka vyama sawa sawa, tulikuwa na muafaka I wa wajumbe kutoka vyama sawa sawa, muafaka II

hivyo hivyo, Bagamoyo hivyo hivyo, Kamati ya Makatibu Wakuu hivyo hivyo. Lakini wakati wote kamati hizi mjue kwamba zilikuwa si kamati ambazo zinatekeleza hasa, lakini zilikuwa ni kamati za ushauri kusaidia yale mambo ambayo tunataka yaende, na ndio maana baadhi ya wajumbe wakasema kulikuwa na sheria tulizozipeleka hata ile sheria ya uanzishwaji wa DPP, marekebisho mengine ya katiba kutokana na kamati hizi. Sasa zikifanya pamoja halafu zikapeleka *final* hapa *authority* atakuwa ni serikali si hii kamati.

Baraza la Wawakilishi hapa tuna kamati nyingi ambazo zinafanya hayo baadae tunapeleka *as* ushauri halafu baadae serikali ndio inaamua. Kwa hivyo, mimi mawazo yangu binafsi sioni kwamba kuwepo kwa kamati hii kuna matatizo, ninavyohisi mimi kuwepo kwa kamati hii ni kwamba kutasaidia haya yote tuliyokubaliana hapa kusukumwa haraka haraka. Kwa sababu serikali kwa vyovyote tujue kwamba ina shughuli nyingi na kama hakuna kitu angalau cha kushtua shitua kidogo wanaweza wakasahau wakaona kwamba hiki tukifanye mwanzo, hiki mwisho, hiki baadae. Sasa angalau kukiwa na hiyo kamati mimi naamini kwamba itasaidia sana katika kusukuma mbele haya ambayo tutakubaliana. Kamati hii haitokuwa ndio *final*, hii itakuwa ni kamati ya ushauri kama kamati nyengine kama mifano niliyoitoa kwa kamati ambazo tulikuwa nazo hapo mwanzo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa kifungu hiki vifungu vingi hapa kwa nia ya kujenga nimekubali tuvifanyie marekebisho na hiki kwa nia ya kujenga na-*appeal* sana kwa Waheshimiwa Wajumbe kwamba nacho hiki tukione kwa misingi hiyo ili tuweze kuyashughulikia haya mambo yetu tunayoyakubali hapa ili kusukuma mbele na kuishauri serikali katika masuala hayo.

Mhe. Spika, haya ndio majumuisho yangu ambayo nilisema niyatoe mbele ya Baraza lako tukufu. Lakini kabla sijamaliza naomba niseme mambo mawili ambayo yamezungumzwa.

Kwanza ni suala la Wakuu wa Mikoa, ambalo nalo lilikuwa linazungumzwa sana. Kulikuwa kuna wengine wanasema Wakuu wa Mikoa wateuliwe na rais au wawemo katika marekebisho haya, wengine wakasema Wakuu wa Mikoa na Wilaya, wengine wakasema Wakuu wa Wilaya wasiwemo. Pia ikatoka *suggestion* nyengine kwamba Wakuu wa Mikoa hata wakiteuliwa wawe ni *civil servant*, ambayo hii inaonekana kwamba ilichukua watu wengi, walipenda *version* hii na mimi naikubali.

Lakini ninachopenda kusema ni kwamba hata kama tunaikubali hapa *of course* marekebisho haya yatakuja wakati serikali hapo tukishakubaliana kwamba tunapeleka kwa serikali yale marekebisho tuliyokubali. Kwa hivyo, serikali

itakapoleta mswada wake na hilo tutaiomba izingatie serikali kwa misingi hiyo. Kwa hivyo, mimi *personal* nakubali na sina matatizo nalo.

La mwisho katika suala hili ni lile ambalo Mhe. Hamad Masoud alinileta kwa maandishi, nahisi niliseme kwa sababu ni muhimu nalo. Alisema katika suala la marais, tunasema kwamba makamo wa rais atatokana na chama ambacho kimepata mshindi wa pili, makamo wa rais wa kwanza. Sasa kaniandikia hapa Mhe. Hamad Masoud anasema katika kanuni zetu ambazo nakubaliana naye kuna suala la pingamizi. Sasa tujaalie mimi na Mhe. Haji Omar Kheir tumegombea urais lakini mimi nikamuwekea pingamizi Mhe. Haji Omar kwa hivyo, itakuwa rais ni mmoja tu, sasa huyu makamo wa rais atapatikana vipi? Mimi nafikiri kuna *logic.*

Kwa sababu pale itakuwa hakuna tena kura za makamo wa rais kwa sababu kuna pingamizi kwa hivyo mgombea ni mmoja tu. Sasa mimi nilikuwa nafikiria kama litatokea hilo basi zile kura na ndio hapa nikasema kura katika wawakilishi tusichukue viti zile kura zilizomo katika wawakilishi zile ndizo zita-*determine* makamo wa kwanza wa rais. Katika misingi hiyo ya kwamba mgombea urais ni mmoja tu.

Waheshimiwa Wajumbe: Rudia hatujafahamu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa rudia.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Hamad Masoud alinileta maoni yake kwa maandishi, akasema anakubaliana na mawazo yaliyotolewa, lakini tuchukulie kwamba katika katiba na kanuni wagombea wa urais mwanzo nilisema wawili lakini niseme watatu, kuna a, b na c. Sasa katika siku ya pingamizi a akamuwekea pingamizi b na c na zile pingamizi zote zikakubalika, *at means* sasa mgombea wa urais atakuwa ni mmoja tu, itakuwa hakuna wagombewa wengine wa urais. Kwa maana hiyo hatutopata kura za rais nambari mbili, sasa huyu makamo wa rais wa kwanza tutampata vipi? Ndio swali lake. Mimi nikaona hili suala ni muhimu ambalo nalo itabidi lazima liwekwe katika marekebisho hayo ya katiba, kwamba ikitokea hivyo na kwamba watu wamewekeana pingamizi na akatokea mgombea urais mmoja tu sasa yule makamo wa rais atapatikana kwa wazo langu, atapatikana kwa kura za wawakilishi waliomo katika Baraza wa kile chumba ambacho kitakuwa ni nambari mbili.

Kwa mfano, rais (a) chama chake kiko ndani ya Baraza vile vile basi zile kura zake zitakuwa hazina maana tena kwa sababu yeye keshakuwa ni rais huku, lakini yule mgombea wa rais (b) na (c) vile vyama vyao vimo ndani ya Baraza kwa hivyo, zile kura za wawakilishi wao waliyomo ndani ya Baraza ndio zita-

determine chama gani kitoe makamo wa rais wa kwanza. Hivyo ndivyo nilivyofikiria na hayo yatawekwa katika utaratibu wa sheria.

Mhe. Spika, haya ndio maoni ambayo nilisema niyatoe kwa wenzangu na kwamba mimi moja kwa moja nakubaliana na mawazo ambayo wameyatoa na mapendekezo ambayo wameyatoa. Hii nasema kwa moyo safi kwa sababu lengo letu ni kujenga hii nchi yetu.

Sasa kwa kumalizia Mhe. Spika, mimi nasema hapa wawakilishi tunajenga historia yetu, na historia yetu itajulikana hapo baadae na vijukuu vyetu na watoto wetu. Naomba nimalizie kwa kusema mambo mawili.

La kwanza, Siti binti Sadi alisema katika enzi zake kwamba, "Uzuri wa mtu na ubaya wa mtu, na amali za mtu, na umuhimu wake, haujulikani mpaka pale kiwiliwili cha mtu yule kimeshachanganyika na mavumbi". Yaani mtu yule akishakufa ndio wenzetu watakuja kusema bwana fulani *Alhamdulillah* alikuwa hivi, ndiye aliyefanya hivi, Baraza ndilo lililomfanya hivi, baada ya hapo sisi tumeshakufa vizazi vyetu ndivyo vitakavyotupima sisi.

Lakini na msafiri maarufu sana kwa kale, Ibni Batuta wengi tunamjua. Ibni Batuta alitembelea mwambao wa Afrika huu na hapa Zanzibar alifika, alisema maneno haya katika karne ya 21, akasema kwamba, "Tutakapokufa msitutafute katika makaburi yetu, bali tutafuteni katika nyoyo na kumbukumbu za watu wetu kwa yale tuliyowatendea". Yaani tukishakufa sisi msiende mkatafuta kaburi langu lipo pahala gani, aa, lakini mtanipata katika vijukuu na watoto wetu mkiwauliza Abubakar, Hamza, Ramadhan Abdala Shaaban walifanya nini kwa taifa hili? Wale watoto ndio watajibu.

Sasa mimi naomba tuweke *history* kwa misingi hiyo, ni watoto wetu watakaojibu na ni watoto wetu ambao ama watatuombea au watatulani kwa mambo tutakayofanya. Mimi naomba mambo haya tuyafanye kwa vizuri ili *history* yetu ikae vizuri kama tunavyotarajia. *Inshaallha* Mwenyezi Mungu atatuwafikishia kwa mema yote.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, nimemfuatilia mtoa hoja kwa makini sana, mambo mengi kayaweka sawa, lakini kuna mambo mawili ningeomba tuwekewe sawa. Kwanza kwa upatikanaji wa mawaziri na pili la urais. Kwa sababu Mhe. Mtoa hoja alisema kwamba kura tuhesabu kwa kura za wawakilishi, lakini maoni ya huku wengi wanasema aa tuhesabu kwa viti na msimamo nafikiri bado uko huo huo kwamba kwa vyovyote vile mawaziri wapatikane kwa viti. Lakini hata lile la

makamo wa rais aliyesema kwamba kama kawekewa pingamizi, basi bila shaka tuje kwenye viti Barazani kwa sababu kutakuwa na chama kimoja kina viti vingi ndicho ambacho kitatakiwa kitoe makamo wa rais kutokana na viti vyake ndani ya Baraza na sio kura za wajumbe.

Mhe. Spika: nilifikiri unaleta *point* kuhusu utaratibu, hoja imetolewa sasa ilikuwa kiti hapa kielekeze namna ya kwenda kwenye hizi hoja na itapofikia hapo kama vile tunavyopitisha vitu kwenye Baraza zima basi hiyo *point* unaweza ukai-*raise*. Kwa hivyo, nataka nitoe muongozi kuhusu namna ya kwenda na hii kazi. Muongozo wa kwanza ni kwamba niliwaambia makatibu wangu hapa na mimi nilikuwa naifanya hiyo kazi hapa juu, pale mlipokuwa mnaniona kama siwasikilizi kwa kweli nilikuwa nachukua *points* kuhusu namna majadiliano yalivyokuwa yanakwenda kuna jambo gani labda limekubaliwa. Bahati nzuri majumuisho aliyofanya mheshimiwa hapa ndio mengi ambayo sisi tumefanya *summary*.

Kwa hivyo, nitawaomba na pengine itatusaidia katika kujikumbusha yale majumuisho aliyofanya Mhe. Abubakar hapa na hatimaye akamalizia kwa kutoa hoja. Kuna mengi ameyakubali na mengi hayo sisi tumeya-*summarize* katika waraka fulani. Tutaugawa waraka huo mtauona na kwa sababu aliyoyataja sijui kama umeandika Mhe. Abubakar pahala?

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Ndio nimeandika pahala.

Mhe. Spika: Sasa yanaweza kuowana sana kwa sababu ulipokuwa unafuatilia kwa karibu na mimi nilikuwa nina *tic* yale mambo ambayo tumekwenda sambamba na ile *summary* tuliifanya sisi. Watendaji hebu gaweni hizo nyaraka ili tuende kwenye utaratibu.

Wakati nyaraka zinatolewa jambo kama hili nadhani hatuwezi tukafuata kanuni moja kwa moja inavyohitaji, kwamba mtoa hoja ameshatoa hoja yake kwamba tuikubali kwa pamoja hiyo itakuwa ni ngumu, ambapo kanuni zinaelekeza tuwe tunafanya hivyo. Lakini kwa sababu hoja yenyewe ina vifungu mbali mbali tafauti kama alivyokuwa anafafanua hapa Mhe. Mtoa hoja, basi tutakwenda kwenye vifungu hivyo. Lakini wakati huo huo tumemuona hapa Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi ame…hebu ngoja nisimame sauti iingie vizuri, unajua unaposimama ile sauti inakuwa inaji-*gravity* inaingia vizuri zaidi.

Kwa hivyo, wacha nisimame ili na ile sauti iwe inakuja na mshindo ili iweze kufahamika vizuri. Hivyo tutakwenda kifungu kwa kifungu kama alivyokuwa anafafanua mtoa hoja. Pale ambapo kwa mfano Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi ameona kuna kitu kidogo hakijakaa sawa akasimama

pale nikadhani anasema *point of order* kumbe sivyo, ana hoji hii hii, ndio nikasema tutakwenda kifungu kwa kifungu mpaka pale tutapofikia halafu basi tuhojiane hapo.

Lakini utaratibu wa kuweza kusema kanyanyuka huyu na nini kwa kawaida kwenye miswada na kwenye miswada ile ya makadirio huwa tunaifanya kwenye Kamati ya Baraza Zima. Tuko pamoja Waheshimiwa? Kwa kawaida vile vifungu kwa vifungu ama vya makadirio au vya miswada kazi hiyo huwa tunaifanya kwenye Kamati ya Baraza Zima au kwenye Kamati ya Matumizi, lakini huu si mswada na wala sio mswada wa makadirio, kwa maana hiyo ili tuweze tusivunje utaratibu wa kanuni. Kwa sababu Spika anapokuwa kitini haki ya kusema iko mara moja tu, kwa mheshimiwa mjumbe. Unapokuwa kwenye Kamati ya Baraza Zima mjumbe ana nafasi ya kusema zaidi ya mara moja ndio tofauti kubwa.

Kwa maana hiyo basi, kwa kuwa huu si mswada bado Spika atakuwa hapa hapa kitini mlipomuweka isipokuwa sasa tutenge kanuni kando kwa mujibu wa kifungu cha 150 na kanuni yenyewe ya kuitenda kando ni kanuni ya 60(1) na zinazofuatia. Hizi itatuwezesha sisi tukikubaliana hoja ikatolewa hapa na kwamba kanuni hiyo ya 60 na vijalizo vyake tuitenge kando basi sasa tutakuwa tunakubaliana twende kama vile tunavyokaa katika Kamati ya Baraza Zima. Madhumuni ni nini?

Madhumuni ni kwamba tunapofikia kifungu ambacho hatujaelewana vizuri mjumbe mmoja anaweza kupata ya kusimama zaidi ya mara moja hasa mtoa hoja katika kutoa ufafanuzi lakini na maoni mengine kutoka kwa wajumbe wengine ndani ya chombo chetu. Nadhani tunakubaliana hiyo. Basi kabla hatujafika kwenye vifungu vyenyewe rai hiyo tuitolee hoja na nimuombe Mhe. Mjumbe mmoja asimame ili kutoa hoja ya kutenga kanuni hii ya 60 kando kwa mujibu wa kifungu cha 150 cha utengaji wa kanuni kando ili tuweze kupata utaratibu wa kwenda kwa utaratibu huo ninaousema. Haya.

TAARIFA

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba muongozo wa Spika kwa yule mjumbe ambaye hakubahatika kuchangia na aliomba je, katika kanuni ataruhusika naye kutoa yake aliyokuwanayo katika hayo? Naomba muongozo wako Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Tunakusudia kujenga na nia hasa tufikie pahala kama nilivyosema mapema pale asubuhi ni kitu gani tunawapelekea wananchi, kama tutasema tuwapelekee. Kwa hivyo *discretion* itatumika. Basi nione huyo

ambaye anataka atoe hiyo hoja tutenge hiyo kanuni ya 60 kando na vijalizo vyake ili tuweze kwenda kwa utaratibu nilioulekeza.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, tunaomba kutoa hoja kwamba kanuni ya 60 iwekwe kando tuendelee na kazi.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, kuitenga kanuni ya 60 kando na vijalizo vyake ili tuweze kupata utaratibu wa kushughulikia suala hili kwa kuweza kusimama mjumbe zaidi ya mara moja wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Sasa kanuni ile ya 60 tumeshaitenga kando na sasa ile nafasi ya kuja kuhoji kifungu na kifungu itakuwa ipo wazi na mjumbe anaweza akasimama zaidi ya mara moja. utengaji huu kanuni kando ni kwa sababu ya dharura ya jambo hili, tukimaliza kazi hii inarudi pale pale. Nafikiri ule waraka mmeuona.

Kwa hivyo, nambari moja Baraza lifanye marekebisho ya vifungu 9(3), 39, 42, 61. hii katibu nikumbushe tumeiweka wapi hii, kwa sababu haiku kwenye mtiririko wa moja kwa moja.

Katibu: Mhe. Spika, sisi hatukufuata utaratibu wa huku katika hoja, isipokuwa tuliangalia *issues* zenyewe. Kwa hivyo, ni vyema bora twende yote tumeya-*summarize* katika waraka huu tupitishe kwa mujibu wa waraka huu mpya tuliokubaliana.

Mhe. Spika: Tunakubaliana?

Waheshimiwa Wajumbe: Ndio.

Mhe. Spika: Basi kwenye waraka huu ambao umechukua pamoja na marekebisho sasa tunakwenda nao ambao kwa bahati nzuri mengi yao ndio yale ambayo Mhe. Mtoa Hoja ameyazungumza. Waheshimiwa tuko pamoja hapo?

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: Mhe. Spika, mimi binafsi yamenipita, sasa naomba tena urejee.

Mhe. Spika: Nasema hivi, tumetenga kanuni kando madhumuni yake ukiwa unataka kuhoji jambo zaidi utaratibu wa Barazani hapa nikikwita mara moja husimami tena, lakini kwa hili kwa sababu kanuni hiyo ya Nam. 60 tumeitenga kando sasa una nafasi kuuliza mara moja, mbili kama vile tunavyokuwa kwenye Kamati ya Baraza Zima, ndio madhumuni.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu: Kuhusu huu waraka Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waraka huu tume-*summarize* vile namna mlivyokuwa mnachangia. Waraka huu kwa kiasi kikubwa umechanganya na marekebisho mliyoyasema na bahati nzuri mengi yake ni yale ambayo Mhe. Mtoa Hoja amesema mimi hili nakubali, hili nakubali. Sasa ninachokisema tutakwenda kwenye waraka huu na mtoa hoja amekubali hivyo, na kama kuna jambo bado halijafafanuka basi utauliza mtoa hoja atasema na tutafikia pale ambapo tumefikia kwa mtazamo wa wengi. Tumekubaliana.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, muongozo wako tena. Nilivyofahamu mimi kwamba waraka huu umetayarishwa na meza ya watendaji, sasa katika waraka huu na kwenye *hansard* Mhe. Abubakar Khamis amezungumza pale na yameshaingia kwenye *hansard*. Sasa nitatoa mfano mmoja.

Point yake ya mwisho alipokuwa anachangia maandishi ya Mhe. Hamad Masoud point hii haimo humu. Je, tunafanyaje kwa hilo?

Mhe. Spika: Mimi huku nimei-*note down* hiyo *point* ambayo tumeisema, nilipotizama nyuso hapa ikawa jambo hilo halijafafanuka vizuri. Mhe. Waziri wa Nchi pale amesema, tukifika hapo tutairudia ili tufahamishane mpaka tufikie pahala. Tumeelewana. Nani anasoma? Katibu.

Katibu: Mhe. Spika, tumeanza kwa kusema kwamba Baraza la Wawakilishi katika hoja hii ya mjumbe Mhe. Abubakar Khamis Bakari, Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni Pemba linakubaliana na hoja hiyo katika baadhi ya mambo na limekubali baadhi ya mapendekezo ya wajumbe kufanya marekebisho katika baadhi ya vipengele. Maamuzi ya Baraza ni kama yafuatayo:-

Kwanza, Baraza la Wawakilishi linapongeza mazungumzo ya maridhiano yaliyofanyika tarehe 5 Novemba, 2009 baina ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Amani Abeid Karume ambaye ni Makamo Mwenyekiti wa CCM Zanzibar na Maalim Seif Sharif Hamad Katibu Mkuu wa *CUF*.

Mhe. Spika: *Item* hiyo inakubaliwa?

Waheshimiwa Wajumbe: Ndio.

Katibu: Pili, kimsingi Baraza limekubali kwamba ipo haja ya kufanywa kura ya maoni *referendum* itakayowashirikisha wananchi moja kwa moja katika kupata ridhaa ya wananchi kuhusu uanzishwaji wa Mfumo na Muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika: *Item* hiyo inakubaliwa?

Waheshimiwa Wajumbe: Ndio.

Mhe. Spika: Hebu ngoja kidogo, Mhe. Abass Juma Muhunzi hebu tusikie hooja yako.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, mimi nakubali hii *referendum* lakini suala lililokuweko katika *referendum* ilikuwa ifanyike katika mwezi wa Mei, yakatoka maoni humu kwama iende zaidi isije ikafika uchaguzi. Hapakuwa na tareha ambayo ilikuwa *fixed.* Kwa hivyo, mimi nilitaka nipate maelezo ni wakati gani ambao tunataka kufanya *referendum*. Hilo ni moja.

Lakini la pili je, *referendum* hii ambayo itaingizwa katika katiba, ni *referendum* kwa ajili ya jambo hili tu. Tunaingia katiba kwa kufanya jambo hili tu, au sasa *referendum* itaangalia na mambo mengine ambayo yanaweza baadae yakajitokeza katika nchi. Kwa sababu kuingiza kitu katika katiba ambacho kinashughulikia hiki tu kikishamaliza iko *redundant* mimi nilikuwa nikifikiria hilo tupate maelezo ili tufahamu nini tunaondoka nacho.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, katika suala lake la mwanzo katika kifungu cha 13 katika hii tuliyopewa inakidhi haja. Kinasema marekebisho ya sheria ya uchaguzi hatua ya kutaka ridhaa ya wananchi kwa njia ya kura ya maoni na marekebisho ya katiba endapo wananchi wataridhia Uanzishwa wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Yote hayo yafanywe kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010.

Halafu suala lake la pili ni kwamba hapa tunazungumzia suala la *referenduma* na ndio nikasema tuliweke katika misingi ya kikatiba. Lakini serikali haifungiki na kufanya jambo jengine lolote kwa njia ya *referendum.* Unapotunga sheria ya *referendum* ile inakuwa ni *open* si kwa mambo ya uchaguzi tu na vitu vyengine, lakini ni kwa mambo yote ambayo serikali itahisi inawajibika kuwapelekea wananchi. Kwa hivyo, hii haifungi wakati wa uandikaji wa sheria.

Mhe. Spika: Katibu irudie tena, tulimpa nafasi mjumbe ingawatulikwishaitaja.

Katibu: Kifungu cha pili ni kwamba, kimsingi Baraza limekubali kwamba ipo haja ya kufanywa kura ya maoni itayowashirikisha wananchi moja kwa moja katika kupata ridhaa ya wananchi kuhusu uanzishaji wa Mfumo na Muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar.

Mhe. Spika: naiuliza tena tumekubaliana?

Waheshimiwa Wajumbe: Ndio.

Katibu: *Item* Nam. 3 ni muundo unaopendekezwa ni kuwa na rais mtendaji ambaye atapatikana kutokana na kupata ushindi kwenye kura za rais atayesaidiwa na manaibu rais wawili, naibu rais wa kwanza atatoka chama kilichoshika nafasi ya pili katika kura za rais na naibu rais wa pili atatoka chama anachotoka rais na huyo naibu rais wa pili ndiye atakuwa kiongozi wa shughuli za serikali kwenye Baraza la Wawakilishi na atakuwa ndiye mrithi wa rais endapo litatokea lisilotarajiwa.

Mhe. Spika: Samahani hivi sasa umetangulia wewe, lakini hoja hii nilimwambia Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi tutapokuja hapa atasema maneno yake.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, hapa naona pamekaa sawa, lakini kuna jambo moja nalipendekeza kwa Baraza hili kubadilisha tu jina. Mimi napendekeza tuseme makamo wa rais sio naibu wa rais. Kwa sababu ya kujenga hadhi kidogo hivi na utendaji.

Mhe. Spika: Tuondoe naibu wa rais iwe makamo wa rais. Sawa tunaondoa naibu.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, kwa bahati na mimi nilikuwa hii ndio *suggestion* yangu. Kwa sababu hata katika hayo makubaliano ya *CUF* na CCM huko Bagamoyo ninayo hapa, ni kwamba inasema kutakuwa na Makamo wa Rais wa Zanzibar. Kwa hivyo, neno sahihi ni Makamo wa Rais.

Mhe. Juma Duni: Mhe. Spika, tumeowana kwa suala la Makamo na Naibu, kwamba naibu iondoke ni makamo, na ilikuwa kwa sababu nilikuwa na kumbukumbu hii aliyosema Mhe. Abubakar Khamis Bakary. Nakushukuru.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, rais shughuli zake zimetajwa katika katiba, na makamo wa pili wa rais kwa mujibu wa mabadiliko haya atakuwa ni mkuu wa shughuli za serikali katika Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, na yeye kazi zake zimekwishatajwa, nini zitakuwa kazi za Makamo wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, hapa tunazungumzia ile principle, sasa unapoandika katiba, katiba haikuruhusu kuandika tu kwamba kutakuwa na hichi na hichi mpaka zile kazi zake uziweke. Kwa hivyo, Makamo wa Rais wa Kwanza zitawekwa kazi zake, Makamo wa Rais wa Pili zitawekwa kazi zake na kila mtu zitawekwa kazi zake kwa mujibu wa katiba.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa sana na taadhima jambo tunalolifanya ni jambo kubwa. Hata kama Makamo wa Pili wa Rais hatutoweka kazi yoyote, lakini ile kusema ni Mkuu wa Shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi kazi zake zimekwishajulikana na Rais tayari kwenye katiba hii zipo. Lakini leo tukiondoka hapa mtu mkubwa Makamo wa Rais hatujamjua kazi zake. Mimi Mhe. Spika, bado sijatosheka.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, hapa hatupitishi katiba, tunapitisha mfumo. Sasa katiba ikiwa haikutaja kwa sababu katiba baadae si itakuja hapa Barazani na itasema kazi za kila mtu. Sasa pale kama haipo hapo hata mimi sitokubali. Lakini hapa huu ni mfumo, kwa hivyo mfumo ni kitu ambacho tunakijenga, sasa baadae itakapokuja ile katiba na utaratibu wake na sheria ndio kila kitu kitakuwemo mle. Kwa hivyo, hii hapana tatizo Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Tunajenga *structure* lakini viti vitakaa wapi, watu watalia sehemu gani, hiyo itakuwa baadae. Si ndio hivyo. Mhe. Abass Juma Muhunzi tena. Nadhani tumekubaliana

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, mimi naomba ufafanuzi kidogo, sina tatizo kwenye Rais na Makamo wa Pili wa Rais, lakini Makamo wa Kwanza wa Rais. Kuna wakati Mhe. Abubakar Khamis Bakary anajumuisha hoja yake pale na ninaomba nitumie mfano huo huo alimtaja Mhe. Haji Omar Kheri, sasa tuchukulie Mhe. Haji Omar Kheri ndio Rais na Makamo wake wa Pili Mhe. Hamza Hassan Juma.

Sasa kumewekwa pingamizi ilizungumzwa hiyo pointi ndio sikuifahamu. Imewekwa pingamizi juu ya yule mgombea wa chama chengine nap engine tuna vyama zaidi ya viwili au vitatu ndani ya Baraza la Wawakilishi wakati huo. Je, ile pingamizi yule Makamo wa Kwanza wa Rais atapatikana vipi, labda atufafanulie zaidi.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, mimi nilisema kwamba hoja ya Mhe. Hamad Masoud Hamad ilikuwa na mantiki. Nikatoa mfano kabla hatujampata Makamo wa Pili wa Rais, tunazungumzia suala la Rais tu. Suala la Rais wakati tunapotaka kugombea Urais kila chama kinapeleka jina lake la mgombea katika Tume ya Uchaguzi. Kwa hivyo, mimi nikatoa mfano kwamba

kuna chama A, B na C ambavyo vyote vimepeleka majina yao ya wagombea wake katika uchaguzi kwamba wao watasimamia uchaguzi na watagombea nafasi ya Urais.

Kwa bahati nzuri au mbaya, chama A kikaweka pingamizi kwa mgombea wa chama B na pia kwa mgombea wa chama C. Ikasikilizwa pingamizi yao kwa utaratibu ambao tumeuweka na pingamizi ile ikakubalika.

Kwa hivyo, kwa mujibu wa sheria zetu za uchaguzi ni kwamba sasa kutakuwa na mgombea mmoja wa Urais wa chama kimoja, vyama vyengine vyote vile vitakuwa vimeshaenguliwa. Sisi tutaingia katika uchaguzi na mgombea mmoja, kwa hivyo yule *definitely* ndie atakayekuwa Rais.

Sasa swali linakuja Makamo wa Rais wa Kwanza atapatikana vipi? Kwa sababu wa pili atateuliwa na Rais, kwa hivyo si *problem* hiyo. Sasa mimi nikasema kwa misingi hiyo kwa sababu hakuna kura za Rais namba mbili pale itabidi twende katika Baraza. Idadi ya kura za vile vyama zilizopata za wawakilishi wao, zile ndio zita-*determine* nani au chama kipi kiwe Makamo wa Rais wa Kwanza. Huku hatuna kura za Rais kwa sababu wote wameshaenguliwa. Kwa hivyo, pahala ambapo tunaweza tukapahalalisha ni wawakilishi wao walioingia katika Baraza la Wawakilishi, zile kura zao za wawakilishi wao waliomo katika Baraza, zile ndio iwe *determining factor* ya kumjua Makamo wa Kwanza wa Rais, ndio nilivyosema.

Mhe. Spika: Unakusudia jumla ya kura za wawakilishi wa upande huu wa chama fulani, jumla ya kura za chama fulani ndani ya Baraza na jumla ya kura kama kuna na chengine ya chama fulani. Ndio unavyokusudia za wawakilishi wale waliomo?

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, ninachokusudia ni kwamba kwa sababu ni wagombea watatu A, B na C, lakini B na C wameenguliwa. Kwa hivyo, A atakuwa ameshajulikana ndio Rais, sasa vile vyama viwili vilivyobakia B na C idadi ya kura zao zilizomo ndani ya Baraza. Kwa hivyo, B na C mmoja hapo atakuwa ndio Makamo wa Rais kwa mujibu wa kura zao za wawakilishi waliomo ndani ya Baraza.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, tatizo hili nakumbuka limeshawahi kutokea kisiwani Mauritius wakati wa uchaguzi wa Rais Ram Gullam kwa sababu kule wana mfumo kama huu ambao tunaujadili sasa hivi sisi na kujaribu kuupitisha hapa. Ilipotokezea chama kile cha tatu kilijitoa kwa sababu hakikuwa kinam-*support* yule mgombea wa upinzani.

Yule mgombea ambaye ameshawekewa pingamizi sasa si mgombea tena wa Makamo wa Kwanza wa Rais. Je, katika hivyo vyama vilivyobakia ndani ya Baraza, kitaleta mgombea miongoni mwa wale wajumbe wa Baraza kutoka vyama vile au vipi.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, hata hivi sasa ni chama ambacho kinatoa mgombea. Kwa hivyo, ikiwa kile chama B na C, tuseme chama B kimepata kura laki moja na C kimepata kura 80,000. *Definitely* chama B ndio chama ambacho kitatoa Makamo wa Rais wa Kwanza. Sasa utaratibu huo kwa mujibu wa makubaliano haya ya Bagamoyo na Butiama ni kwamba hapo litapelekwa katika chama husika, chama husika ndio kitasema kwamba huyu ndio Makamo wetu wa Rais.

Mhe. Spika: Lakini *of course* asije yule aliyeenguliwa.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, hapa sina jibu, isipokuwa jibu litakuja katika katiba. Katiba ikisema kwamba yule aliyeenguliwa hatoruhusiwa tena kuwa Makamo wa Rais *of course* tutakuwa tumeshaweka wazi. Lakini ikiwa katiba haitosema hivyo hatuwezi kumzuia. Sasa hizo mimi napendekeza itakuwa ni *details* za hapo tunapojadili yale marekebisho ya katiba.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, mimi nina swali katika hili hili. Mjumbe anasema kwamba tuchukue idadi ya kura za wale wawakilishi wa vile vyama waliomo Barazani kwa kila chama B na C. Lakini likitokea tatizo kwamba B ana kura laki moja lakini wawakilishi wake ni wanne tu, C ana kura 60,000 wawakilishi wake ni watano tutaamua vipi hao.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, hiyo si tatizo. Tukisema kwamba suala ni kura, kwani Marekani kura za Rais ni nyingi, lakini zile za watu wake katika *House of Commons* ni ndogo. Sasa *once* tukisema kwamba kura zinazo-*determining factor* hapa ni kura za wawakilishi wao katika hayo majimbo, *it means* ni kura, *whether* yule ana laki moja lakini ana viti vitatu, kwa hivyo yule bado atakuwa ndio Makamo wa Rais lakini ana viti vitatu. Yule kama ana 60,000 atakuwa ha-*qualify* kwa misingi hiyo ingawa ana viti vitano. Ndio utaratibu ulivyo sehemu zote.

Mhe. Spika: Jamani hapa tunachotaka kufahamiana ni wakati huo utakapokuja Mswada wa Marekebisho ya Katiba. Lakini ile *structure* hivi sasa kimsingi tumekubaliana. Nafikiri ni sawa mtoa hoja. Sasa pointi hii inakuwa *noted* mpaka wakati huo yule *exception* hizi ndio zitakuja kuonekana huko. Nadhani unakusudia hivyo.

Mhe. Spika: Mhe. Spika, Zanzibar ni nchi, anayesema si nchi muache ajifurahishe. Sisi hapa tuko tunajadili mustakbali wa nchi yetu Zanzibar na ndio maana tumefanya mapendekezo mbali mbali ambayo yameridhiwa. Lakini Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa naomba nitolewe wasi wasi na hofu iliyonijaa moyoni mwangu. Tunazungumzia vyeo vya Makamo wa Rais lakini tayari tunae Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hapa tunataka kuanzisha Makamo wa Rais wa Zanzibar.

Mhe. Spika, wasi wasi wangu uko hapa. Makamo wa Rais hao watakuwa Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamo wa Rais wa Zanzibar. Kwa mfano, Makamo wa Rais wa Zanzibar ni Mhe. Said Ali Mbarouk, Makamo wa Rais wa Zanzibar wa pili Ramadhan Nyonje Pandu. Sasa hapa hakuna muingiliano wowote wa kikatiba na migongano mitafaruku kidogo.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, mimi sifikiri kwamba kutakuwa na mgongano. Kwa sababu hivi sasa tuna Jamhuri ya Muungano, tuna Rais wa Zanzibar, sasa unaposema una-*qualify* ni Rais wa Zanzibar, Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Makamo wa Rais wa Zanzibar, Makamo wa Rais wa Pili wa Zanzibar. Sasa hiyo peke yake inaonesha kwamba huyu ni Makamo wa Rais wa Zanzibar wa nchi yako unayoipenda.

Hata Mawaziri Mhe. Spika, si kuna Waziri wa Kilimo wa Jamhuri ya Muungano, Waziri wa Kilimo wa Zanzibar, kwa hivyo hakuna *confusion* ambayo italetwa.

Mhe. Spika: Ni kuwataja kikamilifu kwa mujibu wa wadhifa na kutoka upande upi.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, linalozungumzwa hapa na mimi naunga mkono kwamba ni suala la nchi yetu kwa ajili ya wananchi wetu na huwezi kupanga kitu bila ya kujua utaratibu mzuri. Lakini Mhe. Spika, pamoja na hayo maazimio ya Bagamoyo yaliyozungumzwa hapa, suala la Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais, kimfumo Makamo wa Pili wa Rais atakuwa ndio Mtendaji Mkuu wa Shughuli za Serikali.

Je, katika mambo ya itifaki, ndio haki yangu niulize, huyo anayeguta hiari yake. Mhe. Spika, katika suala la itifaki Makamo wa Pili wa Rais na Makamo wa Kwanza wa Rais nani atahudhuria mwanzo katika hafla yoyote. Aaa ndio tujue eti.

Mhe. Spika: Sitaki nijibu mimi lakini mtoa hoja atasema.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, hii ni *structure* ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tunasema *structure* yenyewe iwe na Rais ndio *head* na Makamo wa Kwanza wa Rais ndio msaidizi wake mkuu, halafu kuwe na Makamo wa Pili wa Rais. Sasa kiitifaki Makamo wa Kwanza wa Rais ni mkubwa na atahudhuria mwanzo kuliko Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika: Katika kuhudhuria atahudhuria mwisho kabla ya Makamo wa Pili, katika kuondoka ataondoka mwanzo kabla ya Makamo wa Pili. Nadhani sawa. Sasa tuendelee.

Katibu: Muundo unaopendekezwa ni wa kuwa na Rais Mtendaji ambaye atapatikana kutokana na kupata ushindi kwenye kura za Rais atakayesaidiwa na Makamo wa Rais wawili. Makamo wa Rais wa Kwanza atatoka chama kilichoshika nafasi ya pili katika kura za Rais na Makamo wa Rais wa Pili atatoka chama anachotoka Rais, na huyo Makamo wa Rais wa Pili ndie atakuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali kwenye Baraza la Wawakilishi na atakuwa ndie mrithi wa Rais endapo litatokea lisilotarajiwa.

Kifungu cha 4 - Baraza limekubali kwamba katika mfumo huo Rais atateua Mawaziri kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuzingatia uwiano wa viti vya majimbo kwa vyama vya siasa vilivyomo kwenye Baraza.

Kifungu cha 5 - Baraza la Wawakilishi linasisitiza kwamba Serikali hiyo ya Umoja wa Kitaifa itakayoundwa itaendelea kuheshimu na kuthamini misingi mikuu ya Mapinduzi ya tarehe 12 Januari, 1964.

Mhe. Spika: Hii mtoa hoja alisema kuna vijifungu vile tulitoa na mawazo hapa kwamba vinarekebishwa kufuatana na sera na mambo yalivyo wakati huu. Nafikiri ni sawa. Kwa hiyo, kifungu hichi pamoja na marekebisho yake, marekebisho ndio yale vifungu a, b, c?

Katibu: Mhe. Spika, marekebisho ndio tumeshayafanya kwa sababu hatukuweka hivyo vitu vilivyokuwa vimeongezwa. Kwa hivyo, hivi ndio itabakia vile.

Kifungu cha 6 - Serikali ilete kwenye Baraza la Wawakilishi haraka iwezekanavyo mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kuifanyia

Marekebisho Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar Nam. 11 ya 1984 kwa madhumuni ya kuweka utaratibu, masharti na namna ya uendeshaji wa kura ya maoni, na pia kuipa mamlaka Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar mbali ya majukumu yake iliyonayo sasa. Pia kusimamia na kuendesha kura ya maoni kwa yale masuala mazito yanayohitaji maamuzi ya wananchi moja kwa moja.

Kifungu cha 7 - Baraza la Wawakilishi inaviomba, Mhe. Abubakar Khamis Bakary alisema inavishauri vyama vyote vya siasa vyenye Wajumbe kwenye Baraza la Wawakilishi na vilivyo nje ya Baraza la Wawakilishi kujikubalisha kuunga mkono hoja itakayopelekwa kwa wananchi ya kuwaomba kuridhia na kuidhinisha uanzishwaji wa mfumo huo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Kamal Basha Pandu: Mhe. Spika, mimi nilikuwa naomba tufanye marekebisho madogo hapo kwa sababu tukiiacha kama ilivyo inaonekana kwamba kama maamuzi yameshafanyika. Tuiondoe moja, mbili, tatu, nne, mstari wa nne hapo kuanzia wananchi "ya kuwaomba kuridhia na kuidhinisha". Nafikiri maneno hayo yatoke yaanzie wananchi ya uanzishwaji wa mfumo huo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika: Sasa kuwaomba kuridhia au kuwaomba kuidhinisha uanzishwaji. Hebu tuondoe lipi hapo.

Mhe. Kamal Basha Pandu: Mhe. Spika, kuridhia sio kuidhinisha.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, hapa ni katika suala lile la wajumbe kuwaomba wananchi kuunga mkono hii. Sasa unapowaomba unaomba mambo mawili waridhie kwamba wao wenyewe wakubali hili suala, halafu watoe *concept* yao kwamba sasa fanyeni. Yaani sisi hatuwezi kufanya kabla hatujapata ridhaa ya wananchi, wao ndio watatuidhinisha sisi. Kwa hivyo, hii kuwaomba na kuridhia ni sahihi kwamba wao lazima watuidhinishe sisi, vyenginevyo hatuwezi kufanya bila kutuidhinisha, ndio madhumuni yake.

Mhe. Spika: Kwa hiyo, ilivyo hapa ndio sahihi.

Mhe. Kamal Basha Pandu: Mhe. Spika, kama katika Kiswahili ni sawa sawa basi naafiki.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, bado kifungu hichi cha 7 naona kama kimenikalia sio sahihi. Mhe. Spika, naomba ninukuu. "Baraza la Wawakilishi inaviomba vyama vyote vya siasa vyenye Wajumbe kwenye Baraza la Wawakilishi kujikubalisha kuunga mkono hoja itakayopelekwa kwa wananchi ya kuwaomba kuridhia na kuidhinisha uanzishwaji wa mfumo huo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa".

Sasa ni kuwashawishi kujikubalisha kuunga mkono. Mhe. Spika, mimi hapa kidogo sijafahamu. Kwa sababu wananchi sisi wajibu wetu serikali inawapelekea katika hiyo maamuzi yao. Sasa je, kama hawakuridhia. Hapa kuna mambo mawili, kuridhia na kutokuridhia. Mhe. Spika, mimi nataka nifahamishwe zaidi.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, kupeleka kwa wananchi kuna mambo mawili. Tunawaomba waridhie halafu watuidhinishe. Wao wana maamuzi yao unaweza ukawaomba lakini wakasema hili hatulikubali. Hata katika hiyo Sheria ya *Referendum* lazima kuwe na kifungu kinachosema kwamba maamuzi ya wananchi walio wengi ndio yatakayoheshimiwa.

Kwa hivyo, ikiwa wengi wamesema kwamba ni *no*, lazima tuheshimu *no* yao. Hii nafikiri ni sawa sawa, tunawaomba waridhie na watuidhinishe. Lakini wanaweza wakasema sisi haturidhii wala hatutaki, itakuwa ndio basi.
Mhe. Spika: Au Mhe. Ali Suleiman Ali ulikuwa unaulizia kama vyama vyengine vitakataa, maana vinaombwa vyama hapa viwaambie wananchi waridhie na waidhinishe.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, niko kwa wananchi wangu. Kwa hivyo, nimekubali baada ya maelezo mazuri sina pingamizi.

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman: Mhe. Spika, sina pingamizi na hichi kifungu, lakini hapa ni vyama ambavyo vimo katika uwakilishi tu, vile vyama vidogo vidogo tumevisahau kuvitia na wao wawemo.

Mhe. Spika: Mheshimiwa mtoa hoja kuna hoja pale kwamba vyama vyote vile *of course registered.*

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, hii ni kweli kwa sababu hata katika *summary* yangu nilisema kwamba vyama vyote, ni vizuri tuwashirikishe wananchi wote.

Mhe. Spika: Pale tunafanya marekebisho ya hii iliyopo kwamba Baraza la Wawakilishi inaviomba vyama vyote vya siasa, hii "vyenye wajumbe" nadhani iondoke sasa. Ni sawa. Vyama vyote vya siasa vilivyosajiliwa. Nadhani tunaendelea.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, mimi naomba kusaidiwa kwanza. Huku nyuma tumeshakuwa na kipengele tumekubaliana kuwa suala hili lipelekwe kwa wananchi kama ni *referendum* kutoa maoni yao. Lakini tunaingiza kipengele hiki, hivyo kweli uhuru wa huyo mwananchi si tutakuwa tunamuingilia kwa kipengele hichi. Hapati uhuru wa mwenyewe kuweza kuamua kwa kwenda kumshawishi, mimi naona kama kinapingana kuwapa uhuru watu kwenda kutoa maoni.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe ana hofu kwamba kuviambia vyama na kuviomba vitaingilia uhuru wa wananchi katika kuridhia na kuidhinisha jambo hilo.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, uhuru wa wananchi hauingiliwi kwa njia hii. Kwa sababu *referendum* ni sawa sawa na uchaguzi mwengine wowote ule, isipokuwa hatuchagui mtu, tunachagua neno au hoja.

Sasa kwa mujibu wa Sheria ya *Referendum* lazima kuwe kuna kampeni sawa sawa na unavyofanya kampeni ya chama chako au chama changu kumshawishi mtu kwamba akupigie kura wewe. Pale humuingilii uhuru wake, unamkampeni akikubali sawa, akikataa ni sawa. Pale anapokataa ukamlazimisha ndio hapo unamuingilia uhuru wake. Lakini katika kufanya kampeni au kufanya ushawishi uliohalalishwa kisheria, hiyo si kumuingilia uhuru wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, katika majumuisho ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary wakati anazungumza pale kwa vifungu vyote viwili, cha 6 na cha 7, ingawa cha 6 tumeshakipita, alitaja katika *hansard* imo pia "… kabla ya Uchaguzi Mkuu". Sasa je, hilo linaondoka au vipi.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, iko katika ukurasa wa 3 kifungu cha 13.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, katika kifungu cha 7 hii ni *process* ya kuwaomba, sasa hii ya huku ni majumuisho. Je, tunachukulia majumuisho haya ni kwa vifungu vyote?
Mhe. Spika: Ulitaka iweje hapa?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, sio nilivyotaka, vile ilivyojumuishwa ndio ninavyozungumza mimi.

Mhe. Spika: Uliona iweje?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, nilivyosikia wakati inajumuishwa "Baraza la Wawakilishi inaviomba vyama vyote vya siasa vilivyosajiliwa kujikubalisha kuunga mkono hoja itakayopelekwa kwa wananchi ya kuomba kuridhia na kuidhinisha uanzishwaji wa mfumo huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kabla ya Uchaguzi Mkuu".

Mhe. Spika: Kwa hiyo, iwekwe kabla ya Uchaguzi Mkuu.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, kifungu cha 13 kinasema hivi: "Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi, Hatua ya Kutaka Ridhaa ya Wananchi kwa Njia ya Kura ya Maoni na Marekebisho ya Katiba endapo Wananchi wataridhia Uanzishwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, yote hayo yafanywe kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2010.

Kwa hivyo, haya ni mambo matatu na yote yanasema kwamba yafanywe kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2010. Sasa imeingiza kila kitu.

Mhe. Spika: Tayari amekubali.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, mimi nilikuwa na hoja tu kwamba kwani hichi kifungu cha 7 kikiondoka, hichi kifungu cha 13 si kimeshamaliza mambo yote.

Mhe. Spika: Je, hicho kifungu cha 13 hakikidhi haja.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, kifungu cha 7 Baraza la Wawakilishi hapa tunalihusisha na vyama vya siasa vilivyosajiliwa kihalali. Kifungu cha 13 tunazungumzia kwamba mambo haya ya kura ya maoni na urekebishaji wa Sheria ya Uchaguzi yafanywe kabla ya Uchaguzi Mkuu. Kwa hivyo, ni kitu tofauti.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri umeiona hiyo tofauti iliyopo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, nimeiona, lakini ilikuwa wasi wasi wangu mimi ni kwamba na kwa sababu hiki kifungu kimeleta mjadala mkubwa, wanaoitikia wanaitikia shingo begani nahisi kwani kikiondoka kitakuwa kimeharibu maana.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, mimi sijaona kwamba wameitikia shingo begani kwa sababu wana uhuru, kama hawajaridhia au harajaridhika basi waseme huo ndio uhuru. Mimi nahisi vifungu hivi ni tofauti.

Sasa tukijadili kimoja kimoja, lakini tusiseme kwamba kinaondoka kimoja kwa kukipisha chengine. Maana yake ni tofauti kabisa.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, ninavyozitizama mimi hizi hoja ni kwamba hapa tunaweka hoja ambazo baadaye, aidha hiyo kamati pamoja na tume ya uchaguzi watatoa dondoo za kwenda kuwauliza wananchi katika huo waraka utakaopelekwa kwenye *referendum*. Sasa sidhani katika dondoo zile kutakuwa na kifungu kinamuuliza mwananchi je, unakubali vyama vilivyosajiliwa vije vikushawishi. Aidha kusema ndio au hapana. Nahisi kifungu hiki kiko *more* kwenye *process* kuliko kwenye zile dondoo zenyewe ambazo ni za msingi tunataka kuzipeleka kule.

Mhe. Spika, kwa sababu ukitizame nyengine zote zinatupa mwelekeo kwamba je, wananchi washirikishwe kuulizwa hili na kuulizwa hili. Lakini kifungu hiki, *and for that matter* Mhe. Spika, naomba unisamehe sana niseme na kifungu cha 8 ambacho hata mtoa hoja alikubali kwamba kinaweza kikawa hakipo. Hayo ndio maoni yangu Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Kwa hivyo, maoni yako hiki kiondoke.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Ndio Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ngoja kwanza. Sasa labda tuzikusanye hizi, maana nilikuwa nimeanza kutamka hii ni ya mwisho. Vipi kuna hoja tofauti Mhe. Rashid.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ndio Mhe. Spika. Mhe. Spika, ukikisoma sana hiki kifungu kwa undani ni elimu ya uraia, na hakuna wasi wasi kwamba suala hili na uzito wake ulivyo linahitaji elimu ya uraia. Kwa hivyo, tukubaliane kwamba iwapo tutaondoa vyama vya siasa tuikabidhi kamati shughuli hii. Lakini kilichokusudiwa hasa ni elimu ya uraia kuhusu hili jambo, lakini huwezi kukiondoa kifungu hiki moja kwa moja, unaweza ukabadilishia nani atakaye-*play role* ya kutoa elimu, lakini sio kukiondoa kifungu hiki. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, mimi nafikiri tunazozana kwa jambo dogo sana. Nadhani Mhe. Moh'd Ali Salim kama hajakisoma hiki kifungu ni vizuri akisome tena. Mimi nadhani kama nitakuwa nafahamu vizuri Kiswahili, hiki kifungu lengo lake ni moja tu, ni kuviomba vyama vya siasa vilivyopata usajili kukubaliana na hii hoja ya kwenda kwa wananchi na sio jambo jengine, ni kuviomba hivi vyama vikubali. Kama nitakuwa nafahamu vizuri Kiswahili nafikiri hii ndio maana ya hiki kifungu. Hii elimu ya uraia sidhani kama wanabebeshwa vyama kwenda kuitoa kwa wananchi. Kwa hivyo,

kama hakuna haja ya kuviomba vyama vya siasa vikubaliane na hii hoja, basi tukifute.

Mhe. Spika: Mimi nilikuwa na *consign* moja tu ambalo naomba muniwie radhi sana. Pengine wasi wasi isije ikatokea *distortion* ya lile ambalo linapelekwa kwa wananchi, kama kuna wasi wasi huo, basi kazi hii pengine ile inayotajwa kwamba labda kuna kamati ifanyiwe kati sijui kama ndio ile ya watu sita au vipi, sina hakika. Lakini kama kuna wasi wasi kwamba vyama vinaweza vikafanya *distortion*. Kwanza kuna vyama vingine pengine havihisi kama vitapata viti.

Kwa hivyo, kama tuna wasi wasi wa kwamba vyama vinaweza vikajakufanya *distortion* na lile jambo ambalo tumelipitisha hapa kulipeleka kwa wananchi, basi hapo kweli tatizo la kuwepo hapa juu ya kazi hiyo kufanywa na vyama ni tatizo. Lakini kama tunaridhia kwamba vyama vitafanya kazi vilivyo, nadhani itakuwa haina tatizo. Sasa mtoa hoja hebu tusaidie.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, kwa sababu lengo kama nilivyosema mwanzo ni kujenga. Kwa sababu huku kwenye hii kamati, kama nilivyosema mwanzo itashughulikia mambo hayo kwa kuishauri serikali, basi mimi nakubali tuiondowe.

Mhe. Spika: Kwa hivyo, kifungu nambari 7 tunakubali kukiondowa.

Wajumbe: Ndio.

Katibu: Kifungu cha (viii)

> Endapo itaona inafaa serikali ifanye mawasiliano na nchi rafiki, washirika wa maendeleo na jumuia za kimataifa kwa lengo la kuona uwezekano wa kusaidiwa gharama za uendeshaji wa kura za maoni ili kupata ridhaa ya wananchi katika suala hili.

Kifungu hiki pia Mhe. Abubakar Khamis katika majumuisho alikiondowa.

Mhe. Spika: Kwa hivyo, kifungu cha (viii) pia kimeondolewa.

Wajumbe: Ndio.

Katibu: Kifungu cha (ix)

> Endapo katika kura ya maoni wananchi wataridhia uanzishwaji wa mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, basi serikali iandae mswada wa marekebisho ya katiba ili

uletwe kwenye Baraza la Wawakilishi kwa madhumuni ya kufanya marekebisho katika katiba ya Zanzibar kukidhi maamuzi hayo ya wananchi. Marekebisho hayo yatahusu vifungu vyote vya katiba ambavyo vitalazimika kurekebishwa kwa ajili hiyo, vikiwemo vifungu vya 9, 39, 42 na vyenginevyo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, mimi sina tatizo na maelezo haya, isipokuwa tu niombe serikali kwamba itakapofanya marekebisho ya katiba, basi iangalie vifungu vyote kwa sababu katiba yetu ina marekebisho mengi. Ahsante.

Mhe. Spika: Hiyo na vyenginevyo ndio inachukua nafasi hiyo. Nadhani wala sina haja ya kumpatisha kazi mtoa hoja.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mimi nilikuwa naomba kwamba kwa sababu mtoa hoja alikitaja kifungu cha 61, basi kiingizwe halafu ndio ije na vyenginevyo. Vifungu vya 9, 39, 42, 61 na vyenginevyo. Nilikuwa naomba hilo tu.

Katibu: Mhe. Spika, kifungu cha 61 maelezo yake ndio hii hoja nyengine ambayo tunataka kuisoma, ambayo ni ya wakuu wa mikoa.

Mhe. Spika: Hoja hiyo iko mbele huko.

Katibu: Ambapo kifungu kinachofuata kiko kwenye ukurasa wa 3.

Mhe. Spika: Kifungu hicho tunakubaliana?

Wajumbe: Ndio.

Katibu: Kwenye ukurasa wa 3, hapa sisi tuliweka mapendelezo matatu, lakini kwa mujibu wa majumuisho ni kwamba inaonekana kitasomeka kama hivi ifuatavyo: Tutasoma mstari wa kwanza na mistari mitatu ya mwisho.

Kifungu cha (x)

Baraza limekubali kwamba Wakuu wa Mikoa waondolewe kabisa kwenye siasa yaani wasiwe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wateuliwe na Rais kama atakavyoona inafaa.

Mhe Spika: Kifungu kimekubaliwa?

Wajumbe: Ndio.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, Wakuu wa Wilaya mbona wameondoshwa.

Mhe. Spika: Ipo chini yake.

Katibu: Kifungu cha (xi)

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishili limekubali kuwa uteuzi wa nafasi za Wakuu wa Wilaya uendelee kama ulivyo sasa.

Mhe. Spika: Kinakubaliwa?

Wajumbe: Ndio.

Katibu: Kifungu cha (xii)

Baraza limekubali iundwe kamati ya Wajumbe sita, watatu kutoka upande wa Serikali na watatu kutoka upande wa upinzani kwa madhumuni ya kusimamia hatua zote zilizopendekezwa kwenye utekelezaji wa maamuzi ya hoja hii hadi kukamilika kwake.

Mhe Spika: Kinakubaliwa?

Wajumbe: Ndio.

Katibu: Kifungu cha (xiii)

Kifungu cha mwisho, Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi, hatua ya kutaka ridhaa ya wananchi kwa njia ya kura ya maoni na marekebisho na marekebisho ya Katiba endapo wananchi wataridhia uanzishwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa yote hayo yafanywe kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2010.

Mhe. Spika: Kifungu kinakubaliwa?

Mtoa hoja kuna jambo tumeacha?

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, nafikiri yote tuliyoeleza yamo humu, nashukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, nilipokuwa nikiandika *summary*, kuna kitu kimoja muhimu sana nafikiri

mmekisahau kimekupiteni. Kuhusu suala la kurekebisha utaratibu wa kikatiba utakaomuezesha Rais kumdhibiti mjumbe yeyote katika serikali yake atakayeonekana anazorotesha utekelezaji kwa makusudi.

Mhe. Spika: Unataka tui-*frame* namna gani, hebu sema?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Kinasema kwamba uwepo utaratibu wa kikatiba wa kumwezesha Rais kumdhibiti mshiriki yeyote, anayeonekana kwa makusudi anakwamisha uendeshaji bora wa shughuli za serikali shirikishi.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, kwanza katiba inaruhusu hivyo, kwamba Rais amuwajibishe mtu yeyote kwa sababu Rais ndio wa juu.

Pili, makubaliano tuliokubaliana Bagamoyo imo. Sasa mimi sioni haja ya kupinga, mimi nakubaliana nayo, kwa sababu ni kitu kizuri na ni utendaji mzuri *(Makofi).*

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, kwanza naona vibaya kwa haya makofi yaliyopigwa kufanya *interferes*. Lakini unajua wakati mwengine kuuliza ni haki ya mtu. Kwa hivyo naomba univumilie.

Mhe. Spika, ukiangalia katika utaratibu wa katiba Waziri Kiongozi na Rais kuna utaratibu wa *impeachment*. Ukiangalia hata kwenye sheria tulioipitisha juzi DPP na Jaji Mkuu wote kuna taratibu zao za kundolewa katika madaraka. Sasa sijui hizi hazitoshi kwani hata tukaenda huko. Ikiwa kama tu ka-*misbehave*. DPP anapokiuka maadili yake ya kazi, kwa mujibu wa ile sheria tuliyoipitisha juzi, kuna utaratibu unaoandaliwa ambao si rahisi au hauko rahisi sana, lakini ni lazima na taratibu zifanyike. Jaji Mkuu vile vile anapokiuka maadili yake ya kazi kuna utaratibu unaotumika kumuondoa madarakani, Waziri Kiongozi vile vile anapokiuka maadili yake ya kazi Baraza linaweza kumu-*impeach*, lakini nao ule utaratibu hauko kirahisi sana kuweza kum-*impeach* mtu kirahisi. Kwa hivyo, suala hili lilikuwa linanipa hofu kidogo.

Mhe. Spika: Unachosema Mhe. Haji Faki Shaali ni kwamba na huyu Makamo wa Rais aingie kwenye mtiririko huu?

Mhe. Haji Faki Shaali: Hee, mimi nilikuwa nafikiria ule utaratibu wa *impeachment* unaotumika kwa Rais, Waziri Kiongozi na Jaji Mkuu pia ungetumika kwa Makamo wa Rais.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tunakumbuka hiyo kwamba kuna kuweza kum-*impeach* Rais, Baraza ndio kazi yake. Kum-*impeach* Waziri

Kiongozi kama ilivyo sasa ndio kazi yake, ambapo kwa wakati huo maana yake itakuwa Makamo wa pili wa Rais. Kwa hivyo, Mhe. Haji Faki Shaali anachosema na huyu Makamo wa Kwanza wa Rais aingie kwenye mtiririko huo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, tunazungumzia serikali ya aina mpya inayoshirikisha vyama. Sasa hapa tunasema uwepo utaratibu wa kikatiba wa kumuezesha Rais kumdhibiti mshiriki yeyote anayeonekana kwa makusudi anakwamisha utendaji bora wa shughuli za serikali shirikishi. Sasa mimi wasi wasi wangu ni kwamba kama tutakwenda kwenye *impeachment,* litakuwa hilo suala hatukumpa huyo Rais anayeongoza hii serikali.

Kwa hivyo, mimi naona kwamba kwa sababu ni suala ambalo linahusu vyama mbali mbali, inaweza ikatokea mzozo baina ya vyama tusielewane na Rais hana la kufanya, anangoja *impeachment* kutoka Baraza la Wawakilishi au mahala mwengine, itakuwa ngumu. Lakini bora kuwe na utaratibu utakaomuezesha kumdhibiti yeye moja kwa moja. Huo utaratibu tutakubaliana uwe vipi tutakapojadiliana na tutaweka. Mengineyo yatakubaliwa na mengine yatakataliwa, lakini utakuwepo utaratibu maalum ili serikali hii iende kwa utulivu na amani kabisa.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, mimi sioni kama kuna haja ya kugombana, kwa sababu kama nilivyosema Rais ndio kiongozi wa nchi. Rais ana nguvu za aina mbili, ukiacha hilo suala la *impeachment* la Waziri Kiongozi na Rais na tukibadilisha katiba Makamo wa Rais. Lakini bado Rais anao uwezo wa kumuondoa mtu yeyote au kumuweka mtu yeyote. Sasa kwa sababu hiyo hiyo aliyosema Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban na kwa sababu ni mfumo wa Serikali Shirikishi ni lazima kuwe na utaratibu katika katiba wa Rais katika ile kumdhibiti yule Makamo wa Kwanza wa Rais kuwe na utaratibu ili ajuwe kwamba ni hivi. Kwa sababu Rais na yeye vile vile anaweza akasema tu, Mimi namchukia Makamo wa Rais wa Kwanza kwa mambo fulani basi akachukua uamuzi.

Lakini Mhe. Spika, ikiwa kuna utaratibu ambao ndio huo aliosema Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban ni sawa, ni lazima tufuate katiba na huo tutasema ndio uliokubaliwa Bagamoyo na kwenye katiba zimo. Kwa hivyo, mimi sioni kama kuna tatizo, nakubaliana na yeye.

Mhe. Spika: Kwa hivyo, wakati wa marekebisho ya katiba, lifanyike jambo hilo na liingizwe katika marekebisho hayo.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mimi nataka kusaidia tu kidigo. Mhe. Spika, hoja hii inakuja kwa sababu ya wasi wasi kuwa vyama vitakavyokuwa vinafanya kazi kwenye serikali sasa vitakuwa ni tofauti. Tunayo haki ya kuwa na hofu ya aina hii. Lakini mimi sioni msingi mkubwa hata wa kulitumia neno kudhibiti. Kwa sababu watu hawa wakubwa wakishapewa nafasi hizi, wana nguvu kubwa sana katika jamii. Tusiombe Mungu, lakini inapotokea mikwaruzano baina yao nchi inakuwa inatetemeka na inakuwa si rahisi kutumia neno kudhibiti. Kwa sababu tuna-*force conflict* inayoweza kutokea kutingisha watu hawa wawili na nchi, basi huo utaratibu wa katiba uelekezwe zaidi kuwa na Baraza la Usuluhishi ili waendelee kuliko kuweka kudhibiti.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, sikutaka kwenda kwenye *details* hizo, lakini kamati ya Bagamoyo, ilikwenda mpaka ikaanza kufanya *draft* ya hilo Baraza la Usuluhishi litakuwa vipi, na hiyo ilikwenda mpaka Butiama. Kwa hivyo, mimi bado nakubaliana nayo sina matatizo.

Mhe. Haji Omar Kheir: Mhe. Spika, hoja ya Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, mtoa hoja kaikubali. Hivi vijalizo vyengine nafikiri sasa hivi tungeviacha tukabaki na maamuzi ambayo yameshatolewa.

Mhe. Spika: Sasa tunakwenda wapi. Tumeshaimaliza. Kwa hivyo, kuna kitu jambo lile ambalo tunalipeleka kwa wananchi na haya tuliyoyaamua. Ni sawa?

Wajumbe: Ndio.

Mhe. Spika: Kuhusu muundo wa serikali inaingia mle au vipi, ni sawa. Nataka nijiridhishe ni sawa.

Wajumbe: Ndio.

Mhe. Spika: Haya basi. Mimi niwashukuru maana sijui kama kuna haja ya kuuliza, lakini haina haja ya kuuliza kwa jumla, wala haina usomwaji wa mara ya kwanza na ya pili. Kwa hivyo, tumemaliza jambo hili nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, nadhani sasa tunaendelea *(Makofi).*

Katibu: Mhe. Spika, sasa ni Uchaguzi wa Mwenyekiti.

Mhe. Spika: Hebu Katibu ngoja kidogo, nataka kuweka kibwagizo cha mwisho. Waheshimiwa Wajumbe wote mmeshinda *(Makofi).*

Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Baraza

Katibu: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba nimepokea majina mawili ya wanaogombea nafasi hii. Jina moja limetoka upande wa Chama cha Mapinduzi ambaye ni mgombea Mhe. Thuwaybah Edington Kisasi.
Mhe. Spika: Ni yule pale aliyesimama. Haya kaa kitako.

Katibu: Jina la pili ni kutoka upande wa Chama cha CUF ambaye ni mgombea Mhe. Najma Khalfan Juma.

Mhe. Spika: Ni yule pale aliyesimama. Haya kaa kitako.

Haya sasa gaweni karatasi, tunangojea mwenzetu atuite halafu tumalize hii kazi.

Enhe. Vipi kuna taarifa. Ngoja kwanza tumsubiri mwenzetu atowe taarifa. Leo naona imekuwa kidogo tabu. Naomba wajumbe kidogo mubaki, ili nije nihakikishe kama kila mjumbe amepata karatasi ya kura.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa taarifa yangu rasmi. Mimi Najma Khalfan Juma, mgombea wa uenyekiti kutoka katika chama changu cha CUF bila kushawishiwa, ni kwa ridhaa yangu, kwa sababu ya maelewano yaliopo hivi sasa na kwa sababu ya mustakbali na utendaji wa kazi katika Baraza kuleta pamoja naomba kuliondoa jina langu *(Makofi).*

Mhe. Spika: Katibu kanuni zinasemaje.

Katibu: Mhe. Spika, kanuni zinasema, endapo kutakuwa na mgombea mmoja tu kwa hivyo tumpigie kura ya ndio au hapana.

Mhe. Spika: Kwa hivyo, niwaombe kwa kuwa jambo lenyewe limetokea sasa hivi na hatuwezi tukaanza kuleta nyengine muda utakwenda. Kwa hivyo, tukate lile jina la mgombea aliyejitoa, kama mtu atamkubali atamuwekea na kama hakubali basi. Huo ndio utaratibu

Wajumbe: Kura ya kunyanyua mkono.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, naomba turahisishe kazi, wakati mgombea ni mmoja, basi utuulize turidhike tu *(Makofi*).

Katibu: Mhe. Spika, kanuni zinasema uchaguzi wa Mwenyekiti utakuwa ni kwa kura ya siri.

Mhe. Spika: Ndio hiyo. Haya sasa tupige kura kwa jina hilo liliopo, kama tunalikataa, basi itakuwa tupu sawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwa kuwa mwenzetu mmoja keshajitoa kwa kuonesha *solidarity* na hii hali tuliyokuwanayo. Kwa hivyo, na sisi tunaweza kuweka kando kanuni tukasema tuendelee *(Makofi).*

Mhe. Spika: Tuchukulie ametoa hoja. Je, tunaikubali?

Wajumbe: Ndio.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe Spika, suala la uchaguzi ni tofauti na kanuni nyengine zozote. Uchaguzi unasema kura ya siri, hata kama ni mtu mmoja, tupigeni kura ya siri.

Mhe. Spika: Sawa. Kwa hivyo, kwanza wajumbe wote tumepata kura.

Wajumbe: Ndio.

Mhe. Spika: Basi tupige kura. Hebu hilo sanduku la kutilia kura lifunguwe kwanza tuone ndani, hamna humo ndani kitu chochote. Hebu nione. Haya hamna, hebu waoneshe na wajumbe wote.

Sasa wahudumu kusanyeni kura, pitisheni sanduku litiwe kura na wajumbe. Halafu Mhe. Makame Mshimba utakwenda kusimamia uhesabuji wa kura za mheshimiwa mgombea.

Vipi, tayari zimeshakusanywa kura zote, hakuna ambaye hajakusanya. Sasa Waheshimiwa Wajumbe zoezi hili linamalizika mara baada ya kuja kutangaza matokeo.

Tukubaliane kwamba shughuli yetu hii leo inaweza ikaenda mbele kidogo kwa ridhaa yenu baadae. Sasa tuwape nafasi watendaji wakahesabu kura na tukubaliane tukasali mpaka kwenye saa 1:15 tutarudi hapa. Kwa hivyo, naahirisha kikao hiki kwa muda mfupi hadi saa 1: 15 usiku huu.

(Saa 1:00 usiku Baraza liliahirishwa hadi saa 1:15 usiku)

(Saa 1:15 usiku Baraza lilirudia)

MATOKEO YA KURA YA MWENYEKITI

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nimepata taarifa ya matokeo ya kura tuliyopiga hivi punde kiasi ya robo saa iliyopita. Kwa kweli kazi haikuwa ndogo ilikuwa ngumu na Makatibu walifanyakazi kubwa chini ya ulinzi mkali wa kwa ajili ya kazi ya kuhesabu kura. *(Kicheko/Makofi)*

Nashukuru nimepewa taarifa kwamba kazi ya kuhesabu kura ilikwenda vizuri na yule aliyekwenda kusimamia uhesabuji wa kura za Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi, amethibitisha kwamba kazi ya kuhesabu kura imekwenda vizuri na wala hakukuwa na tatizo lolote pamoja na uzito wa kazi iliyofanyika huko. *(Makofi)*

Kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe nyote kwa kutumia haki yenu ya kupiga kura, kwa ajili ya kumchagua Mwenyekiti kama yalivyo marekebisho tuliyoyafanya mkutano uliopita. *(Makofi)*

Pili niwashukuru watendaji wangu kwa matayarisho haya pia niwashukuru sana kwa kufanyakazi hii ya kuhesabu kura kwa uadilifu mkubwa.

Nadhani tumtafute Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi.

Kwa kweli kazi imefanyika kwa uadilifu mkubwa bila ya tatizo lolote na sijui kutokuwepo kwake ameona hali ilikuwa ngumu, ndio ameona akajificha pahala, lakini tayari ameshaletwa yule pale. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hivyo, matokeo ya kura yalikuwa kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wajumbe wote waliopiga kura idadi yao ni 75,
Kura zilioharibika ni 6,
Kura ambazo zimemkataa mgombea asiwe Mwenyekiti wa Baraza hili ni 4 na
Kura ambazo zimemkubali na kumchagua Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi ni 65. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, natangaza rasmi kwamba Mhe. Thuwayba Edington Kissasi amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza hili la Wawakilishi. *(Makofi)*

Nadhani asubiri kidogo baadaye nitampa nafasi.
Lakini nichukue nafasi hii kwa uzalendo mkubwa na kwa maridhiano makubwa aliyoonesha mgombea mwengine, ambaye kabla ya hapo ni mmoja kati ya mtiririko wa wagombea Mhe. Najma Khalfan Juma. Kwa kweli kitendo chake cha kuamua kujiondoa, ili amuachie mgombea mwenzake ni kitendo cha

uzalendo. Vile vile amenieleza kwamba hiyo ni muhanga wa maridhiano ambayo tuliyofanya hapa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nichukue nafasi hii kumshukuru sana kwa kitendo hicho cha kuonesha maridhiano kwa vitendo hapa katika ukumbi wetu wa Baraza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana kwa kazi nzuri hiyo mliyoifanya. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi (Mwenyekiti mpya) unayo amelezo yoyote.

Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii kwa ajili ya kutoa shukurani zangu za dhati, kutoka sakafu ya moyo wangu kwa mashirikiano yaliyooneshwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kweli nimeemewa nataka nikubaliana na wewe kwamba hiki kitendo kilichotokea hapa leo, ndio mfano halisi wa mashirikiano ambayo tunatarajia tutakuwa nayo mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2010, yaani hapa tumeona mfano wake. Kwa hivyo, Inshaallah Mwenyezi Mungu atufikishe na huko tuweze kuwa na haya na zaidi ya haya. *(Makofi)*

Namshukuru sana mgombea mwenzangu kwa kuonesha mfano wa kunipatia nafasi. Kwa kweli nimuahidi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote kwamba nitayaenzi mashirikiano haya, nitawaheshimu pamoja na kuomba mashirikiano yao ya dhati katika kufanikisha kazi hii mpya, ambayo naamini Baraza lako tukufu limeniamini mimi kunipatia nafasi hii Mhe. Spika.

Vile vile mpambe wangu naye nimshukuru sana kwa kuwa muaminifu kwangu na kwenda kuzihesabu kura zangu naamini kwamba amejitolea. Pamoja na hayo hahitaji chochote kutoka kwangu kwa ajili ya malipo Mhe. Spika. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amenituma niseme kwamba msaada wake ulikuwa wa bure. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Najma Khalfan Juma unayo maneno yoyote ambayo unataka kusema.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Mhe. Spika, ahsante sana nami lazima nilishukuru Baraza la Wawakilishi kwa kufanya mabadiliko ya Kanuni na

kuona kwamba wanawake tunayo haja ya kuingia sehemu za juu kama hizi. Kwa kweli hicho ndicho kitu kikubwa ambacho tunakililia kila siku.

Mhe. Spika, kama Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi ni mwanamme, basi nisingeondoa jina langu. Lakini kwa vile yeye ni mwanamke mwenzangu na ninajua pale tunachokigombania ni mambo mazuri kwa wanawake sote Watanzania au wa Zanzibar kwa jumla, basi sikuwa na haja ya kupingana na mwanamke mwenzangu ambaye anakwenda pale kutekeleza yale yale ambayo mimi vilevile ningeyatekeleza au tunayalilia kwa pamoja kupata zile haki kama wanavyopata wenzetu wanaume.

Kwa hivyo mimi ninalihakikisha Baraza hili kwamba nitatoa ushirikiano wa dhati kwa Mhe. Thuwayba na Wajumbe wote wa Baraza. Vile vile kujitoa kwangu kumeonesha yale maridhiano tunayofikia sasa hivi Zanzibar tunayoyata, hivyo hakuja haja ya kukaa watu wawili ambao sote tunataka maridhiano ya pamoja ya Wazanzibari tukavutana.

Kwa hivyo mimi nimempa ridhaa yeye agombee peke yake kwa kuleta ule umoja na mshikamano, maelewano na mapenzi kwa Wazanzibari wote.

Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ninashukuru ahante sana Mhe. Najma. Mhe. Thuwaiba karibu katika kazi yako hii mpya ulioongezewa na ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe mushirikiane sana naye katika kazi hiyo. Ahsante sana.

KUONGEZWA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi naomba kutoa hoja kwamba tuzidishe muda wetu mpaka Mhe. Waziri Kiongozi aweze kumaliza kutoa hotuba yake.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KUAHIRISHWA BARAZA

Mhe. Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kuendesha shughuli za Baraza lako tukufu kwa

ufanisi mkubwa. Pili, nakushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kuongoza mkutano huu kwa hekma na busara. Halikadhalika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wawakilishi kwa kuuliza maswali mazuri kuhusu utendaji wa shughuli za Serikali na kujadili hoja mbali mbali zilizowasilishwa katika mkutano huu. Mwisho, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kuyajibu vizuri maswali yote yalioulizwa na kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali.

Katika mkutano huu jumla ya maswali 66 yaliulizwa na kujibiwa na Waheshimiwa Mawaziri. Vile vile mkutano huu ulijadili na kuipitisha miswada miwili ya sheria:-

1. Mswada wa Sheria ya Kurekebisha sheria ya Tume ya Utangazaji.
2. Mswada wa sheria ya kuweka Masharti ya Uanzishaji na Uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Baraza lako Tukufu pia lilijadili na kupitisha Sera ya Nishati na Hoja Binafsi kuhusu kuanzishwa kwa mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kufanyika Uchaguzi wa Mwenyekiti.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Tume ya Utangazaji Nam.7 ya 1997 una shabaha ya kurekebisha sheria hiyo ili iweze kukidhi mabadiliko ya mfumo wa utangazaji kutoka mfumo wa "*analogue*" kwenda kwenye matumizi ya mfumo wa "*digital*". Wataalamu wa utangazaji na mawasiliano ya umma wanatueleza kuwa mfumo wa utangazaji wa "*digital*" una faida kubwa kwa wananchi. Vyombo vya habari vinavyotumia mfumo wa utangazaji wa "*digital*" vinawawezesha wananchi kupata matangazo yenye picha na sauti nzuri zaidi.

Mhe. Spika**,** wakati tulipokuwa tukifanya marekebisho ya sheria ya Tume ya Utangazaji ya mwaka 1997 tuliuzingatia sana ushauri tuliopewa na Waheshimiwa Wawakilishi. Baadhi ya Wajumbe walipendekeza kuwa Bodi ya Utangazaji iwe na wajumbe wachache ili iweze kupunguza gharama za uendeshaji na kuharakisha utoaji wa maamuzi. Vile vile Wajumbe walimshauri Waziri wa Habari azingatie ujuzi na utaalamu anapoteua wajumbe wa Bodi ya Utangazaji ili kuongeza ufanisi. Halikadhalika, wajumbe waliishauri Wizara ya Habari kupunguza masharti ya kutoa leseni ya kuanzisha vyombo vya habari ili kuwawezesha wawekezaji wazalendo kumiliki vyombo vya habari. Wajumbe waliiomba Wizara iweke utaratibu wa kuwaruhusu wananchi wamiliki vyombo vya habari kwa ubia hasa tukizingatia kuwa Wazanzibari wengi hawana mitaji ya kutosha. Uamuzi huu utawasaidia wamiliki wa vyombo vya habari wa Zanzibar kukabiliana na ushindani dhidi ya wageni kutoka nje ya Zanzibar.

Mhe. Spika**,** Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka una lengo la kuimarisha utendaji wa Afisi hii katika usimamizi wa kesi za jinai. Tangu Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ilipoanzishwa mwaka 2002 imekuwa ikitekeleza majukumu yake ipasavyo chini ya kifungu cha 56 (a) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 na Sheria ya Mwenendo wa Jinai Nam. 7 ya mwaka 2004. Lakini kutokana na kuongezeka kwa majukumu ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, imeonekana kuwa kuna umuhimu wa kuunda afisi hii kisheria ili kuiongezea uwezo wa kusimamia upelelezi wa makosa ya jinai.

Mhe. Spika, tangu Afisi hii ilipoanzishwa imekuwa ikijitahidi sana kuajiri wafanyakazi wenye utaalamu na ujuzi katika masuala ya sheria ili kuimarisha utendaji wa kazi. Hivi sasa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ina wafanyakazi wenye ujuzi wapatao 32. Vile vile Afisi hii imeweza kuwapatia mafunzo mbali mbali wafanyakazi katika Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai kuhusu Rwanda mjini Arusha, Mahakama za Tanzania Bara na kuwapeleka nje ya nchi baadhi ya wafanyakazi ili kujifunza masuala yanayohusu sheria za mikataba ya uchimbaji wa mafuta.

Mhe. Spika**,** Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imefanya mageuzi makubwa sana katika usimamizi wa mashtaka na mwenendo wa kesi za jinai hapa Zanzibar. Kama mnavyoelewa hapo awali upelelezi wa kesi zote za jinai ulikuwa ukifanywa na Jeshi la Polisi kuanzia kukamata wahalifu, uendeshaji wa kesi hadi kuwatia hatiani wahalifu. Mfumo huu ulisababisha mrundikano wa kesi nyingi katika Mahakama zetu na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi. Ndio maana Serikali yenu ikaipa majukumu Afisi hii ya kuendesha upelelezi wa kesi za jinai ili kupunguza mrundikano huo wa kesi Mahakamani

Mhe. Spika, ili Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iweze kufanyakazi kwa ufanisi, naiomba Afisi hii ikiimarishe Kitengo cha Sera na Utafiti ili kusimamia utekelezaji wa majukumu yake kwa ukamilifu zaidi. Serikali ya Mapinduzi kwa kushirikiana na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Washirika wengine wa maendeleo, kama vile Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia makosa ya jinai na madawa ya kulevya, zina mpango wa kuanzisha kitengo maalum kitakachosaidia uendeshaji wa kesi za jinai kwa kutumia nyenzo za kisasa katika uchunguzi na utoaji wa ushahidi.

Mhe. Spika**,** Baraza lako tukufu pia limepata wasaa wa kujadili Sera ya Nishati ya Zanzibar. Sera hii ina lengo la kuweka mwongozo wa kuiendeleza sekta ya nishati ili kuwawezesha wananchi kupata nishati endelevu. Sera ya nishati ya Zanzibar inaainisha majukumu ya Serikali na sekta binafsi katika kutafuta vyanzo mbadala vya nishati ili Zanzibar iweze kujitegemea kwa vyanzo hivyo vya nishati. Suala hili litawasaidia sana wananchi kupata nishati ya uhakika na

kwa bei nafuu kwa ajili ya matumizi ya majumbani na shughuli za maendeleo kwa ujumla.

Mhe. Spika, kama mnavyoelewa mahitaji ya nishati yanaongezeka kila kukicha. Kutokana na mahitaji makubwa ya nishati wananchi wanalazimika kukata miti kwa wingi kwa ajili ya kupata kuni za kupikia. Hali hii inasababisha uharibifu mkubwa wa mazingira. Ili kuidhibiti hali hii Serikali inatafuta vyanzo mbadala vya nishati, kuanzia majenereta ya akiba, umeme wa upepo na jua na nguvu za nyuklia. Serikali yenu tayari imewasiliana na washirika wa maendeleo kuwaomba msaada wa ununuzi wa majenereta ya umeme wa akiba.

Mhe. ninapenda kuwapa taarifa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, washirika wa maendeleo wamekubali kutusaidia. Washirika hao ni kama ifuatavyo, Shirika la Maendeleo la Sweden, Norway na Shirika la Maendeleo la Uingereza. (*Makofi*).

Mhe. Spika**,** katika hotuba yangu ya kufunga mkutano wa kumi na saba wa Baraza la Wawakilishi nilielezea kuhusu masuala mbali mbali ya mazingira na matarajio ya Tanzania katika mkutano wa mabadiliko ya hali ya hewa duniani uliofanyika Denmark Disemba, 2009.

Mkutano huu ulifanyika kama ulivyopangwa ingawa kwa bahati mbaya haukuweza kufikia matarajio ya nchi zinazoendelea. Mataifa yaliyoendelea kiviwanda kama vile Marekani, China, Ujerumani hayakuwa tayari kupunguza uzalishaji wa gesi chafu. Nchi hizi zimelaumiwa sana kwa kukataa kupunguza uzalishaji wa gesi chafu kwa asilimia 4. Pengine mkutano huu haukuweza kufikia matarajio kwa sababu nchi zinazoendelea hazikuwa na sauti moja katika kutetea msimamo wao huo. Nchi za Brazil, India na Afrika ya Kusini ziligawanyika na hatimaye kulegeza masharti waliyojiwekea awali na kusababisha msimamo wao kuyumba.

Mhe. Spika**,** katika jitihada za kupoza hasira za nchi zinazoendelea, mataifa yenye viwanda yametoa ahadi ya msaada wa dola bilioni 30 kati ya mwaka 2010 na 2012 kwa madhumuni ya kuzisaidia nchi masikini kukabiliana na majanga yanayotokana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani. Halikadhalika, mataifa makubwa yameahidi kuzisaidia nchi maskini kuendeleza misitu, kilimo na elimu kwa ajili ya utunzaji wa mazingira.

Mhe. Spika**,** hapana shaka uchafuzi wa mazingira unaotokana na uzalishaji wa hewa chafu unasababisha kuongezeka kwa joto duniani. Hali hii inasababisha kuyeyuka kwa barafu ambayo hatimaye inasababisha kupanda kwa kina cha maji ya bahari. Kupanda kwa kina cha bahari kuna athari kubwa kwa nchi za visiwa kama tulivyo sisi Zanzibar. Nina hakika tunapotembelea maeneo yaliyo

karibu na bahari tunaona jinsi maji ya bahari yanavyosababisha mmong'onyoko wa ardhi. Ili kukabiliana na janga hili wataalamu wanatushauri tupande miti angalau isiyopungua 500,000 kila mwaka kwa ajili ya kufyonza hewa chafu na kutupatia kuni.

Mhe. Spika**,** pamoja na juhudi mbali mbali tunazozichukua katika kuwahimiza wananchi kudumisha usafi wa mazingira, bado utupaji taka ovyo unaendelea kwa kasi ya kutisha. Mifuko ya plastiki na takataka nyengine za majumbani zimeenea katika mitaa na kwenye mitaro ya maji machafu. Hali inazidi kuwa mbaya kwa sababu baadhi ya Halmashauri za Wilaya zinaanzisha majaa mitaani. Vile vile baadhi ya watu wanachukua takatakaza majumbani kwa ajili ya kuzisambaza katika mashamba yao. Tabia hii ya kutumia takataka za majumbani kama mbolea inahatarisha afya kwa sababu baadhi ya takataka zina sumu. Iwapo takataka zenye sumu zitatumiwa kama mbolea, sumu iliyo katika mbolea hiyo itaishia katika mboga mboga na matunda tunayoyatumia kama chakula. Jambo hili ni hatari sana kwa afya zetu.

Mhe. Spika**,** ili kuimarisha usafi wa mazingira Idara ya Mazingira inapaswa kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa usafi. Halikadhalika, Idara hiyo inatakiwa isimamie marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki. Nalisema jambo hili kwa sababu nimebaini bado mifuko ya plastiki inatumika licha ya kuipiga marufuku. Nayaomba Mabaraza ya Miji pamoja na Halmashauri za Wilaya zihakikishe zinatenga maeneo ya mbali ya kutupia taka. Halmashauri za Wilaya ziweke vifaa vya kutupia taka katika mitaa ili kuzuia takataka zisitupwe ovyo kwenye makaazi ya wananchi.

Mhe. Spika**,** hivi sasa imebaki miezi 9 kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu mwaka huu. Kwa hiyo ipo haja ya kutathmini utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Serikali ya Mapinduzi chini ya uongozi wa Mhe. Dk. Amani Karume imetekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005-2010 kwa zaidi ya kiwango cha asilimia 90 hivi sasa. Utawala wa Rais Karume umeweza kujenga misingi imara ya uchumi na ustawi wa jamii. Ili kufikia lengo hilo Serikali inajitahidi kuimarisha miundombinu ya kiuchumi na huduma za jamii kwa ujumla.

Mhe. Spika, katika kuimarisha jitahada za kuwapunguzia wananchi umasikini, mfuko wa kuwawezesha wananchi (mfuko wa JK na AK) umetenga fedha zipatazo shilingi 3.6 bilioni ili kuwakopesha wafanya biashara wadogo wadogo waweze kukuza biashara zao. Hadi kufikia mwezi Novemba, 2009, jumla ya shilingi 952.9 milioni zimetolewa Unguja na Pemba kwa vyama vya *SACCOS* na watu binafsi.

Mhe. Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) nao unatoa mchango

mkubwa sana katika kuwapunguzia wananchi matatizo ya umaskini. Mwaka uliopita jumla ya miradi 307 ilitekelezwa. Miradi hii yenye thamani ya shilingi bilioni 3.8 inajumuisha miradi ya maji safi, elimu, kilimo, mifugo, uvuvi, ushonaji na ufumaji, ufugaji nyuki, uhifadhi wa mazingira na elimu ya UKIMWI.

Mhe. Spika, mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani (*MACEMP*) umewasaidia sana wananchi wanaoishi kwenye vijiji vilivyo karibu na bahari kutekeleza miradi ya hifadhi ya mazingira ya bahari. Serikali yenu kupitia Wizara ya Kilimo kwa mwaka uliopita imetekeleza jumla ya miradi 251 yenye thamani ya shilingi bilioni 4. Kati ya hiyo miradi 114 yenye thamani ya shilingi bilioni 2 inatekelezwa Unguja na miradi 137 yenye thamani ya shilingi bilioni 2 inatekelezwa Pemba.

Mhe. Spika, uzoefu unaonyesha kwamba nchi haiwezi kujenga uchumi wa kisiasa iwapo haitawekeza katika sekta za miundombinu na huduma za jamii. Kwa kutambua ukweli huo Serikali ya Rais Karume imekuwa ikitilia mkazo mkubwa sana uwekezaji katika sekta hizi ili kuvutia uwekezaji mitaji na miradi ya biashara. Nitaeleza mafanikio ya kila sekta kwa kifupi.

Mhe. Spika**,** sekta ya Kilimo ina umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya nchi. Ili tuweze kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo, Serikali yenu inawekeza katika kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji na kuwapatia wakulima mbegu zilizo bora. Vile vile, Serikali inawapatia wakulima mafunzo kuhusu mbinu bora za ukulima wa mpunga na mbogamboga ili kuongeza tija na uzalishaji.

Mhe. Spika, Serikali yenu inaendelea kuvitangaza vivutio vya utalii vya Zanzibar ili kuongeza idadi ya watalii. Katika jitihada za kuimarisha shughuli za utalii, Chuo cha Maendeleo ya Utalii – Maruhubi kilisajili wanafunzi 541 kwa 2008/2009 katika fani mbali mbali. Katika kipindi hicho wanafunzi 532 walihitimu masomo yao katika ngazi ya cheti na Diploma. Chuo cha Maendeleo ya Utalii kinaendelea kuimarisha mitaala yake ili kunyanyua kiwango cha elimu.

Mhe. Spika, maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii yanategemea sana ubora wa miundombinu ya barabara, bandari na viwanja vya ndege. Serikali yenu imekamilisha kuandaa Sera ya Taifa ya Usafiri na Mpango Mkuu wa Usafiri ili kuimarisha mtandao wa miundombinu. Serikali imeweza kukamilisha ujenzi wa barabara mbali mbali. Kwa upande wa Unguja Serikali imejenga kwa lami barabara za Mshelishelini - Pwanimchangani, Mazizini – Fumba na Mtoni – Mwanyanya. Barabara za Amani – Dunga ujenzi wake hivi sasa unaendelea. Kwa upande wa Pemba Serikali imekamilisha ujenzi wa barabara za Mkoani – Makombeni na Mtemani – Kizimbani. Vile vile Serikali inaendelea na ujenzi wa barabara za Wete – Chake-Chake, Wete – Konde, Wete – Gando na Mgagadu –

Kiwani.

Mhe. Spika**,** Serikali pia imetangaza tenda za kupata mkandarasi wa ujenzi wa barabara za Ole – Kengeja. Barabara za vijijini za Mkoa wa Kaskazini Pemba zinafanyiwa kazi za usanifu. Barabara hizi ni Bahanasa - Daya - Mtambwe, Kipangani – Kangagani, Mzambarau karimu – Mapofu, Chwale – Kojani na Mzambarautakao – Pandani – Finya. Barabara hizi zinatarajiwa kujengwa kwa ufadhili wa Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Changamoto za Milenia.

Mhe. Spika, kama mnavyoelewa ujenzi wa bandari ya Malindi ulikamilika tangu mwaka juzi. Hivi sasa bandari ya Malindi inafanyakazi kwa ufanisi baada ya Shirika la Bandari kununua vifaa vya kuteremshia na kupakia mizigo. Vile vile Serikali yenu inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya kurukia na kutulia ndege katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Zanzibar ili kuongeza urefu kutoka mita 2,462 hadi mita 3,022. Mradi huu umeanza na unatarajiwa kukamilika mnamo mwezi wa Agosti, 2010.

Mhe. Spika, Serikali yenu inaendelea kuimarisha mazingira ya elimu ili kunyanyua kiwango cha elimu. Katika kipindi cha mwaka 2009 jumla ya madarasa mapya 229 yamejengwa katika skuli za msingi. Serikali imekamilisha utengenezaji wa mitaala mipya ya elimu ya msingi inayotarajiwa kuanza kutumiwa mwaka huu. Ili kuongeza fursa za elimu ya Sekondari, Wizara ya Elimu imetia saini mkataba wa ujenzi wa skuli za sekondari katika Wilaya zote Unguja na Pemba. Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imenunua vitabu vya masomo ya kemia, fizikia na hesabati kwa madarasa ya kidato cha kwanza hadi cha sita na kusambazwa katika skuli zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kutokana na juhudi mbali mbali zinazochukuliwa na Serikali, idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu vya Zanzibar imeongezeka. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar hivi sasa kina wanafunzi wapatao 703. Katika Chuo Kikuu cha Zanzibar kuna wanafunzi 1,727 wa masomo ya shahada ya kwanza. Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Chukwani kimesajili wanafunzi wapatao 725. Serikali yenu inaendelea kugharamia masomo ya wanafunzi wa vyuo vikuu kwa kupitia mfuko wake wa Elimu ya Juu. Hadi kufikia mwaka 2009 Serikali iliwadhamini wanafunzi wapatao 710 wanaosoma vyuo vikuu viliopo Tanzania Bara na nje ya Tanzania. Idadi hii ya wanafunzi wanaogharimiwa na Mfuko wa Elimu ya Juu mwaka 2009 ni kubwa ikilinganishwa na ile ya mwaka 2008 ambapo jumla ya wanafunzi 474 ndio waliogharamiwa masomo yao.

Mhe. Spika**,** sekta ya afya ni moja ya sekta zilizopewa umuhimu mkubwa sana katika dira ya maendeleo ya 2020 na mpango wa kupunguza umaskini. Katika kipindi cha 2009/2010, Serikali imepata vifaa vya kisasa vya huduma ya macho

kutoka Serikali ya Jamhuri wa Watu wa China kwa ajili ya Hospitali ya Mnazimmoja. Vile vile Serikali imenunua mitambo ya kisasa ya kupiga picha za *X-ray* na *CT-Scan* ili kurahisisha uchunguzi wa maradhi na kuwapunguzia usumbufu wagonjwa waliokuwa wanafuatilia huduma hizi Tanzania Bara.

Mhe. Spika, katika jitihada za kupunguza ugonjwa wa malaria hapa Zanzibar, Serikali yenu inaendelea na zoezi la upigaji dawa majumbani kwa awamu ya nne. Jumla ya kaya 199,837 kati ya kaya 213,531 zilipigwa dawa kwa kipindi cha Novemba, 2008 hadi Januari, 2009. Serikali imegawa vyandarua 643,000 kwa wajawazito na watoto ili kujikinga na ugonjwa wa malaria.
Mhe. Spika, kama mnavyojua UKIMWI bado unaendelea kuleta maafa makubwa sana kwa wananchi wetu. Ili kukabiliana na ugonjwa huu Serikali inatoa elimu ya kujikinga na maambukizi mapya na kutoa huduma kwa watu walioathirika na ugonjwa huo. Huduma za kuwapatia waathirika wa UKIMWI dawa za kurefusha maisha zinaendelea kutolewa. Mpaka kufikia mwezi Septemba, 2009 jumla ya wagonjwa 1,794 wamepatiwa dawa za kurefusha maisha. Natoa wito kwa wananchi wazitumie vizuri huduma hizo ambazo hupatikana bila ya malipo. Pia tujenge upendo kwa wenzetu ambao kwa bahati mbaya wamefikwa na janga hili.

Mhe. Spika, Serikali yenu inaendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa maji katika Manispaa ya Zanzibar. Mradi huu una lengo la kujenga matangi mawili katika maeneo ya Dole na Kinuni. Tangi la Kinuni litakuwa na uwezo wa kuchukua lita 2,700,000 na tangi la Dole litakuwa na uwezo wa kuchukua lita 1,200,000. Ujenzi wa matangi haya unakwenda sambamba na ulazaji wa mabomba mapya yenye urefu wa kilomita 21.3 pamoja na uchimbaji wa visima vitano katika maeneo ya Kizimbani na Kimara. Mradi huu utakapokamilika hapana shaka yoyote utawanufaisha wananchi wapatao 460,000 wa Mkoa wa Mjini/Magharibi.

Mhe. Spika, huduma ya nishati zina umuhimu mkubwa katika kukuza maendeleo ya nchi. Ili kuwapatia wananchi huduma bora za nishati, Serikali yenu inatekeleza mradi wa kupeleka umeme Pemba kutoka Tanga. Mnamo tarehe 04 Disemba, 2009 Rais Karume alizindua mradi huo kule Tanga na tarehe 15/12/2009 alishuhudia zoezi la kuufikisha waya wa umeme Pemba. Kwa ujumla kazi za upelekaji waya wa umeme Pemba inaendelea vizuri sana na tunatarajia kuwa majaribio ya awali yanatarajiwa kufanywa Machi, 2010. Vile vile, Serikali inaendelea na maandalizi ya kutekeleza mradi wa uwekaji waya mpya wa umeme Unguja kwa ufadhili wa Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Changamoto za Milenia. Mradi huu unatarajiwa kugharimu kiasi cha dola za Kimarekani milioni 63.2. Mradi huu utaongeza kiwango cha umeme kwa Kisiwa cha Unguja kutoka Megawati 45 hadi za sasa hadi Megawati 100.

Mhe. Spika, Baraza lako tukufu lilipata nafasi ya kujadili Hoja Binafsi kuhusu uanzishwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wawakilishi kwa umakini wao katika kujadili hoja hii nzito inayobeba hisia za Wazanzibari na Watanzania kwa jumla. Kila mjumbe Mhe. Spika, aliyesimama alitoa mchango mzito kwa ufundi na uhodari mkubwa. Hapana shaka yo yote kuwasilishwa kwa hoja hii katika Baraza lako tukufu kunafungua mwanga wa matumaini katika kuijenga Zanzibar mpya. Hili ni tokeo la kihistoria ambalo sisi kama Wajumbe wa Baraza hili hatupaswi kulisahau katika maisha yetu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, hapana shaka hali ya utulivu tunayoishuhudia sasa ni matokeo ya maridhiano yaliyofikiwa kati ya Rais Karume na Maalim Seif Sharif Hamad Katibu wa Chama cha CUF hivi karibuni. Namshukuru sana Rais Karume, ninamshukuru Maalim Seif kwa hatua walizozichukua za kizalendo na kijasiri.

Mhe. Spika, kiongozi aliyemakini na anayewapenda watu wake na kuwajali atafanya kama alivyofanya Rais Karume. Najua wapo watu watakaotilia shaka jambo hili lakini mwisho wake sote tukubali kuwa maridhiano ya kutafuta amani na usalama ni jambo jema. Kama yupo mtu au kiongozi anahisi anayo njia sahihi zaidi ya kuleta amani na umoja zaidi kuliko hii, basi anaweza kuipendekeza na sisi tutaitafakari na kuifanyia kazi. Lakini kwa sasa tuamini kwamba njia hii ndio sahihi. Safari yetu ni moja lakini njia za kutufikisha tunakokwenda zinaweza kuwa ni nyingi. Mimi Shamsi Nahodha nikiwa ndani ya Serikali au nje ya Serikali nitamsaidia kiongozi ye yote atakayekuwa na dhamana ya kutuongoza kudumisha amani na umoja wa taifa letu. Nifatanya hivyo kwa sababu siku zote ninaamini "Umoja ni nguvu na utengano ni Udhaifu". (*Makofi*).

Mhe**.** Spika, sote tunaelewa umuhimu wa umoja na amani katika maendeleo ya taifa. Sijui nchi ambayo imedumisha amani na umoja ikiwa dhalili, siijui. Lakini mifano ya nchi ambazo zimeshindwa kudumisha amani zikapata matatizo ninazijua.

Mhe. Spika, ipo nchi moja Waingereza wanaita Lebanon, sisi Waswahili tunaita Lebanoni, ilikuwa ni nchi ya mfano katika Mashariki ya Kati. Leo ukenda ni magofu matupu. Zimbabwe ilikuwa inaongoza kwa uzalishaji wa chakula katika nchi za *SADC*, leo ukenda utaona huruma. Yaliyotokea Kenya sote tunayafahamu kwa sababu ndio mfano ulio karibu yetu. Yaliyotokea Rwanda tunayafahamu kwa sababu ni mfano ulio katika karibu yetu.

Ninamshukuru Rais Karume, ninampongeza Maalim Seif kwa hatua waliyoichukua, kwa nini? Hatua ya kudumisha amani na umoja Zanzibar ni jambo ambalo limehimizwa katika mafunzo ya dini. Mwenyezi Mungu anasema katika kitabu chake kitukufu, "Shikamaneni na musifarikiane". Lakini wenzetu

katika Biblia wanasema, “Wamebarikiwa wale wanaopigania amani kwa sababu wao wanaorithi ulimwengu”.

Sera za Chama cha Mapinduzi zinasisitiza juu ya umoja, maelewano na maendeleo ya taifa letu. Ilani ya uchaguzi wa mwaka 2005 inatuhimiza hivyo hivyo kuwaunganisha Wazanzibari ili kuleta maendeleo ya nchi yao.

Mhe. Spika, juhudi za kutafuta maelewano ya Zanzibar zimeanza miaka mingi sana na mimi binafsi nilitarajia kwamba hali tunayoiona leo, nilitamani sana ingetokea kabla ya mwaka 2005. Lakini sisikitiki sana kwa sababu kila jambo na wakati wake. Mwanafasihi mmoja maarufu wa kale wa Uingereza – Shakespeare aliwahi kusema maneno yafuatayo na naomba uniruhusu niseme katika lugha yake ya asili.

There is a time to love and time to hate but the time to love has come and defenitely to Zanzibar. Shakespeare anasema katika maisha kuna wakati ya watu kuchukiana lakini kuna wakati watu wa kupendana na kwa mawazo yake anahisi wakati wa watu kupendana umefika. Mimi nimeongeza kuweka mkazo kwa Zanzibar ya leo. Iko kauli moja ya Kiingereza inayosema, *“Great Thinkers think alike”.* Watu wanafalsafa, ni watu wenye mawazo mapana wana fikra zenye kufanana na nitawataja.

Watu waliosaidia kuizungumza hali ya Zanzibar wakati ule ambapo ilikuwa mtu inahitaji kuwa na unajisiri wa wendawazimu na akathubutu kusema hadharani kwamba Zanzibar kuna tatizo. Maana kuna wakati tulifika tatizo lipo lakini kila mmoja anazungumzia ndani ya chumba, hawezi akakaa hadharani kuna tatizo. Ndio maana nikasema ilihitaji ujasiri wa kienda wazimu. Lakini kuna watu walithubutu kusema hadharani kuwa kuna tatizo. Niwataja wanafalsafa sita.

Lakini hapa hakuna mzungu hata mmoja wote ni Watanzania na kwa bahati nzuri Wazanzibari wapo. Mwaka 1995 Marehemu Mwalimu Nyeree aliyoyasema munayajua baada ya uchaguzi mkuu. Akasema Zanzibar kwa hali yake mukenda hivi mutapata matatizo. Mwaka 2000 Dk. Karume alipokuwa anaomba ridhaa ya kuchaguliwa kuwa Rais wetu, akasema ninatamani sana nikipata nafasi ya kuwa Rais wetu, ninataka kujenga Zanzibar mpya, na sishangai kuyafanya haya anayoyafanya sasa hivi. (*Makofi*).

Mwana falsafa wa tatu mwaka 2003, Rais Benjamin Mkapa alisema anasononeka sana na hali ya Zanzibar, alisema anakosa usingizi. Mwanafalsafa wa nne ni mwaka 2005 Dk. Jakaya Kikwete alisema hali ya Zanzibar inamsikitisha sana.

Juni mwaka 2009 mwanafalsafa Abass Muhunzi aliyoyasema, alisema kutokumtambua Rais ni mbwembwe za kisiasa, ninamuomba Maalim Seif aende Ikulu. (Makofi).

Mwanafalsafa wa sita. Novemba, 2009 Dk. Karume na Maalum Seif wamefanya hatua hii tunayoiona.

Ndugu zangu viongozi, ndugu zangu Wazanzibari. Zanzibar ni kama jahazi kubwa linalotarajiwa kutuvusha ng'ambu ya pili na sisi Wazanzibari wote ni abiria wake. tukigombanagombana ndani ya jahazi hilo, tukifanya vurugu litazama, likizama sote na watoto wetu tutaangamia. Lakini tukifanya kinyume chake, tukielewana, tukisaidiana, tukishauriana tutafika ng'ambu ya pili salama na sote tutakuwa washindi na watoto wetu. Sasa uchaguzi ni wetu.

Ndugu zangu viongozi hapa tulipofika naomba sana tusirudi nyuma, wananchi wetu wamechoka. Lakini ninajua kazi ya kujenga moyo wa kuaminiana si kazi rahisi sana kwa sababu tunakotoka mnakujua. Mtu ambaye jana ungesema akatwe ngeu lakini leo asubuhi unasema unambusu kwa kumpenda, inakuwa vigumu sana kwa kuaminiana.

Sasa katika hali ya namna hiyo tunahitaji sasa maridhiano haya kuyalea na kuyaengaenga, tutayaengaenga vipi? Nawaomba sana wenzangu viongozi wa kisiasa tujizuie sana na kauli. Tuzuie sana ulimi wetu kwa sababu ulimi na ninafikiri ndio maana Mwenyezi Mungu ulimi ameufanya mdogo sana, ninajiuliza angeufanya ukawa mkubwa kama mguu ungekuwaje. (*Kicheko*).

Ninashauri tuutumie ulimi kwa hekma, tuache kauli za kuwachonganisha wananchi, tukifanya hivyo watajenga matumaini. Sisi hapa tumezungumzia juu ya haja ya kuwapelekea wananchi wafanye kura za maoni ili waidhinishe suala la kuundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mimi ndugu zangu ninaamini katika maisha kila jambo linawezekana, lakini nini tatizo. Tatizo langu kubwa ninasema wananchi hawana matatizo, wenye matatizo ni viongozi. (*Makofi*).

Viongozi tukidhamiria ndani ya dhati ya moyo wetu, tukiliamini hili kulisimamia Zanzibar ya kesho ndugu zetu itakuwa ni nchi ya matumaini. Ninarudia tena ndugu zangu kuwaambia tukitamani Zanzibar, tukielewana milango ya neema Mwenyezi Mungu taifungua.

Nitawapa siri, sitotaja jina la mtu. Kuna rafiki yangu mmoja nilizungumza naye jana kutola Cyprus alikuwa anasoma magazeti akaniuliza ninasikia Hoja ya kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa inajadiliwa? Nikamwambia ndio na kwa mwelekeo ninavyouona tutaelewana hoja hiyo kwa kupelekwa kwa wananchi, akasema alhamdulillah ninaona mwanga wa matumaini. Akaniambia

wapo wawekezaji ambao walikuwa wanasita kuja Zanzibar kwa hali yetu hawaamini, lakini tukifikia hapo kaniahidi. Moja ya jambo ambalo si vibaya kutoa siri, anasema wanafikiria fikiria pengine kutoa msaada katika kuuendeleza Uwanja wa Ndege wa Zanzibar.

Sasa ninasema fedha, mitaji vina hulka ya ndege mmoja anayeitwa njiwa. Njiwa ukimuona anaishi mahali kuna watu wema na hakuna vurugu. Njiwa kwenye vurugu hakai. Fedha na mitaji ni hivyo hivyo. Kama kweli tunataka kuvutia mitaji tuache mambo haya tuelekee kwenye amani na utulivu na bila shaka nchi ya matumaini itakuwepo.

Mhe. Spika**,** sasa naomba natamka rasmi kuwa Baraza lako Tukufu baada ya nasaha hizo, liakhirishwe hadi tarehe 24 Machi, 2010 saa 3.00 asubuhi.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri Kiongozi kwa hotuba na nasaha alizotupa hapa. Baada ya kazi kubwa muliyoifanya tangu tulipoanza shughuli yetu hii mnamo tarehe 20 mwezi huu.

Ninashukkurani kwa mashirikiano makubwa katika kuifanya kazi hiyo na kunisaidia sana katika kuendesha shughuli hii. Mwenyezi Mungu atujaalie tuendelee kushirikiana kiasi hicho kutimiza wajibu wetu wa shughuli zetu kama Wawakilishi wa wananchi.

Ninakushukuruni sana.

Nikumbushe tu kwamba mara baada ya kuahirisha Mkutano huu wa Baraza, baada ya kuwahoji tutasikiliza ule muziki wetu wa taifa kama hatutokwenda sambamba na muziki utakavyochezeshwa, bora tunyamaze kimya ili tusije tukawa na sauti tofauti.

Baada ya hapo nitawaaga na tunakwenda zetu.

((Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 2:15 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 24/03/2010 saa 3: 00 asubuhi)